# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Hamsini na Moja-Tarehe 18 Juni, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huu ni Mkutano wa Kumi na Moja na hiki ni Kikao cha Hamsini na Moja, kwa hiyo, naomba sasa nimwite Katibu aweze kutuongoza kwenye ratiba ya shughuli za leo.

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, leo tunaanza na ajenda ya maswali moja kwa moja, swali la kwanza linakwenda Ofisi ya Waziri Mkuu.

Na. 410

**Upungufu wa Walimu na Vitendea kazi kwenye Sule za Msingi Vijijini**

**MHE. RAMADHAN HAJI SALEH** aliuliza:-

Shule za msingi hasa za vijijini zimekuwa na upungufu wa vitendea kazi kama vile vitabu, Walimu na nyumba za kuishi Walimu.

Je, ni lini Serikali itachukua hatua za makusudi za kuondoa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa fedha za uendeshaji *(capitation grant)* kwa kila shule ambapo asilimia 50 kwa shule za sekondari na 40 kwa shule za msingi na fedha hizi hutumika kununua vitabu. Mwaka 2012/2013 hadi mwezi Aprili, 2013, Serikali imepeleka fedha za *capitation* katika Halmashauri zote nchini shilingi bilioni 82 zikiwemo shilingi bilioni 60 kwa shule za msingi na shilingi bilioni 22 kwa shule za sekondari, vitabu vya shilingi bilioni 76.4 vimeanza kusambazwa katika shule mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuwaajiri na kuwapanga Walimu wapya katika shule za msingi na sekondari kila mwaka kadiri wanavyohitimu na kulingana na uwiano wa mahitaji ya Walimu katika Halmashauri. Hadi mwezi Desemba, 2012, katika shule za msingi walikuwepo Walimu 171,986 na katika shule za sekondari walikuwepo waliomu 51,469. Mwaka 2013, Serikali imeajiri Walimu 27,693 wakiwemo wa shule za msingi 13,633 na wa shule za sekondari 14,060. Aidha, ili kuwa na uwiano sawa wa Walimu katika shule, Wakurugenzi wa Halmashauri wameagizwa kuwapanga Walimu wapya maeneo ya pembezoni yenye upungufu na kusawazisha ikama ili kuondoa mlundikano maeneo ya mjini na katika shule zilizo kandokando ya njia kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo dhamira ya kukabiliana na changamoto ya nyumba za Walimu vijijini na maeneo ya pembezoni. Katika kutekeleza azma hii, mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi katika Halmashauri 40 zilizobainishwa kuwa na mazingira magumu ambapo kila Halmashauri itapata shilingi milioni 500. Aidha, Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba

za Walimu kupitia programu za *MMEM* na *MMES* na kupitia ruzuku ya maendeleo katika mamlaka za Serikali za Mitaa (*LGCDG*).

**MHE. RAMADHAN HAJI SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na nina swali moja tu la nyongeza. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie kwamba kwa mwaka huu wa 2013/2014, ni nyumba ngapi wamepanga kuzijenga nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotengwa kwa ajili ya kazi hii kwa mwaka 2013/2014 ili niweze kutoa picha kamili ni shilingi bilioni 20 na kila Halmashauri ambayo imepata fedha hizi, imetengewa shilingi milioni 500, yaani nusu bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno mengine tunachozungumza hapa, Halmashauri ambazo zimepata fedha hizi ni 40 na vigezo vilivyotumika hapa ili wasije wakasimama watu wengi humu ndani, ni pamoja na kuangalia wale ambao wako katika mazingira magumu kama Mheshimiwa Haji mwenyewe alivyoulizia swali hili. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba akitumia shilingi milioni 500 katika Halmashauri kwenye nyumba za Walimu, yeye kama atatumia na nguvu za wananchi kule wakasaidiana, wakakaa wakaangalia jinsi ya kuzitumia hizi fedha wanaweza wakajenga nyumba nyingi, lakini ninachotaka kusema hapa, Halmashauri ambazo zimepata sasa fedha hizi shilingi milioni 500 ni 40 ambazo zinatupeleka kwenye bilioni 20.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Shule ya sekondari ya Lugalo iliyoko katika Manispaa ya Iringa, Jimbo la Iringa Mjini, ni kati ya shule ambazo zinafundisha watoto wenye uhitaji maalum, yaani watoto wenye ulemavu wa macho (kutoona) na ulemavu wa ngozi. Shule hii imekuwa ikikabiliwa na upungufu mkubwa sana wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia pamoja na Walimu. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fungu katika shule

hiyo ili watoto hawa wapate haki yao ya msingi ya kupata elimu bora? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *issue* anayoisema ya Lugalo, mimi nimefika Iringa, Mheshimwa Ritta anajishughulisha sana na maendeleo ya Manispaa ya Iringa na ninapenda kumpongeza sana hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba hivi vitu vyote anavyovizungumza hapa vinaingia katika fedha ambazo zinapelekwa kama *capitation* na fedha zile ambazo tumepeleka kama chenchi ya Rada, vyote hivi katika nchi nzima tunatumia kama shilingi bilioni 100. *I am quite sure* kwamba angenipa nafasi nikaenda nikaa vizuri nikafanya mchanganuo, nitakuta hata hiyo shule yake anayoizungumza ipo, kwa sababu kwa upande wa madawati anayozungumza ni kama kila shule katika Halmashauri zote hizi zitapata, nitajibu katika swali lingine linalokuja.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Nilitaka kujua Serikali je ilishafanya tathmini kujua uhitaji wa vitabu ili tumalize kabisa tatizo la vitabu, ni vitabu vingapi vinahitajika na vinagharimu kiasi gani na kwa sababu tuko kwenye bajeti tuweze kumaliza kabisa tatizo hilo na tusiongelee tena kuhusu vitabu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa idadi hapa tutapata shida kidogo kwa sababu kuna fedha nyingine zinakwenda kununua Kamusi na wale ambao wamepewa kazi hii ya kununa vitabu hivi watakuja na bei tofauti tofauti. Kwa ajili ya ku-*capture* hii *point* anayoizungumza Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, ukiangalia katika hesabu zetu, vitabu pamoja na madawati, sasa vitabu kwa sababu ameulizia vitabu, vinakwenda kwenye shilingi bilioni 76.4, ndizo ambazo zitakazokuwa zimetengwa. Sasa nilipokaa na wataalam wangu wakati nilipojaribu kutafuta idadi, tulipata tabu kidogo kwa sababu

kuna wengine watakuja na bei tofauti tofauti, kwa sababu siyo mtu mmoja ambaye atafanya kazi hii ya ku-*supply*, lakini awe na hakika tu kwamba, Iramba nayo itakuwa *considered* na hakutakuwa na matatizo.

**MWENYEKITI**: Nakushukuru. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata, lakini kabla hatujaendelea Mheshimiwa Naibu Waziri nikuombe sana ili kuondoa maswali ya namna hii tena, hiyo orodha ya Halmashauri 40 ambazo zitapatiwa hizo shilingi milioni 500 kwa kila Halmashauri, itakuwa vizuri sana kabla Bunge hili halijaisha, Waheshimiwa Wabunge wapatiwe orodha hiyo waweze kujua ni Halmashauri zipi kusudi itakapokuja mgao mwingine wajue tunaendeleaje, ni kitu cha msingi sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 411

**Uwekaji wa Vifaa kwenye Maabara ya Kituo cha Afya**

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Magu imekamilisha ujenzi wa maabara katika Kituo cha Afya kwenye Mji mdogo wa Kabila:-

Je, ni lini sasa Serikali itachangia nguvu za wananchi na Halmashauri ya Wilaya kuweka vifaa vya maabara na samani ili ianze kutoa huduma bora zaidi kwa Tarafa nzima ya Ndagalu na vijiji vya Wilaya ya jirani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Magu imefanya ukarabati wa chumba cha maabara katika Kituo cha Afya Kabila katika mwaka wa fedha 2009/2010 na jumla ya shilingi milioni 26.086 zilitumika kupitia fedha za Mfuko wa Pamoja wa Ukarabati *(Joint Rehabilitation Fund)*. Serikali imepeleka vifaa vya maabara pamoja na Mtaalam wa Maabara katika Kituo cha Afya Kabila na tayari maabara hiyo imeanza kufanya kazi tangu mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vilivyopelekwa katika Kituo cha Afya cha Kabila ni pamoja na darubini moja ya kisasa, vipimo vya haraka vya kupima malaria (*MRD*), vitendanishi vya kupimia malaria (*MRDT*), choo na wingi wa damu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali imetenga na kutumia jumla ya shilingi milioni 27.6 kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya *(Health Basket Fund)* na shilingi milioni 9.5 kupitia fedha za dawa kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwenda Bohari ya Serikali ya Dawa (*MSD*) kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara na vitendanishi kwa maabara saba zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Magu ikiwemo maabara ya Kituo cha Afya cha Kabila. Kituo cha Afya cha Kabila kimepata shilingi milioni 3.43 kutoka Mfuko wa Pamoja wa Afya (*Heath Basket Fund)* na shilingi milioni 2.556 kutoka Bohari ya Serikali ya Dawa (*MSD*) kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo hiki cha Afya cha Kabila ni muhimu sana kwa sababu kinahudumia Tarafa nzima ya Ndagalu yenye Kata nne lakini pia kinahudumia wagonjwa kutoka Wilaya ya Kwimba na Maswa. Jibu la Serikali linaonyesha jinsi gani Serikali inajali na imefanya makubwa katika kuimarisha Kituo hiki cha Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ikumbukwe kwamba Serikali ilikipelekea Kituo hiki cha Afya *ambulance*. Kwa hiyo, napongeza sana juhudi za Serikali ikishirikiana na juhudi za Mbunge katika kuimarisha huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Makamu wa Rais alikwenda kufungua jengo kwa ajili ya *theater* (chumba kidogo cha upasuaji) na kimekamilika na sasa chumba kile hakijapata huduma muhimu ili kiweze kufanya kazi inayokusudiwa kwa ajili ya wakazi wa Tarafa nzima na wa Wilaya hizi mbili nilizozitaja. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kushirikiana nami katika kuangalia mahitaji halisi kwa ajili ya chumba hiki cha upasuaji ili kiweze kuhudumia watu wengi niliowataja wa Tarafa hii na Wilaya za jirani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, swali limehama kutoka maabara sasa kwenda kwenye chumba cha upasuaji.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kukiri mbele yako kwa sababu Magu mimi nimekwenda kule, ni kweli Mheshimiwa Dokta Festus Limbu ame-*devote* muda wake mwingi na amejaribu sana kuona kwamba kituo hiki kinafanya kazi kwa kiwango cha hali ya juu sana. Kwa hiyo, napenda kumpongeza, *it is my judgment* kwamba *the Member of Parliament is the very serious*, anafanya kazi nzuri sana pale na ndiyo maana unaoana hata na sisi kama Serikali anaona kwamba tumesaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili eneo ambalo analizungumzia, wao walikwenda wakaomba mkopo unaopitia katika Bima ya Afya ya Taifa (*NHIF*), wakapata kama shilingi milioni 89 ambazo zilitumika kwa ajili ya kupata mashine za kufulia nguo. Bahati nzuri nilipo-*check* na hawa jamaa imeonyesha kwamba wameshamaliza hiyo ungwe na tayari wameshalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hicho chumba cha upasuaji anachokisema ni kidogo, watahitaji kama shilingi milioni 55 na sisi kwa sababu ya *trend* na *pattern* ya namna walivyolipa pale, tuna *endorse* kwamba ni sawasawa wanaweza wakaendelea kufanya hivyo. Kwa hiyo,

tutakachofanya hapa tutasaidiana na kushirikiana na wao kuhakikisha kwamba hizo shilingi milioni 55 zinapatikana na ningeomba wenzetu wengine waige mfano wa Magu, hizi fedha zitapatikana kwa ajili ya chumba hicho cha upasuaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya nilikuona na hakuna Mbunge mwingine aliyesimama kipindi hicho, kwa hiyo, huyo atakuwa muulizaji swali wetu wa mwisho.

**MHE. ESTER A. BULAYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kampeni za Urais, Rais wetu, Mheshimiwa Dokta Jakaya M. Kikwete, alikuwa ameahidi kuwapa *X-ray* kwenye Hospitali ya Wilaya ya Bunda, ambacho kilikuwa Kituo cha Afya cha Manyamanyama. Sasa nilitaka kujua, ahadi hiyo itatekelezwa lini na ukizingatia hospitali hiyo imeshapandishwa hadhi na inatoa huduma kwa wananchi siyo wa Bunda tu, hata wa Musoma Vijijini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hatuna tabia ya ku-*debate* kuhusu habari ya ahadi iliyotolewa na Rais yaani huwa haipo katika utaratibu wetu, Rais akishatoa ahadi mahali ni maelekezo na hatutoki tena tukamfuata Rais tukamwambia Rais, fedha zile za Bunda ziko wapi, hatufanyi hivyo. Sisi tunachofanya ni kwamba yeye kama Mwenyekiti anayesimamia mambo ya bajeti yote, ikishapita, sisi sasa kama Halmashauri tunakwenda kukaa na TAMISEMI kuona kwamba ni kwa namna gani tutakavyopeleka hizi fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niseme tu kwamba, kwanza kabisa nikiri, kama kuna ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais itatekelezwa tu. Mheshimiwa Rais ameahidi kwa kipindi cha miaka mitano, kwa hiyo, nitafuatilia jambo hili kwa karibu sana kwa sababu watu wangu mimi kule nilishawaweka, wakati najibu hapa kule wanaandika, ili nikitoka hapa na barua itakwenda kule. Kwa hiyo, siyo

kwamba tunatoa majibu tu, wao kule wanaandika na wanaanza kuwasiliana na Bunda na Bunda nao wananisikiliza. Kwa hiyo, nitakwenda kusimamia jambo hilo ili kuona ahadi hiyo ya Rais inatekelezwa. Hapa ndani tumeshaleta orodha ya ahadi zote zilizotolewa na Rais, nitakwenda ku-*check* tena kwenye ile orodha iliyoletwa Bungeni. Mheshimiwa Bulaya asiwe na wasiwasi nitatekeleza jambo hili, hii ikiwa ni pamoja na jitihada za Mheshimiwa Wasira. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante kwa majibu. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa James Mbatia.

Na. 412

**Kushuka kwa kiwango cha Elimu Wilaya ya Kigoma**

**MHE. JAMES F. MBATIA (K.n.y. MHE. MHONGA S. RUHWANYA)** aliuliza:-

Wilaya ya Kigoma ina Walimu 1981 kati yao Walimu wa kiume ni 1273 na Walimu wa kike ni 708, Wilaya ina upungufu wa Walimu 563 pia liko tatizo la upungufu wa madarasa, madawati, ukosefu wa maabara, hakuna nyumba za Walimu, matatizo ambayo huchangia kushuka kwa kiwango cha elimu katika Wilaya hiyo.

Je, Serikali inasema nini katika hali kama hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya

Kigoma hadi kufikia Mei, 2013, ina jumla ya Walimu 2,965 wakiwemo wa shule za msingi 2,441 na shule za sekondari 524. Mwaka 2013, Serikali imeajiri Walimu 27,693 kati yao Walimu 416 walipangwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma. Serikali itaendelea kuajiri Walimu na kuwapanga kadri wanavyohitimu na kufaulu. Halmashauri inashauriwa kuwapanga Walimu wapya katika shule zenye upungufu zikiwemo shule za sekondari za Mkabogo na Lagoso na shule ya msingi ya Kapalamsenga na Lubalisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mipango ya *MMES* na *MMEM*, Serikali ina mikakati ya kuboresha elimu ya msingi na sekondari ili kuondokana na changamoto mbalimbali. Hadi kufikia mwaka 2015, Serikali itakarabati na kukamilisha kwa awamu shule za sekondari 1,200 kwa kiwango cha kuwa na miundombinu yote muhimu ikiwemo maabara, madarasa, nyumba za Walimu, maktaba, vyoo, umeme na maji. Utekelezaji wa awamu ya kwanza umeanza kwa shule 264 kwa gharama ya shilingi bilioni 56.3 zikiwemo shule za sekondari Nyarubanda na Kalinzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hutenga fedha na kupeleka katika Halmashauri kwa ajili ya miundombinu mbalimbali ikiwemo madarasa, maabara, madawati na ukarabati wa shule kongwe. Kati ya mwaka 2009 na 2013, Serikali imetoa shilingi bilioni 39 kupitia mipango ya *MMEM* na *MMES*, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma imepokea shilingi milioni 377 zikiwemo za maabara shilingi milioni 104, nyumba za Walimu shilingi milioni 173 na madawati shilingi milioni 73. Mwaka 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma imetengewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu na itanufaika kwa kupata madawati yatakayonunuliwa nchi nzima kwa shilingi bilioni 23.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma iko kwenye mazingira magumu, kwa mfano shule ya msingi Reli Mpya, Kata ya Nguruka, iko kwenye mazingira ambayo ni tete sana. Kwa kuwa Sera ya sasa hivi ya Elimu ni

kuchanganya elimu ya msingi na sekondari kuwa ndiyo elimu msingi na mahitaji ya Mheshimiwa Waziri kwenye jibu alilojibu hapa ni kwamba fedha hizi zitawekwa kwenye shule hizi za Kigoma sasa.

(a) Je ujenzi huu na shule hizi zikienda kwa pamoja wakati Sera ni mpya yenye mazingira mapya, Waziri haoni kwamba tunatawanya rasilimali hizi badala ya kusubiri Sera mpya ili twende na mfumo unaostahili?

(b) Kwa kuwa Halmashauri ya Kigoma iko kwenye mazingira magumu kwenye utendaji wa Walimu na hasa Walimu wa masomo ya sayansi. Ili kuweza kumfanya Mwanakigoma aweze kuwa na uelewa wa kujitambua na kutawala mazingira yake, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Walimu wa sayansi na wenye uelewa wa kutosha wanapelekwa kwenye shule zote za Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimempata vizuri, mimi ninachojua hapa ni kwamba tunaleta mipango ya Serikali, kama lilivyopitisha Bunge hapa. *Much as I appreciate* mawazo aliyonayo Mheshimiwa Mbunge, kwa maana kwamba kuna *development*s hapa katika ambazo zimetembea ambazo zinasema labda tutahitaji kuangalia tena upya jambo hili, mimi ninacholeta hapa ni bajeti ya Serikali. Bajeti ya Serikali ni mpango wa Serikali unaoonyesha namna hela zitakavyopatikana na namna zitakavyotumika. Kwa hiyo, hizi hela sisi tunazipeleka Kigoma na hao wenzetu wa Kigoma kama wana mawazo ambayo yata-*accommodate* hili analozungumza Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, ambaye ni Mbunge pia hapa, *well and good,* hatutakuwa na matatizo lakini hii sasa ni lazima ipite tena upya katika utaratibu unaotakiwa. Halmashauri lazima ikakae, iseme kwamba kwa sababu hizi tulizozieleza hapa, tunafikiri kwamba sisi kuna haja ya ku-*hold* hizi hela kwanza, zisifanye kazi mpaka baadaye, hiyo lazima ipite katika *Regional Consultative Committee.* Ikitoka *Regional Consultative Committee,* itakuja Makao

Makuu kwa maana ya TAMISEMI na ile sheria inasema Katibu Mkuu *in collaboration* na Katibu wa Hazina, wako hapa wananisikia, wataafikiana kuhusu huo mchakato ambao nimeueleza hapa. Sasa mimi hapa kusema *okay* sasa *hold* hizo hela, Mkuu wa Serikali yuko hapa ananisikiliza ataniambia wewe umetoa wapi hicho kibali cha ku-*hold* hapa, hilo ndilo tatizo nitakalolipaa hapa. Mimi ninajibu kile ninachokijua cha Serikali, kama kuna mawazo mengine mapya yakija hapa mimi nitajibu hicho kitakachosemwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu Walimu, ni kweli anachosema Mheshimiwa Mbatia. Katika shule zote wakisimama Wabunge hapa, watakuambia hakuna Walimu wa hesabu, *physics, chemistry,* Kiingereza na Kiswahili pia huwa tunapata matatizo. Kama tungekwenda vizuri na wasingekuwa Walimu wanakufa, *by the year* 2015, tungekuwa tumemaliza hili tatizo analolisema Mheshimiwa Mbatia kwa asilimia 100. Mpango uliopo ni huu wa kudahili Mheshimiwa Kassim Majaliwa kila siku anajibu hapa na kuhakikisha kwamba idadi yetu imeongezeka na kuweka mikondo mingi katika hilo eneo la sayansi ambalo tunakiri sisi wote kwamba linaonekana lina matatizo. Ninakubalibna na hoja yake. Kwa sasa hivi hapa mpaka kufikia mwaka 2014 tumepunguza tatizo la Walimu katika nchi yetu kwa asilimia 90. Tutachukua mawazo ya Mheshimiwa Mbatia, *you have a valid point,* ni kweli hata ukienda katika *performance* matatizo makubwa ni katika masomo ya sayansi. Nilikuwa ninajibu hili kwa sabahu ni kitu *sensitive,* sasa mkiniambia vinginevyo basi ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Diana Chilolo, swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa upungufu wa vitabu katika shule zetu za misingi, vilevile unasababishwa na masomo kuwa na vitabu vingi. Kwa mfano, somo moja tu la Kiswahili, Darasa la Tatu, unakuta lina vitabu aina tano. Mkoa wa Mwanza wanatumia kingine, Mkoa wa Singida wanatumia vingine na Mikoa mingine hivyo hivyo, suala ambalo linawafanya wanafunzi

washindwe kujua ni kitabu gani hasa kinachotakiwa katika somo husika na kuwafanya Walimu Wakuu wawe na mzigo mkubwa wa kununua vitabu vingi bila zozote za msingi. Je, ni lini Serikali itaondoa vitabu hivi na kutoa kitabu kimoja kimoja kwa kila somo ili kuwarahisishia wanafunzi na Walimu wao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Diana lakini huko nyuma Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, mwaka 2010, aliagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi tuanze mchakato wa kuwa angalau na kitabu kimoja ama vitabu viwili vya kiada, kwa ajili ya shule za msingi na zoezi hilo linaendelea. Hata katika hizi fedha za Rada ambazo mchakato wake unaendelea na mwishoni mwa mwaka huu tutaanza kugawa vitabu hivyo. Tumefuata maagizo ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na vitabu viwili vya kiada.

Na. 413

**Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Musoma**

**MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MHE. AMINA NASSORO MAKILAGI)** aliuliza:-

Serikali imeonyesha nia yake ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kwangwa Mjini Musoma:-

Je, ujenzi wa Hospitali hiyo utaanza lini na kiasi gani cha fedha kinategemewa kutumika kwa ajili hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo ya kujenga Hospitali ya Rufaa katika Mkoa wa Mara yaliibuliwa na wananchi mnamo mwaka 1975 na mchakato wa ujenzi wake ulianza rasmi 1980. Ulipofika mwaka 1985, ujenzi ulisimama kutokana na matatizo ya kifedha yaliyojitokeza katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010, Uongozi wa Mkoa wa Mara kupitia kikao cha Kamati ya ushauri ya Mkoa kilichofanyika tarehe 21 Mei, uliamua kuendeleza ujenzi wa Hospitali hiyo kwa ruzuku ya Serikali na uhisani wa wadau mbalimbali kwa kutilia maanani kwamba Mkoa hauna Hospitali ya Rufaa na mahitaji ya Mkoa ya kuwa na Hospitali ya Rufaa yanazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara ilitenga shilingi milioni 100.997 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi waliopisha eneo la ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mkoa umeidhinishiwa shilingi bilioni 2.16 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ambapo kati ya fedha hizo shilingi milioni 155.2 ni kwa ajili ya fidia kwa wananchi ambao walikuwa hawajalipwa fidia na shilingi bilioni mbili (2) ni kwa ajili ya ujenzi. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mkoa umeidhinishiwa shilingi bilioni 2.16 kuendeleza ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ambazo zimefanyika mpaka sasa ni pamoja na kuwalipa fidia wananchi waliopisha eneo la mradi, kumpata mkandarasi kwa ajili ya kujenga uzio na kumpata Mashauri Mwelekezi yaani (*Consultant)* ambaye ni *M/s. SR Consultant Ltd* wa Dar es Saalam, kwa sasa Mkoa upo kwenye hatua za mwisho za kumpata Mkadarasi. Mshauri Mwelekezi tayari ameandaa michoro ya majengo na makisio ya gharama za ujenzi ambazo zinakisiwa zitakuwa ni shilingi bilioni 37.4.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ninasikitika, wananchi wa Mkoa wa Mara wanaokipenda Chama cha Mapinduzi, kabla hata sijazaliwa tangu mwaka 1975 wameona umuhimu wa kujenga Hospitali

ya Rufaa. Ujenzi umesimama, nina miaka mitano mwaka 1985 na mpaka leo hii hakijajengwa. Waziri anasema mwaka huu zimetengwa fedha, lakini mwaka 2012 katika jumba hilihili, Serikali ilitenga shilingi bilioni 2.0 lakini hazikwenda. Swali langu, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kujenga Hospitali hii ya Rufaa, ili mama zangu kule Mara wasifie njiani wakiwa wanaenda katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wakati tunapewa semina na *MSD*, *graph* zilionyesha kabisa, kati ya Mikoa ambayo ina upungufu wa vifaa vya tiba na dawa ni Mkoa wa Mara. Sasa nilitaka kujua, ni lini Serikali itamaliza tatizo la kutoa dawa za kutosha na vifaa tiba katika hospitali zote na Zahanati na Vituo vya Afya vya Mkoa wa Mara?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu mafupi lakini kwa fasaha, usichukue muda mrefu sana kujibu maswali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazingatia maelezo yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka niwape picha kamili hapa. Kwa mwaka 2013/2014, ukichukua hela zote zilizotengwa kwa ajili ya *Regional Secretariet (RS),* ni shilingi bilioni 10.9 na hela ambazo zimepangwa sasa hivi tunavyozungumza hapa ni shilingi bilioni 9.7 na hizi takwimu ambazo Mheshimiwa Bulaya amezitoa hapa ni sahihi kabisa lakini wakati ninakuja hapa asubuhi ya leo, nime-*check* na watu wangu kuhakikisha kwamba hizi hela ambazo zilikuwa zimetamkwa zimekwenda. Wale wasingeweza wakamwita mpaka *Consultant,* akafanya haya yote niliyoyaeleza hapa kama zile hela zisingekuwa zimekwenda kule na ile ungwe ya mwisho nimei-*check,* Mheshimiwa Bulaya unaweza ukaja uka-*chek* na sisi, hela hizi zimekwenda. Ninajua anachokisema hapa kwamba ni toka akiwa mdogo, mimi nimekwenda pale nikashanga, *that is a very ambitious project* ni mradi mkubwa, Waheshimiwa Wabunge mkienda kule mtashangaa.

Hela zinazotakiwa hapa kwa ajili ya kazi hiyo, kama tukiamua kutoa hapa hizi hela ili tusikilize hiki kilio ambacho anasema toka akiwa mdogo, ni shilingi bilioni 37.4, ninazipata wapi? Mimi ninachoweza kusema hapa, tuiagize Sektretarieti ambayo imekuwa inafanya kazi nzuri, ili-*arrange priorities* zao. Mwaka uliopita shilingi bilioni tisa, mwaka huu shilingi bilioni 10 zimekwenda kwenye *Regional Secretariet*, kwenye *Development* shilingi 3.5 bilioni na ile ya mwaka 2012 ni shilingi 2.5, acha zile za mishahara na mambo mengine, tukiziangalia hizi pamoja na wale wapenzi wote waliopo pale, tunaweza tukawaondoa wenzetu hapa awamu kwa awamu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Swali linalofuata. Hakukuwa na mtu aliyesimama kwenye swali hili la msingi kwa ajili ya swali la nyongeza. Sasa tunaenda Wizara ya Ujenzi na swali linaulizwa na Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa.

Na. 214

**Barabara ya Kutoka Mpili – Mlimba Kufanywa ya Mkoa**

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA** aliuliza:-

Barabara ya kutoka Mtili – Ifwagi – Mdaburo – Lulanda – Mpanga Tazera – Mlimba inaunganisha Mkoa wa Iringa na Morogoro na kuna shughuli nyingi za kiuchumi kwenye maeneo hayo kama vile kilimo cha chai, misitu ya mbao, mazao ya chakula na biashara na shughuli za utalii:-

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuifanya barabara hiyo kuwa ya Mkoa ili iweze kuboreshwa na kupitika mwaka mzima kuliko ilivyo sasa ambapo Halmashauri haina uwezo wa kutosha kuitengeneza?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufundi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyojibu Swali Nambari 279, la Mheshimiwa Selemani Said Jafo tarehe 27 Mei, 2013 katika Mkutano huu, utatraribu wakupandisha hadhi barabara umeainishwa katika Sheria ya Barabara Na.13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huo unahitaji mapendekezo yaanzie katika Halmashauri husika na ikiridhika yapelekwe katika Bodi ya Barabara ya Mkoa ambayo ikiridhika itawasilisha mapendekezo hayo kwa Waziri mwenye dhamana ya Ujenzi. Hivyo, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge kufuata utaratibu huo. Aidha, kwa vile Halmashauri hupata fedha pia kutoka Mfuko wa Barabara *(Road Fund),* ninamshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri husika ili fedha kutoka Mfuko huo wa Barabara zitumike ipasavyo katika matengenezo ya barabara hiyo.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kidogo na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini kuna jambo la msingi hapa. Ni miaka mitano mfululizo tumekuwa tunaomba ile barabara ipandishwe hadhi na vikao vya msingi vimeishafanyika lakini Serikali haionyeshi kama ina nia ya dhati ya kutaka kuhakikisha kwamba ile barabara inapandishwa hadhi, ambayo ina urefu wa kilometa 116. Lile eneo ni nyeti, kuna viwanda vya chai, mbao zinatoka pale na kuna wakulima wengine wadogo wadogo, wanaendelea kupata shida, ile hela inayotolea kwa ajili ya *Road Fund* ni ndogo. Swali la kwanza, tunataka tamko la Serikali, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, haina uwezo, je, Serikali iko tayari kuongezea kidogo ile hela inayokwenda kwenye *Road Fund* kwa ajili ya kuhakisha ile barabara inatengenezwa? *(Makofi)*

Mhehimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kijiji cha Mpanga Tazera, kiko mwishoni kabisa kwenye reli. Walikuwa wanategemea kabisa kutengenezwa kwa ile barabara ndiko kungeweza kukawasaidia wale wananchi ile. Kuna tatizo la msingi limezuka hapa katika, kuna wakulima wengi na maisha yao wanayaendesha kutokana na kililmo. Cha kusikitisha ni kwamba Serikali hii, kupitia Wizara ya Uchukuzi, wamekataa

kuchukua mzigo zaidi ya kilo 300, imekuwa ni kero na wananchi mazao yao ya kilimo yanaoza kila siku, kwa hiyo hali zao zinazidi kuwa mbaya. Ninaomba tamko la Serikali hapa, watatusaidiaje kuhakikisha wanachukua zaidi ya kilo 300 katika eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mgimwa namna anavyofuatilia maendeleo ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongeza fedha za Mfuko ili kuweza kutengeneza barabara anayoisema, katika mwaka huu wa fedha, Mfuko wa Barabara umetengewa shilingi bilioni 300 na mwaka unaofuata ni shilingi bilioni 353, kwa maana ya zile barabara zinazohudumiwa na Wizara ya Ujenzi. Katika barabara hizi, tumeweka mgao, kuna barabara ambazo ni za Mkoa na za Wilaya, barabara za Wilaya wanapata asilimia 30 ya Mfuko huu na zile barabara za Serikali Kuu ni asilimia 70. Kila mwaka huwa tunaweka mpango wa matengenezo, kwa hiyo, inabidi Wilaya husika ifanye vipaumbele ni barabara ipi muhimu waanze kuitengeneza kulingana na fedha ambazo zitakuwa zimetengwa. Kwa hiyo kama barabara hiyo anayoisema kwa maana ya Wilaya ya Mufindi wataona ni ya muhimu wa kwanza basi wataainisha ni maeneo yapi waanze kuyatengeneza. Ndiyo maana tunasema kwamba Waheshimiwa Wabunge masuala haya ya barabara kupanda hadhi, ni vizuri tukaanzia pale kwenye Bodi za Barabara za Mikoa ambapo tunaweka vipaumbele vya barabara zetu tulizonazo kulingana na mtandao wa barabara uliopo katika Mkoa husika. Tuweke *priority* yetu, barabara hii inaleta uchumi zaidi, basi tuipe matengenezo na tuipe fedha zaidi ili kuweza kufungua barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kijiji anachokizungumza ambacho kiko kwenye reli, mimi nafikiri suala hili wacha nilichukue, tutaongea na Waziri wa Uchukuzi, tuone ni kwa namna gani wanaweza wakalishughulikia.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali

moja la nyongeza. Barabara hii inaunganisha barabara inayotoka Sawala kuja Mafinga. Ukifika Mafinga ni mji ambao unaunganishwa na barabara nyingi kutoka katika Kata mbalimbali lakini Mafinga pale hatuna stendi kabisa na wananchi wanapata shida sana kutokana na tatizo la stendi. Ile stendi ya Mafinga ndiyo inayounganisha barabara kuu inayoenda Mbeya. Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akatuhakikishia ni lini *stand* ya Mafinga inaweza ikajengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ingawa swali hilo ni jipya, limehama kutoka kwenye barabara kuja kwenye stendi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kujenga stendi ni suala ambalo linabidi lishughulikiwe na Halmashari husika. Sisi tunashughulikia matengenezo ya barabara kuu na barabara za Mikoa. Kwa hiyo, kama ni ushauri tutaendelea kuwasiliana naye ili tuweze kuona ni eneo lipi linalofaa ili waweze kujenga stendi hiyo.

Na. 415

**Miradi ya Ujenzi kuwa Chini ya Kiwango**

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS** aliuliza:-

Kuna ongezeko kubwa la wakandarasi wa miradi ya ujenzi kujenga chini ya kiwango na kusababisha hasara kwa Taifa:-

(a) Je, Serikali inatambua tatizo hilo?

(b) Je, hali hiyo husababishwa na nini wakati kuna Wahandishi Washauri?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mbunge wa Chonga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza si kweli kuwa kuna ongezeko la Wakandarasi wa miradi ya ujenzi kujenga chini ya kiwango. Miradi ya ujenzi wa barabara inatekelezwa kulingana na viwango vya ubora vinavyoainishwa kwenye mkataba. Kwa sasa Wizara ya Ujenzi inatekeleza miradi mingi ya ujenzi wa barabara ambayo kati ya hiyo miradi mingi imekamilika kwa viwango vinavyotakiwa. Ipo miradi michache imeonekana kutekelezwa chini ya viwango vilivyokubaliwa katika mikataba husika. Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) imekuwa ikichukua hatua stahiki pindi inapotokea miradi ya barabara kutekelezwa chini ya viwango vilivyokubaliwa kimkataba.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, wajibu wa Mkandarasi kwenye miradi ni kuhakikisha kazi inafanyika kulingana na viwango vinavyokubalika kimkataba na wajibu wa Mhandisi Mshauri ni kuhakikisha Mkandarasi anatekeleza wajibu wake kimkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza katika sehemu ya kwanza ya swali hili, katika miradi michache kumejitokeza baadhi ya kazi kutokidhi viwango vya mikataba kutokana na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na upungufu ya usanifu, ukosefu wa uaminifu na uzembe wa makandarasi na Wahandishi Wasimamizi. Upungufu huo uliojitokeza unashughulikiwa kulingana na vipaumbele vya mikataba ya ujenzi kwa Makandarasi na mikataba ya usanifu na usimamizi kwa Wahandisi Washauri ikiwa ni pamoja na kurudiwa kwa kazi zisizokidhi viwango kwa gharama zao wenyewe pamoja na kufukuzwa.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya kisiasa zaidi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe makini kabisa wa Kamati ya Miundombinu ambayo inasimamia sekta hii na tumeshuhudia hapa barabara nyingi zinazojengwa zinaharibika kabla ya *life span* yake kukamilika pamoja na nyumba kujengwa na kuporomoka. Sasa nataka

Serikali itujibu kwamba ni vigezo gani Serikali inatumia hata ikatoa majibu haya kwamba miradi inajengwa kwa kiwango kinachostahili? Ni vigezo gani Serikali inavyotumia hata kuyasema majibu haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, je, sasa Serikali itakuwa tayari kuishirikisha ipasavyo Kamati ya Miundombinu katika kukagua miradi hii ya ujenzi ili kupata *value for money* kwa sababu tumekuwa tukiona miradi takribani yote inajengwa chini ya kiwango isipokuwa miradi ya *MCC* tu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba miradi michache imeonekana imejengwa chini ya kiwango na hatua stahiki zimechukuliwa. Sasa tukisema miradi michache basi ndiyo miradi mingi, hiyo ni suala la tafsiri la Mheshimiwa Haroub ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati hii ya Miundombinu. Kwa taarifa zetu ni miradi michache na hii michache tumesema sababu zipi zinatokea kwa sababu hata katika usanifu, unasanifu barabara kwamba iweze kudumu kwa miaka 20 lakini akakosea baadhi ya vigezo vya kuchanganya labda *cement* katika utekelezaji wake, barabara ile inaweza isidumu kama tunavyotegemea lakini tunasema kwamba kuna mambo mengine ni ya uzembe lakini hatua stahiki tunazichukua. Sasa hatuwezi tukasema barabara zote tunazojenga sasa hivi, kilomita 11,000 zinajengwa chini ya kiwango, si kweli! Hakuna nchi yoyote inayoweza kuwekeza katika kujenga barabara chini ya kiwango tutakuwa tunafanya kitu gani? Kwa hiyo, Serikali lazima ijenge barabara zinazoweza kudumu kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, kuhusu kuhusisha Kamati ya Miundombinu kukagua barabara. Kwanza, hili suala la kukagua barabara ili kujua kwamba ni kiwango, ni suala la kitaalamu si suala la siasa kama unavyosema Mheshimiwa bali ni suala la kitaalamu, tuna Wahandisi na sasa hivi Wahandisi washauri ndiyo wanasimamia barabara hizi. Pia tuna Mameneja wa Mikoa wa *TANROADS*, kuna Wahandisi kwa kila mradi wa kuhakikisha

barabara zinajengwa kwa viwango vinavyotakiwa. Sasa kama kutakuwa na *isolated cases* ambazo zinasababisha hili kutofanyika basi tutachukua hatua zinazostahiki. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali mwaka jana ilitutengea fedha ya kuweka barabara yetu ya kutoka Mtwara Pachani kwenda Lusewa eneo la kutoka Ligela kwenda Lusewa lami nyepesi na *TANROADS* walitangaza *tender* na kumpata Mkandarasi na mwaka huu Serikali imeongeza tena fedha nyingine shilingi milioni 100 kuweka lami hiyo nyepesi katika barabara hiyo ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Toka mwaka jana mpaka leo Mkandarasi huyo hajaanza kufanya kazi hiyo.

Je, Serikali mnaweza kuhimiza *TANROADS* kumsimamia Mkandarasi huyo aanze kazi ya kuweka lami nyepesi katika vipande korofi vya barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuahidi tu kwamba nitafuatilia barabara hiyo anayoizungumzia na tutaweza kuhimiza ili kazi hiyo iweze kuanza mara moja.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalufuata. Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu utaratibu, unasimama pale swali la msingi linapoulizwa lakini unapokuja kusimama baada ya majibu, hatuendi hivyo.

Naomba tuendelee na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum na linakwenda Wizara ya Nishati na Madini.

Na. 416

**Utafiti wa Madini Ruangwa**

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Sehemu kubwa ya Ruangwa Mkoani Lindi, ina utajiri mkubwa wa dhahabu, *green tourmaline, green garnet*, madini ya vito mbalimbali, safaya na unga mbalimbali wa kila aina ya rangi na kuna wachimbaji wadogowadogo wa kubahatisha tu sehemu zenye madini:-

Je, Serikali iko tayari kusaidia utafiti wa madini hayo ili yaweze kuchimbwa kwa faida kubwa zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ruangwa inayo madini mbalimbali ikiwa ni pamoja na dhahabu, vito hasa *garnets* na *tourmaline*, shaba na madini ya ujenzi kama vile mchanga, kokoto na mawe. Ni kweli kuwa licha ya kugundulika kwa madini hayo katika Wilaya ya Ruangwa bado utafiti wa kina haujafanywa kujua wingi wa mashapo ya madini katika maeneo hayo. Serikali kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania (*Geological Survey of Tanzania – GST*) imekuwa ikifanya tafiti za awali katika maeneo mbalimbali nchini ili kuainisha maeneo yenye madini na kuandaa ramani zinazoonyesha taarifa za madini mbalimbali yapatikanayo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha, Serikali kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania (*GST*) imeanza kufanya tafiti za kijiolojia na kijiokemia katika maeneo ya Wilaya za Ruangwa, Liwale na Lindi kuanzia mwezi Septemba, 2012. Baada ya utafiti huo kukamilika, *GST*

itaandaa ramani zitakazoonyesha upatikanaji wa madini katika maeneo mbalimbali katika Wilaya hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa taarifa zitakazotolewa na *GST* zitawezesha wawekezaji wa ndani na nje kuvutiwa zaidi kuja kuendeleza rasilimali ya madini iliyoko katika maeneo ya Mkoa wa Lindi, ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Ruangwa. Hata hivyo, ili kujua wingi wa mashapo ya madini yoyote yanayoweza kuchimbwa kibiashara au kwa faida, ni lazima utafiti wa kina (*detailed exploration*) ufanyike katika eneo husika.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi na nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo ameyatoa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kufahamu kwamba haya madini mengi kiasi hiki katika Mkoa wa Lindi miaka yote hii ndiyo ianze kufanya utafiti mwaka 2012? Mkoa mzima wa Lindi una madini kadhaa, Wilaya ya Nachingwea kuna dhahabu, Wilaya ya Lindi Vijijini kuna *gypsum*, Wilaya ya Ruangwa kuna *green tomarine* na *green garnet* kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa nataka kufahamu kwamba mwaka 2012 wameanza kufanya utafiti, majibu yatapatikana lini?

Je, Naibu Waziri yupo tayari kufuatana na mimi kwenda katika Mkoa wa Lindi kuangalia maeneo mbalimbali yaliyopo madini katika Mkoa wa Lindi ili aone taabu wanayopata wachimbaji wadogowadogo? Ni lini hawa watapewa zana za kuchimbia madini hayo? Sasa hivi wanatumia tu sululu, majembe, visu, nyundo na kadhalika, hawana zana wala maeneo, wanavamia maeneo mbalimbali. Naomba majibu ya Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nchi yetu linapokuja suala la madini, limegawanyika katika Kanda ambazo zimekuwa ni *hot sport,* ambazo ni Kanda ya Ziwa na maeneo ya Kanda ya Nyanda za Juu maeneo ya Chunya

ambayo ndiyo yalikuwa na kipaumbele kwa muda mrefu kwa kufanyika tafiti mbalimbali. Maeneo ya Lindi na Mtwara, ni maeneo mapya pamoja na maeneo ya Tanga, Kilindi ambayo Serikali sasa ndiyo imeelekeza nguvu kufanya tafiti za jumla ili kuweza kuainisha maeneo ambayo yana madini na ni madini ya aina gani. Kwa hiyo, baada ya tafiti hizo kufanyika ndipo pale *detailed exploration* inatakiwa ifanyike ili kujua sasa kiwango cha mashapo kilichopo katika maeneo husika. *GST* inachokifanya ni kuainisha na kuandaa ramani za madini za nchi na wanatumia teknolojia ya sasa ambayo ni *air bond survey* kuweza kupita na ku-*map* maeneo yote ya nchi ili kuweza kujua ni sehemu gani kuna madini na ni madini gani. Baada ya hapo sasa wanateremka chini kwenda kupata *detailed* zaidi. Kwa hiyo, kazi hii inaendelea kufanyika kwa maeneo hayo niliyoyataja na niseme tu kwamba kinachochimbwa sasa hivi kwa taarifa tulizonazo ni 10% tu ya rasilimali ya madini tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kwenda Lindi, Mheshimiwa Mbunge nipo tayari, tutapanga ratiba ili tuone lini nitatembelea Lindi kwenda kuona wachimbaji wadogo na kuwatafutia maeneo ya kuchimba.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, mwezi kama huu, niliondoka na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa agizo la Waziri, miongoni mwa kazi ambazo alikuwa nazo ni kutembelea wachimbaji wadogo na kuangalia sekta ya madini. Moja ya mambo ambayo alikutana nayo kule ni uchimbaji ambao umekuwa ukifanyika tangu mwaka 1905 wakati wa Vita ya Majimaji, watu wanachimba pale, kampuni zinarithishana mpaka leo kazi hiyo inaendelea kwa kurithishana kutoka kampuni hadi kampuni, tukakubaliana kwamba lazima ifike mahali wale watu wanyang'anywe au wafutiwe leseni. Napenda kupata kauli ya Serikali kutoka kwake kwamba mpaka sasa ikiwa ni mwaka mmoja wamefikia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulifanya ziara katika Mkoa wa Kigoma na kutembelea wachimbaji

wadogowadogo na kampuni ambayo Mheshimiwa Mbunge anaizungumzia ilikuwa ikifanya shughuli za uchimbaji kabla ya uhuru lakini kweli imekuwa ikibadilishana leseni au umiliki na kampuni nyingine na jambo hili amelifikisha katika ofisi yangu na nimemjibu kwamba ninatuma wataalamu wangu wachunguze na waniletee majibu sahihi ni kwa nini kampuni hiyo imekuwa ikifanya kazi hizo na kama inafanya kazi hizo kwa sheria basi hatuna sababu ya kuwanyang'anya lakini kama inakiuka taratibu na sheria tulizojiwekea wenyewe basi ofisi yangu kupitia Waziri wa Nishati na Madini hatutasita kufuta leseni hiyo. Kwa hiyo, majibu hayo ya kitaalamu sijayapata, lakini nitakapoyapata nitatoa kauli hapa Bungeni hatua ambazo tutazichukua.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Tunaendelea lakini uwahimize hao wanaotakiwa kuleta majibu walete kwa wakati.

Na. 417

**Kuwapandisha Vyeo Wanajeshi Wenye Taaluma Maalum**

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA** aliuliza:-

(a) Serikali ina mpango gani wa kuwapandisha vyeo Wanajeshi wenye taaluma maalum kama vile Wahandisi na Wataalamu wa *IT* ambao wamelipatia Jeshi sifa kubwa lakini hawapandishwi vyeo na badala yake wanaongezewa muda wa utumishi au kustaafu wakiwa na umri mdogo tofauti na wataalamu wengine wasio Wanajeshi?

(b) Je, Serikali itarekebisha lini utaratibu huo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na

Mheshimiwa Mshama kwamba baadhi ya Wanajeshi ambao nafasi zao za kitaalamu haziwezi kujazwa kwa kipindi kifupi wanapofikia muda wa kustaafu utumishi wao. Hata hivyo, Jeshi halina uwezo wa kuwapandisha vyeo Wanajeshi wote wenye taaluma maalum waliofikia muda wa kustaafu utumishi wao. Kwa kawaida, Jeshi linawapandisha vyeo Wanajeshi pale ambapo kuna nafasi ya uongozi inayohitaji kujazwa na kama Wanajeshi hao wana ujuzi na uzoefu wa kutosha.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika nakubaliana na Mheshimiwa Mshama kuwa wapo Wanajeshi wanaostaaafu wakiwa na umri mdogo lakini naomba ifahamike kuwa Wanajeshi hawa wanastaafu utumishi kulingana na majukumu ya utendaji wa kazi za kijeshi walizonazo. Askari wenye vyeo vya chini kuanzia *Private* hadi Sajenti pamoja na Maafisa wao wenye vyeo vya Luteni Usu (*Second Lieutenant*) hadi Kapteni wanapambana na adui moja kwa moja katika vita. Kutokana na hali hiyo, Wanajeshi hao wanalazimika kutembea kwa miguu kwa muda mrefu. Kwa hiyo, Askari na Maafisa hawa wanastaafu wakiwa na umri wa miaka 50. Kwa mantiki hii, Jeshi halina mpango wa kubadilisha umri wa kuwastaafisha Askari na Maafisa pamoja na upandishaji vyeo sababu utaratibu huu unasaidia kuhakikisha kuwa Wanajeshi wanatekeleza majukumu yao ya Kijeshi ipasavyo.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Nitauliza tu swali moja la nyongeza hasa ukizingatia kuwa swali langu la msingi lilikuwa linauliza wataalam maalum kama vile Madaktari na wajuzi wa *IT*, Wahandisi na wengineo hasa ambao Serikali inatumia fedha nyingi sana kuwasomesha na matokeo yake unawakuta wanastaafu wakiwa na umri mdogo, wako mitaani wanahangaika. Kwa hiyo, nashukuru kwa kunipa ufahamu juu ya Wanajeshi wa kawaida ambao na mimi nadhani ni suala jema kabisa wale ambao hawawezi kutembea tena, hawawezi kupigana lakini swali langu la kubadili utaratibu linahusu wale wenye utaalamu ambao mimi katika Jimbo langu nawaona wapo tu na

hawakuongezewa mkataba, nahisi wangeweza kuendelea kulitumikia Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba Serikali inatumia fedha nyingi sana katika kuwatayarisha na kuwasomesha wataalamu wa kada mbalimbali wanaofanya kazi katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa lakini suala la umri hasa katika Utumishi wa Jeshi, ni suala ambalo limefanyiwa utafiti wa kisayansi. Tumebaini kwamba majukumu ya Jeshi yanahitaji kutumia nguvu na kwa maana hiyo basi ndiyo maana umewekwa umri Fulani. Sasa kwa Askari ambao pengine wana taaluma lakini vyeo vyao ni kuanzia Makanali na kuendelea, hao watakuwa na muda mrefu sana wa kufanya kazi katika ofisi na hapo sasa basi utaratibu anaouzungumza mara nyingi tumekuwa tukiuzingatia lakini kama nilivyosema, chini ya vyeo hivyo, Askari hao wanapaswa kufanya kazi katika *field* na kwa maana hiyo ni lazima wawe na afya ya kutosha ili waweze kutekeleza jukumu lao. Hata hivyo, nafikiri wazo lake hili Wizara yangu itaendelea kulitafakari na kulifanyia kazi ipasavyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita sana, naomba tuendelee tu sasa na maswali ya msingi, tunaenda Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Na. 418

**Jukumu la *NHC***

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) lina jukumu kubwa la kuwatafutia wananchi makazi ya kudumu wakiwemo wafanyakazi wa Serikali:-

Je, kwa sasa ni nyumba ngapi za *NHC* zilizojengwa kwa ajili ya kuwauzia wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa limeandaa Mpango Mkakati wa kipindi cha mwaka 2010/ 2011 – 2014/2015 kwa ajili ya kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uhaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Ni maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi kuwa Serikali ijenge nyumba 15,000 ili kuwezesha wananchi wa kipato cha chini na cha kati kupata makazi bora. Mpango huo unaliongoza Shirika la Nyumba la Taifa kuhakikisha kuwa malengo yanayoainishwa kwenye Dira ya Taifa ya mwaka 2025 (*Tanzania Vision 2025*) na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano ya mwaka 2011-2016 yanafikiwa. Mpango Mkakati wa Shirika unaelekeza kuwa 70% ya nyumba za makazi zinazojengwa ziuzwe kwa wananchi na 30% zipangishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Mei, 2013, Shirika lilikuwa linatekeleza miradi 18 ya ujenzi wa nyumba za makazi kwa ajili ya kuwauzia wananchi na kupangisha. Miradi hiyo ina jumla ya nyumba 1,206 ambayo ujenzi wake unaendelea katika miji mbalimbali nchini.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Rais alipozindua nyumba za gharama nafuu Kigamboni, alitoa agizo kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuwa wapunguze bei ya nyumba hizo kwa kuondosha *VAT*. Je, mbona mpaka leo agizo hili halijatekelezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Rais alitoa agizo kwamba nyumba zote za

zamani za Shirika hili wauziwe wale ambao wanakaa katika nyumba hizo ambao wengi wao ni wastaafu wa Serikali hii ambao wamechoka na kuchakaa. Je, mbona mpaka leo agizo hili halijatekelezwa na badala yake wameongezewa kodi ya nyumba hizi? Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kuwa Shirika hili linaongozwa kwa ubabe, dharau kwa kutotekeleza amri ya Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kwamba Rais aliagiza *VAT* iondolewe kwenye nyumba zinazojengwa na Shirika la nyumba ili kupunguza bei. Ni kweli kwamba agizo hilo lilitolewa na Mheshimiwa Rais na kwa kuwa alielekeza tushauriane na Waziri wa Fedha, suala hili tuliliwasilisha kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha nao walilipeleka kwenye Kamati inayoshughulikia masuala ya kupunguza kodi. Kamati ile iliona kwamba sasa hivi kwa kuzingatia mahitaji halisi ya fedha katika nchi, kwa mwaka huu isingewezekana kuondoa kodi hiyo. Hata hivyo, suala hilo bado linaendelea kujadiliwa na litakapokuwa limekamilika basi hatua za kutekeleza maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais zitachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uuzaji wa nyumba za Shirika la Nyumba, kwanza naomba nikanushe mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba Shirika la Nyumba la Taifa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hata siku moja haziwezi kukaidi maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Mawaziri wanaosimamia sekta hii wako kwa ridhaa ya Mheshimiwa Rais. Shirika hili limeundwa na linaendelea kuwepo, Mwenyekiti wa Bodi na Mkurugenzi Mkuu wameteuliwa kwa ridhaa ya Mheshimiwa Rais. Hakuna hata mmoja kati yao mwenye uwezo wa kukataa maagizo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea ni kwamba tulipoingia madarakani, tulijulishwa kwamba kuna agizo la Mheshimiwa Rais kwamba nyumba ziuzwe kwa wapangaji. Tukaomba tupate maagizo haya ya Mheshimiwa Rais na uko utaratibu ufuatao. Mheshimiwa Rais anapotoa agizo lolote

akiwa kwenye ziara ama mikutano ya kawaida, kuna Waziri wa zamu na watendaji ambao wanaandamana na Mheshimiwa Rais. Yale maagizo hurasimishwa kwa kutolewa Waraka ama na Katibu Mkuu Kiongozi au Waziri mhusika. Tumeomba tupate maagizo hayo kwa maandishi hatukuweza kuyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo suala la msingi ni kwamba, nyumba ambazo wapangaji walikuwa wanasema wauziwe, baadhi yake tulizitaifisha mwaka 1971. Sheria ya Utaifishaji wa Nyumba zile iko bayana kwamba nyumba zile hazitauzwa. Vilevile kama tulitaifisha kwa manufaa ya Taifa ni sababu ipi leo inatufanya sisi tubinafsishe kwa watu wengine kwa nini tusiwarudishie wale tuliochukua kutoka kwao? Kwa hivyo, si halali na wala si vyema nyumba ambazo zimetaifishwa tuwauzie watu wengine, badala yake kwa kuwa sehemu kubwa ya nyumba ambazo inasemekana zimechakaa ziko kwenye *prime location,* tunavunja nyumba zile, tunajenga nyingine bora ambazo wapangaji wanaendelea kupata. Wale wananchi ambao wanapanga kwenye nyumba hizi tumewakaribisha pia wanunue nyumba ambazo tunajenga na kuuza hivi sasa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaomba radhi sana tayari tumeshapitiliza sana muda hivyo ni bora tumalize maswali tuliyonayo leo. Tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Henry Dafa Shekifu, Mbunge wa Lushoto.

Na. 419

## Mabaraza ya Ardhi

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU** aliuliza:-

Nia ya Serikali kuunda Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ni kutatua migogoro ya ardhi kwenye maeneo mbalimbali ya nchi kwa ufanisi lakini uko uhaba mkubwa wa Mabaraza ya Ardhi Wilayani Lushoto ambao umesababisha migogoro mingi ya ardhi kwa sababu hakuna Baraza la Ardhi:-

Je, ni lini Serikali itaunda Baraza la Ardhi Wilayani Lushoto ili kuondoa adha wanayopata wananchi wa Lushoto kwenda Korogwe kutafuta haki?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Henry Dafa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianzisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza ya Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002 kwa lengo la kusikiliza na kuamua migogoro ya ardhi na nyumba. Vigezo vya kuzingatia katika uanzishwaji wa Mabaraza ni pamoja na wingi wa migogoro ya ardhi na nyumba katika Wilaya husika, umbali kutoka Wilaya moja yenye Baraza hadi nyingine. Aidha, uwezo wa Serikali katika kuyahudumia Mabaraza ni msingi mkubwa katika utekelezaji. Tangu utekelezaji wa sheria hii ulipoanza mwaka 2004 hadi Aprili, 2013 Serikali imeanzisha jumla ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 42.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Wilaya ya Lushoto ina tatizo la Baraza la Ardhi na Nyumba na ni moja ya wilaya zenye migogoro mingi ya ardhi na nyumba nchini na ni kweli alivyosema wananchi wa Wilaya hiyo huifuata huduma hiyo katika Wilaya ya Korogwe ambapo ni takribani kilomita 70. Kwa mfano wapo wananchi wa kijiji cha Mnazi katika Wilaya hiyo ya Lushoto ambao hulazimika kusafiri takribani kilomita 185 hadi Korogwe kwenye huduma ya Baraza. Ili kuwapunguzia wananchi hao kero ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za Baraza Korogwe, Serikali inatafuta fedha ili kuanzisha Baraza la Ardhi na Nyumba katika Wilaya ya Lushoto.

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nianze kwa

kumshukuru kwa sababu alikwenda Lushoto na alijionea mwenyewe hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ahadi ya kufungua Baraza Lushoto haijatolewa muda, ni lini sasa Baraza hilo litafunguliwa kwa sababu wananchi wamesubiri kwa muda mrefu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa rufaa nyingi zinachukuliwa kwenda kwenye Mabaraza ya Wilaya kutokana na udhaifu katika Mababara ya Kata, na kwa sababu katika Mabaraza haya ya Kata wajumbe hawana elimu na weledi wa kutosha, lakini hata posho hawalipwi. Sasa Serikali inatamka nini juu ya kuchukua hatua ya kuimarisha Mabaraza ya Kata ili kusiwe na mafuriko katika Mabaraza ya Wilaya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu fasaha lakini kwa ufupi kwani tuna tatizo la muda hapa.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kwamba ni tarehe ipi au ni lini Baraza hilo la Lushoto litafunguliwa, kama nilivyoeleza katika jibu la swali la msingi, nilisema kwamba tunatafuta fedha. Kama tunataka kuwa na Baraza kila Wilaya nchini, kwa hesabu tulizopiga wakati tunaandaa bajeti yetu kwa mwaka huu peke yake tungehitaji shilingi 22,600,000,000/= lakini kwa sababu ya ufinyu wa bajeti hatukuweza kupata fedha hizo na kwa msingi huo kwa mwaka huu unaokuja tutaanzisha Mabaraza machache sana. Hata hivyo, nipende kumhakikishia Mheshimiwa Shekifu kwamba tutawapa kipaumbele mara tutakapopata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu udhaifu wa Mabaraza ya Kata na Vijiji, ni kweli kwamba Mabaraza yale Wenyeviti na Wajumbe wanateuliwa kwa kuzingatia mazingira ya pale walipo na kigezo cha elimu hakijapewa kipaumbele. Suala la posho pia ni kweli kwamba posho inayolipwa bado ni kidogo sana, lakini kwa kuwa Mabaraza

haya yanasimamiwa na mamlaka za Halmashauri za Wilaya na Miji, tutashauriana na wenzetu wa TAMISEMI ili tuone namna gani tutaboresha Mabaraza haya. Sisi tuko tayari pale ambapo Wilaya iko tayari kutoa elimu kwa Wenyeviti pamoja na Wajumbe wa Mabaraza yale, lakini suala la posho ni lazima tushauriane na wenzetu wa TAMISEMI kwa sababu ndiyo wanaosimamia Mabaraza yale ya Kata.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaenda swali la mwisho kwa siku ya leo na linaulizwa na Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, Mheshimiwa Rajab kwa niaba yake.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya mtoto wangu mpendwa, Mheshimiwa Kasulumbayi, naomba swali lake Na. 420 lipatiwe majibu. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Huyo mtoto wako sijui umeanza naye lini? Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu swali la mtoto wa Mheshimiwa Rajab. *(Kicheko)*

Na. 420

**Maji ya Mvua kutumika kwa Mifugo**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (K.n.y. MHE. SYLVETSER M. KASULUMBAYI)** aliuliza:-

Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa maji ya mvua hayapotei na badala yake yatumike kwa ajili ya mifugo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvetser Mhoja Kasulumbayi, Mbunge wa Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Programu ya

kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP),* Serikali kuanzia mwaka 2006/2007 imekuwa ikitenga fedha kwa madhumuni ya kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ya uvunaji wa maji ya mvua kwa matumizi ya mifugo. Katika miaka saba ya utekelezaji wa Programu ya *ASDP* hadi kufikia mwaka 2012/2013 jumla ya shilingi bilioni 18 zimetengwa kutekeleza miradi ya kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya mifugo pekee 70 kwa kujenga na kukarabati malambo 500 na uchimbaji wa visima virefu 70 katika Wilaya mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa mkakati huu umechangia kwa kiasi kikubwa katika kuongeza upatikanaji wa maji kwa mifugo hasa kwenye maeneo ya ufugaji ingawaje mahitaji bado ni makubwa. Kwa mfano kuanzia mwaka 2001, Wilaya ya Maswa imeendeleza uvunaji wa maji kwa ajili ya mifugo kwa kujenga na kukarabati malambo 20 na uchimbaji wa visima virefu 25 hadi Desemba 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na uvunaji wa maji ya mvua unategemea sana uibuaji wake unaofanywa na walengwa kupitia Dhana Shirikishi ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo *(Opportunities and Obstacles to Development*). Miradi hii itaendelea kutekelezwa kutokana na mipango ya wilaya kutegemeana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wilaya imeendelea kuhimiza ubunifu wa miradi inayokidhi mahitaji halisi ya maji kupitia mwongozo wake wa ujenzi bora wa vyanzo vya maji ya mifugo uliotolewa mwaka 2007 na kusambazwa kwa wadau mbalimbali zikiwemo Halmashauri zote hapa nchini.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, moja ya tatizo ambalo tunalo katika Halmashauri zetu katika kutekeleza miradi hii ni suala zima la utaalam. Ni kweli fedha

zinapelekwa katika Halmashauri, lakini bado tuna tatizo la wataalam katika Halmashauri zetu, hususan wa mambo haya ya kilimo. Je, Wizara imejipangaje kwa mwaka huu kuhakikisha kwamba zile Halmashauri hususan za pembezoni mwa nchi yetu ambazo hazina wataalam hawa zinafikishiwa wataalam hao kutoka Wizarani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, fedha hizi za *ASDP* huwa ziko katika mfuko mkuu wa Wizara. Tatizo linalotokea hapa ni namna ya kuhamisha fedha hizi kuzipeleka katika akaunti husika na haya yote huwa yanatokana na fedha hizo kuchelewa kutoka pale Wizarani kupelekwa katika Halmashauri husika. Je, ili mpango huu uwe endelevu na miradi hii iweze kuendelea vizuri, Wizara imejipangaje kuhakikisha tatizo hili la ucheleweshaji wa fedha kutoka akaunti kuu kwenda katika Halmashauri sasa hivi halitokei? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la wataalam, Serikali iko kwenye programu ambayo imeanza miaka minne iliyopita kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inakuwa na wataalam wa kutosha kwenye ngazi za Vijiji, Kata, Tarafa na Wilaya. Kwa hiyo, Serikali inasomesha wataalam wa kilimo, mifugo na uvuvi na kwa nchi nzima tunahitaji takribani wataalam wa mifugo 16,000 na sasa hivi tuna takribani 5,000. Tunaendelea na mwaka huu wataajiriwa wengine wataalamu wengine wa mifugo na uvuvi 2,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili linahusiana na ucheleweshaji wa fedha. Fedha zinapelekwa kwenye Wizara na hatimaye kwenye Halmashauri kwa ajili ya miradi hii kutokana upatikanaji na makusanyo ya fedha ya kila mwezi. Hata hivyo, katika miaka ambayo nimeishaitaja zaidi ya shilingi bilioni 18 zimeishatumika, mwaka jana 2012/2013 shilingi bilioni 1.5 na mwaka huu TAMISEMI imetengewa zaidi ya shilingi bilioni tano kwa ajili ya miundombinu ya mifugo na Wizara yangu pia katika fedha za nyongeza zipo zaidi ya shilingi bilioni tatu kwa ajili ya miundombinu ya mifugo katika maeneo ambayo yana matatizo ya miundombinu hiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema muda umetutupa sana, tunayo ajenda nyingine kwenye ratiba na ni lazima tuendelee nayo.

*(Hapa Mheshimiwa Peter Serukamba alikuwa amesimama akiomba Mwongozo wa Spika)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Serukamba nimekuona.

Naomba tu mniruhusu sasa nisome matangazo yaliyopo hapa Mezani.

Tangazo la kwanza ni la kikao cha Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo wanaombwa wakutane kwenye kikao leo tarehe 18, mwezi wa Sita, saa 7.00 mchana katika Ukumbi Na. 219 Ghorofa ya Pili, jengo la Utawala. Kwa hiyo, niwaombe sana wajumbe wa Kamati hiyo ya Katiba, Sheria na Utawala kuhudhuria kikao hicho cha Kamati.

Halafu nina tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI. Tafadhali Waheshimiwa Wabunge, mnafahamishwa kwamba, siku za Jumamosi na Jumapili tarehe 22 na 23 kutakuwa na semina ya Wabunge wote. Semina hiyo ambayo itaambatana na Mkutano Mkuu wa *TAPAC*, itafanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa *Saint Gasper Conference Centre* na itaanza saa 3.00 asubuhi ikuhusu UKIMWI na Sheria. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria bila kukosa na kuzingatia muda. Hilo ni tangazo ambalo limetoka kwa Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na linatukumbusha na nadhani ni muhimu kwenda kuzitazama sheria zilizopo na kuangalia zinaendaje sambamba na tatizo hili la UKIMWI katika nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, huyu ni Katibu wa

Wabunge wa *CUF*, niwatangazie Wabunge wote wa *CUF* na naona wananisikiliza kwa makini sana, kuwa leo tarehe 18/6/2013, saa saba mchana baada ya kusitisha siyo kuahirisha Mheshimiwa Magdalena Sakaya saa saba tutasitisha. Baada ya kusitisha Kikao cha Bunge watakuwa na kikao cha Wabunge wa *CUF* katika Ukumbi namba 227 na mnatakiwa kuhudhuria bila kukosa. Ukumbi namba 227, tangazo limetoka kwa Mheshimiwa Magdalena Sakaya Katibu wa Wabunge wa *CUF* sijui watamwalika na Katibu wa Wabunge wa CCM kuhudhuria kikao hicho. Kwa hiyo, Wabunge wa *CUF* hilo tangazo lenu la kikao. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo matangazo niliyoyapata lakini nichukue nafasi hii kuwakaribisha wageni wote ambao wapo katika Ukumbi wetu leo, tunawashukuru na tunawapongeza kwa kuja kuangalia shughuli zetu zinavyoendeshwa ndani ya Ukumbi wa Bunge, karibuni sana.

Baada ya kusema hayo, nilimwona Mheshimiwa Peter Serukamba, ngoja tumpe nafasi tuendelee.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kulingana na Kanuni ya 68(1). Wakati Naibu Waziri wa Ujenzi anajibu swali la nyongeza la Mbunge Shamsi wa *CUF* ambaye alitaka kujua kama Kamati ya Bunge zinaruhusiwa kwenda kuona miradi ili waweze kujiridhisha na kinachojitokea, Naibu Waziri amesema suala la Wabunge kwenda kuona miradi ni suala la kisiasa zaidi kwa sababu wao hawana utaalam wa kujua kwamba hili linalofanyika ni nzuri ama siyo zuri, kwamba jambo hilo linatakiwa lifanywe na watendaji. Kwa hiyo, nilitaka tu kupata Mwongozo wako kama sasa Serikali imeamua Wabunge tusiende tena kuangalia miradi ya Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri tu Mheshimiwa Naibu Waziri, utaratibu wa ukaguzi wa miradi hata kama kwa mujibu wa sheria na kanuni za Halmashauri

zetu, unakuta Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri inaundwa na Madiwani na Wabunge wakiwa ndani ya Kamati hizo na kwa mujibu wa Kanuni hizo wanaruhusiwa na wao ndiyo wahusika wakuu wa ukaguzi wa utekelezaji bora wa miradi kwenye *level* ya Halmashauri. Sasa kama kwenye *level* ya Halmashauri linachukua sura hiyo haliwezi kuwa sivyo katika *level* ya Bunge kwamba Waheshimiwa Wabunge hawana haki na wajibu wa kukagua miradi.

Mimi nafikiri Mheshimiwa Naibu Waziri, kimsingi ni kwamba zile shughuli ambazo zinahitaji utalaam wa hali ya juu zitafanywa na wataalam lakini haziwazuii Waheshimiwa Wabunge na wao pia kwa kujua majukumu yao ya kuisimama Serikali kufanya kazi hizo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mwongozo wangu ni kwamba Waheshimiwa Wabunge, Kamati zenu bado zina haki ya kufanya kazi hizo na wataalam wenye utaalam wao wa kiufundi na wao wana wajibu wa kufanya kazi hizo.

Kwa hiyo, watu wote tutafanya kazi hizo kwa kushirikiana na hakuna anayewazuia Waheshimiwa Wabunge kupitia Kamati zao kukagua miradi ambayo ipo chini ya Wizara hizo. Kwa hiyo, mimi mwongozo wangu ni kwamba tutaendelea kufanya kazi ya kukagua hiyo miradi kwa mujibu wa kanuni na taratibu ambazo tumepewa. *(Makofi)*

Katibu hatua inayofuata!

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria Sheria ya Fedha wa Mwaka 2013 (The Finance Bill)

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, jana Waziri wa Nchi alitoa hoja ya kubadilisha Kanuni ili Muswada huu leo usomwe kwa Mara ya kKwanza. Kwa hiyo, kwa mujibu wa mabadiliko ya Kikanuni tuliyofanya jana, mmeona kwenye *Oder Paper* leo shughuli yetu ya pili imekuwa ni Kusomwa kwa Mara ya Kwanza kwa Muswada huo wa Sheria ya Fedha, unazingatia mabadiliko tuliyoyakubali jana ndani Bunge yaliyowasilishwa na Mheshimiwa William Lukuvi, *Chief Whip* wa Serikali. Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2012/2013 pamoja na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Sasa tunarudia kwenye hoja yetu ya Serikali na majadiliano yanaendelea. Ilikuwa tuanze na Mheshimiwa Salim Turky, hayupo ndani ya Ukumbi wa Bunge, ilikuwa tumsikie Mheshimiwa Silvestry Koka, hayupo ndani ya Ukumbi wa Bunge, ilikuwa tumsikie Mheshimiwa Halima James Mdee, hayupo ndani ya Ukumbi wa Bunge na ilikuwa tumsikie Mheshimiwa Martha Umbulla, naye hayupo ndani ya Ukumbi wa Bunge. Sasa nimwombe Mheshimiwa Kapt. Komba aanze kuchangia, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Luhaga Mpina, halafu tutaendelea na wachangiaji wengine.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nikipongeze Chama changu cha Mapinduzi kwa kushinda Kata 16 na kuwabwaga wenzetu kwa Kata zao sita, watajijua wenyewe huko waliko. Hongera sana Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika changiachangia zangu nyingi katika kipindi hiki, nimezungumzia sana kuhusu *TBC.* Ninashukuru *TBC* imeongezewa fedha shilingi bilioni sita na sasa ninaomba sana, hii michango ninayochangia hapa kule kwangu hawasikii. Naomba muanze kupeleka kule usikivu ili na wale wananchi wa Nyasa waweze kupata matangazo ya *TBC*. Ninaishukuru sana Serikali kwa kuijali *TBC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, barabara nimeona kuna fedha pale katika Wizara ya Ujenzi, fedha za kutoka Mbinga kwenda Mbambay, naomba fedha zile zianze kutumika sasa kujenga barabara ya lami kutoka Mbinga kwenda Mbambay na wananchi waione kwamba barabara ya lami inaanza kujengwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, *REA*, fedha zimeongezwa zaidi ya shilingi bilioni moja na kitu huko, nina hakika sasa Kata zangu za Tingi, Mjini Mdogo wa Tingi, Mji Mdogo wa Mbambay, Mji wa Liuli na Mji wa Litui ambao tayari ilikuwa kwenye mpango watapatiwa umeme mwaka huu wa fedha. Naomba sana tusitafute sababu zingine kwa sababu fedha zipo pale tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu lingine ni shule, ninamwomba sana Waziri wa TAMISEMI, siku moja ndani ya mwaka huu tufuate naye kwenda kandokando ya Ziwa Nyasa na pia milima ya Matengo akaone namna shule zilivyokuwa duni kuanzia madawati, Walimu, wanafunzi na elimu yenyewe kwa ujumla, aendi akaone, akague, kusudi aweze kunisaidia kilio hiki ninacholia. Tupo duni katika elimu, naomba sana Serikali itilie mkazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri katika mipango ya shule, Waziri angeamua tu ama Serikali ingeamua tu, siyo nyasa pekee yake, lakini ingeamua tu tatizo la madawati waka-*solve* tatizo hili kwa nchi nzima hii kesi ikawa haipo tena lakini wakiendelea kukumbatia kwamba leo madawati tunatoa kidogo, kesho wanatoa kidogo, kesi hiyo haitakwenda. Tuweke *priority* kwenye elimu hasa upande wa

madawati ili wanafunzi wasikae chini, wakae kwenye madawati na nina hakika kwa namna hiyo elimu yetu itapanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumzia habari ya meli. Tulikuwa tunategemea meli ya Malawi, meli ya Malawi haiji tena Tanzania huku, tunaomba meli ya Tanzania ambayo Rais aliahidi ifike mara moja ikomboe wananchi wa upande huo wa mwambao wa Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati mwingine Rais aliahidi kituo cha Afya cha Mbambay kiwe Hospitali. Sasa Mbambay ni Mji Mkuu wa Wilaya na kile Kituo cha Afya ninaomba sasa Serikali kutokana na ahadi ya Rais basi kigeuzwe kuwa hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi nimesema mara nyingi, Ziwa Nyasa ni Ziwa maskini, wananchi wake ni maskini mpaka leo wanatumia mitumbwi. Naomba Serikali ambayo imeongeza fedha kwenye uvuvi wapeleke vifaa vya kisasa kule ili wananchi waweze kufaidi keki hii kwa kutumia maboti na ingini kwa ajili ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nimpongeze Katibu Mkuu wa CCM Kinana kwa kutoa gari la CCM, Wilaya ya Nyasa. Namshukuru sana na kwa kweli ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kapt. Komba. Sasa namwita Mheshimiwa Peter Serukamba atafuatiwa na Mheshimiwa Mpina.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuleta bajeti nzuri lakini yapo maeneo ningependa niyachangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye Mpango wa Maendeleo, misingi ya Mpango wa Maendeleo ya mwaka huu, ni kuhakikisha ukuaji wa uchumi unapunguza

umaskini. Ni kweli ukiangalia *data* zetu za kukua kwa uchumi tumefikia asilimia saba lakini kwa kweli tukubaliana ukienda kwenye maisha ya watu vijijini bado hali ni ngumu sana. Kwa hiyo, ningependa wachumi wetu waanze kupafikiria sasa na kupeleka maendeleo vijijini ili ukuaji huu wa uchumi uwe na mahusiano halisi na hali halisi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango mwingine ni suala la ardhi, nyumba na makazi, hili nimekuwa ninalisema siku zote. Naomba Serikali ije na mpango mkubwa wa kuhakikisha jambo moja linatokea, angalau kila Mtanzania mwenye nyumba, mwenye ardhi, mwenye shamba lake awe na hatimiliki. Tukifanikiwa hapo maana yake Watanzania hawa wataweza kukopesheka na wakiweza kukopesheka, *risk* nazo zitapungua, *interest rates* zitashuka kwa sababu watu wana hatimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo, tubadilishe sheria yetu, maana leo unakwenda unakopa benki, unajenga nyumba, lakini mtu akishindwa kulipa mkopo, benki ikitaka kwenda kuchukua fedha zake, anaweka *court injunction,* haiwezekani. Ndiyo maana *interest rate* za mabenki zinakuwa, hatuwezi kuzishusha. Kwa hiyo, lazima tukubali kwa sababu tumeingia kwenye mfumo huu wa soko huria lazima twende wanavyoenda wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Serikali. *TRA* wanafanya kazi kubwa sana, wanakusanya kodi lakini kama hatutaweka msimamo katika *government expenditure* maana yake hizi kodi hatuwezi kwenda kwa kasi tunayoitarajia. Lazima kama nchi tukubaliane, tuelewane kwenye matumizi ambayo kwa upande wa Serikali ni makubwa. Kwenye Kamati ya Bajeti wameonyesha mfano wa jambo ndogo tu, ukiangalia kasma saba zinatumia shilingi bilioni 899 hizi ni kasma saba tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili suala la matumizi ya Serikali lazima tujiulize, tuangalie Sheria yetu ya Manunuzi. Sheria yetu ya Manunuzi, mimi naomba niseme leo ni sheria ambayo imeleta utaratibu wa kufanya ulaji ambao upo ndani

ya sheria. Unakwenda kwenye ofisi za Serikali, *ream* moja ya karatasi ukienda dukani ni Sh.5,000 lakini nenda kaangalia kwenye *supplier* za Serikali *ream* hiyo moja ni Sh.10,000, lakini wamefuata Sheria za Manunuzi. Kwa hiyo, lazima tujiulize tena, naomba Bunge lako Tukufu tukae tukubaliane kuhusu Sheria hii ya Manunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunanunua magari mengi sana, mimi sina shida ya kununua mashangingi, lakini lazima tuyanunue Toyota? Kwa nini kama Serikali tusiende kwa *manufacturer* mwenyewe, tukamwambia duniani *manufacturer* wapo wengi, tunaomba tununue magari kwako, tuta-*save* kila gari siyo chini ya shilingi milioni 100. Kwa nini *computer* tusinunue kwa *manufacturer,* tuta-*save* zaidi ya asilimia 60 lakini yote haya hakuna anayehangaika nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda leo peleka gari lako la *V8 Toyota*, kafanye *service* halafu uangalie na ya Katibu Mkuu, utakuta bei mbili tofauti za kufanya *service, why?* Kwa hiyo, lazima suala la matumizi tuliangalie kwa upana wake *otherwise* tutawaambia *TRA* wakusanye na watakusanya mabilioni ya fedha lakini zote zitaishia kwenye matumizi na kwenye matumizi hasa kwenye suala la manunuzi, suala la manunuzi hapa ndipo lipo tatizo, naomba tukae tuiangalie sheria hii ili iwe na maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la kodi zilizowekwa. Serikali inaongeza *excise duty* kwenye simu kutoka asilimia 12.5 mpaka asilimia 14.5 lakini tumesema kodi zetu tunaoanisha na wenzetu wa Afrika Mashariki, kodi hii wenzetu wa Afrika Mashariki ni asilimia 10. Mwaka jana tumeongeza kuwa asilimia 12.5 na mwaka huu tunaenda asilimia 14.5 lakini wakati huohuo mwaka jana ilikuwa ni kwa ajili ya *airtime,* sasa tumeongeza *airtime*, tumeongeza *SMS* na tumeongeza *internet* kwa maana ya *data*. Huku tumewasaidia wafanyakazi wa Serikali kupunguza asilimia moja lakini huku tunawaongezea kodi kubwa. Hali ya maisha yetu itaendelea kuwa ngumu. Mimi ninaomba niwashawishi Wabunge wenzangu, tumepanua wigo, tusiongeze *excise*

*duty* kwenye simu ibakie kuwa 12.5, Serikali iende ikatafute hizo fedha itazipata wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la matumizi, Makatibu Wakuu, tunapitisha vitabu hapa, kila kifungu kimoja kimoja tunasema kimepita, kimepita, lakini Makatibu Wakuu wakishapewa fedha, wao ndiyo wanaamua wanavyotumia siyo kulingana na tunavyopitisha hapa. Naomba Bunge lako kwa sababu tumeunda Kamati ya Bajeti twende kila baada ya miezi mitatu tuangalie kweli kama matumizi ni kulingana na vifungu ambavyo Bunge lako limepitisha. Hapa ndiyo penye tatizo namba moja. Naomba Wabunge tupasimamie, tuhakikishe tunaenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, misamaha ya kodi, misamaha ya kodi inatolewa kwa ridhaa, *discretionary,* hii haina usawa na inalenga kuwanufaisha wafanyabiashara wakubwa ambao wana uwezo wa ku-*lobby*. Naomba Bunge lako lidhamirie, misamaha yote ya kodi iwekwe kwenye sheria. Tunapoacha misamaha ya kodi iwe *discretionary* ya mtu mmoja hapa ndipo tatizo linapoanza. Tunapiga kelele tupunguze misamaha ili tuweze kufaidika kama nchi lakini mkishampa mtu mmoja ndiye aamue wafanyabiashara wakubwa wana uwezo mkubwa wa ku- *lobby* watafanya hiyo kazi, naomba hilo tulipunguze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la dizeli. Tumeongeza kwa ajili ya barabara, mimi naipongeza Serikali, tumeongeza kwa ajili ya *REA*, naipongeza Serikali, lakini naomba maongezo mengine yale ya dizeli na petroli kutoka 215 kwenda 217 na dizeli kutoka 300 kwenda 400, hiyo hapana. Kwa sababu tukiongeza kodi ya mafuta hii ni *inflationary,* matokeo yake bei ya kusaga unga itapanda, bei ya nauli zitapanda, bei za maisha zitapanda. Maana ya kodi isiwe ni kukusanya kodi nyingi lakini kama haina nia ya kukuza uchumi, bado tutakuwa hatujafikia lengo tulilolitaka. Kwa hiyo, naomba tuliangalie upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kwenye suala hili ukienda vijijini bei za viwandani vijijini ni kubwa sana lakini

bei za mazao yao ni ndogo sana. Kwa hiyo, tunaendesha chumi mbili nchini hapa. Ukienda kule kijiji kwetu Kalinzi, ukienda Rukwa huko ndani bei ya mahindi ni tofauti na bei ya mahindi inayouzwa Dar es Salaam kwa sababu gani, kwa sababu mazao yanayokwenda kule vijijini yana *inflation*, lakini mazao wanayouza wao hayana *inflation.* Lazima hili tuliangalie, hii ni kazi ya Wachumi, tufanye kazi na ili kuondoa hali hii lazima kupunguza gharama za usafiri tu-*invest* kwenye reli. Reli tuliyoweka kwenye reli ni nyingi, lakini haitoshi kwa sababu reli yetu imeanguka kwa muda mrefu, imefika wakati tuweke mabilioni ya shilingi ili tuondoe tatizo letu kwenye reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi naomba sana pamoja na yote yaliyofanyika, Serikali ikae na Bunge lako tujiulize tunafanyaje kuhusu matumizi ya Serikali. Hapa ndipo ambako kuna tatizo. Hata tukiongeza kodi kikubwa kiasi gani kama bado hatujasimamia matumizi ya Serikali, hatuna tutakachokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nisiunge mkono hoja hii mpaka pale ambapo Waziri wa Fedha atakuja kuniambia ameondoa *excise duty* kwenye simu, ameondoa kodi aliyoongeza kwenye mafuta lakini zaidi ya hapo nataka misamaha isitolewe kwa *discretion,* yote iende kwenye sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Luhaga Mpina atafuatiwa na Mheshimiwa James Mbatia halafu Mheshimiwa Khalifa ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianzie pia kwa kuipongeza Serikali. Mwaka jana ilishindwa kukidhi mahitaji ya mpango wa fedha, badala ya kutenga shilingi trilioni 2.9 Serikali ilitenga shilingi trilioni 2.2 ikiwa na upungufu wa shilingi bilioni 700. Mimi bajeti ile niliipinga kwa nguvu zote kwa sababu haikuzingatia yale tuliyokubaliana katika mpango lakini katika hili niipongeze Serikali kwa leo walau imeweza kufikia hiyo shilingi trilioni 2.9 ambayo ndiyo tuliowaahidi Watanzania kupitia Mpango huu

kwa sababu leo tuna shilingi trilioni 2.98 kutoka kwenye mapato yetu ya ndani zote hizi zinakwenda kutekeleza Mpango kama ambavyo tuliwaahidi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na mimi nijipongeze pia kwa sababu sikuyumba hata wale watu walionibeza, wakaanza kusema kwamba aidha Mpina anatumiwa, aidha Mpina ninalo jambo la kwangu mimi, lakini niliendelea kusimamia kwamba Watanzania tuliwaambia kwamba kila mwaka tutatenga fedha zetu za ndani shilingi trilioni 2.9, nikasimamia msimamo huo. Nataka niwahakikishie wale wote ambao walikuwa wananibeza kwa namna ile au nyingine, kwanza wakubaliane na mimi kabisa kwamba hakuna mwanasiasa yeyote hapa Tanzania na hata duniani ambaye anaweza akanitumia mimi, isipokuwa wanaoweza kunitumia ni wapigakura wangu wa Kisesa au Watanzania, hao ndio wanaoweza kunitumia lakini hakuna mwanasiasa yeyote duniani na hata Tanzania ambaye anaweza akanitumia kwa maslahi yake ya kisiasa. Sasa Serikali imefikia hapo leo shilingi trilioni 2.98 zimepatikana kwa ajili ya kutekeleza Mpango wetu, naipongeza Serikali kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kasoro nyingi ambazo hazijatekelezwa ambazo zinanifanya hata leo siwezi kuiunga mkono bajeti hii ya Serikali ambapo hizo kasoro zinatakiwa kurekebishwa tu. Watu wengine wasiojua na wasioelewa Mbunge ukisema unaipinga bajeti basi unaonekana kwamba bajeti hii hutaki iwepo au vinginevyo, unachotaka ni *commitment* kubwa ya Serikali kufanya mabadiliko uliyoyaona na ndicho nitakachokifanya hapa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nilitoa Maelezo Binafsi na wewe mwenyewe ulitoa maelekezo yako kwamba Serikali ilete majibu ya Maelezo yangu hayo Binafsi lakini mpaka sasa tunavyozungumza Maelezo haya hayajaletwa na Serikali wala sijajua kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni hili suala la matumizi

makubwa ya Serikali, hata mwaka jana wakati nilikataa bajeti nilisema kwamba tunaweza tukapunguza mpaka shilingi bilioni 500 katika matumizi mengineyo na bado Serikali ikafanya kazi zake, shilingi bilioni 500 tunaweza kupunguza lakini matokeo yake katika mwaka huu wa fedha matumizi hayo yameongezeka kutoka shilingi trilioni 1.07 mpaka shilingi trilioni 4.5 ambapo ni ongezeko la shilingi bilioni 430. Sasa Serikali haileti uchambuzi wa kina katika matumizi yake haya, matumizi ya posho, safari, semina, mafuta, vilainisho, viburudisho pamoja na vingine ambavyo viko kwenye upande wa manunuzi kama Mheshimiwa Serukamba ambavyo amezungumzia. Kwa uchambuzi wa SIKIKA walau wanatusaidia kuchambua wamesema mwaka jana matumizi kama haya tu machache niliyoyataja yalikuwa shilingi bilioni 681 lakini leo yamefikia shilingi bilioni 714. Waziri anaendelea kusema kwamba matumizi yamepungua, lakini mpaka sasa hasemi yamepunguzwa kwenye maeneo gani ni kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kubanwa na Bunge hili imekubali kupunguza fedha za matumizi ya kawaida kwa shilingi bilioni 283.5, imekubali kupunguza, haraka haraka wakakubali kupunguza. Kwa maana hiyo, huu ni uthibitisho kwamba kwa muda wote, kwa miaka mingi Serikali imekuwa ikielekeza matumizi yasiyo ya lazima na kuacha vipaumbele vya Kitaifa, shilingi bilioni 283 zilipatikana kwa haraka haraka. Mimi najua zinaweza kupatikana kati ya shilingi bilioni 500 mpaka 700 na ukilichana katikati hili tufe la matumizi mengineyo, unaweza kushangaa sana na Bunge linaweza kushangaa sana kwamba tunaacha kufanya kazi za Watanzania, Watanzania wanaendelea kuwa na mateso makubwa, tunaendelea kupandisha tozo na ushuru kila leo, kumbe ni za watu tu kwenda kufanya anasa. Hili haliwezi kukubalika na mimi Mpina siwezi kuunga mkono bajeti ya namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imeishia tu kusema kwamba kasma za vipaumbele hazitengewi fedha za kutosha na badala yake matumizi hayo kuelekezwa katika matumizi yasiyo ya lazima. Hiyo ni Kamati ya Bajeti, wameishia tu kusema hivyo, hii haitoshi kusema hivyo, waende waifumue hii bajeti wazitafute hizi shilingi bilioni 513, mimi nakwambia

huhitaji kuwapa mzigo Watanzania kwa kuongeza tozo na ushuru huo tulioweka, unahitaji tu kupunguza matumizi ya kawaida haya, ukazichomoa shilingi bilioni zako 513 zako zote ukaenda kutekeleza mipango mingi kabisa ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la misamaha ya kodi ambayo imekuwa ni danadana tu kila mwaka. Hotuba za kutoka mwaka 2008 mpaka 2009 zinazungumza yaleyale, tutapunguza misamaha ya kodi, misamaha hii imeendelea kuongezeka. Leo ongezeko la kutoka mwaka 2010/2011 mpaka 2011/2012 ni la shilingi bilioni 800. Kwa hiyo, ungeacha tu kuendelea kutoa misamaha unge-*save* shilingi bilioni 800 kwenye misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anasisitiza kwamba Serikali inachukua hatua ya kupunguza misamaha ya kodi, katika kitabu hiki cha Waziri wa Fedha ni shilingi zisizozidi shilingi bilioni 100 ndizo tulizozipata kwa kupunguza misamaha ya kodi kati ya shilingi trilioni 1.8 ambazo ziko kwenye msamaha wa kodi sasa hivi. Kwenye sheria ya *VAT*, marekebisho yaliyofanywa tumeokoa shilingi bilioni 48 wakati misamaha ya *VAT* imefikia shilingi bilioni 801 sasa. Kwa hiyo, hakuna tunalolifanya, ni danadana tu na kama Serikali haitaki kabisa kupunguza hii misamaha ya kodi, watuambie leo kwamba hatutaki ili tuache kuwaambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya Serikali, mapato ya Serikali ni kwamba tunao udhaifu mkubwa katika chombo chetu hiki cha kukusanya kodi, udhaifu mkubwa wa *TRA*, udhaifu mkubwa sana wa Wizara katika kukusanya maduhuli, tuna udhaifu mkubwa katika kufuatilia kodi katika *multinational companies*, kuna udhaifu mkubwa wa ukwepaji wa kodi kupitia *transfer prising,* yote haya tunatakiwa kuyatafutia ufumbuzi wa haraka ili Watanzania waweze kupata fedha nyingi za kuendesha shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeng'ang'ania kodi moja ya ushuru wa vinywaji baridi, mvinyo, pombe, vinywaji vikali, sigara, ndizo hizo zinazopanda kila mwaka. Sigara mwaka jana ushuru wake ulipanda kwa asilimia 20 na mwaka huu

asilimia 10. Bia mwaka jana ilipanda asilimia 25 na mwaka huu asilimia 10. Vinywaji baridi vilipanda kwa asilimia 20 na leo ni asilimia 10. Sasa bidhaa hizi tayari wananchi wameanza kuepuka kuvitumia na ndio chanzo chetu kikubwa cha mapato cha kila mwaka ambapo ndio Serikali inategemea. Sasa kwa mwaka jana tu kwa robo ya kwanza uzalishaji wa sigara umeshuka kwa asilimia 10, uzalishaji wa bia pamoja na uuzaji wa bia ulishuka kwa asilimia 16. Kwa hiyo, tunakoenda sasa, mapato haya hata pamoja na Serikali kuendelea kubajeti na kuongeza ushuru katika vyanzo hivi lakini matokeo yake hatuwezi kukusanya fedha katika maeneo haya kwa sababu walaji wa maeneo haya wanaanza kujitoa. Mimi *strongly* sikubaliani na ongezeko la ushuru lililopendekezwa katika maeneo haya. Serikali iondoe ushuru huu tubaki kama tulivyokuwa mwaka jana na ipendekeze maeneo mengine ya kutafuta vyanzo vya mapato kuliko kung'ang'ania vyanzo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mheshimiwa Spika ambayo mimi nilikuwa mjumbe wake, kitabu kile kina kurasa zaidi ya 200, tumeandika mambo mengi ya mapato na ndiyo maana nasema kwa uhakika kwamba hakuna sababu ya kuongeza ushuru hata ule ushuru wa mafuta na tozo unaweza ukasimama tu kwa mwaka huu kwa sababu tunazo fedha nyingi mno. Kamati ya Bajeti ikakae vizuri na Serikali watafute fedha wakati wanatayarisha *Finance Bill* ili tuepukane kabisa na ongezeko hili la fedha ambazo hazina sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika usimamizi wa fedha za umma, nimpongeze sana Mheshimiwa Hosea kwa kauli aliyoitoa. Ni viongozi wachache ambao wanasimama na kuzungumza na ametuambia sisi Wabunge ili sasa sisi Wabunge tuweze kujua tatizo la kukomesha rushwa nchini likoje. Amesema wazi na mimi nampongeza sana kwa ujasiri huo kwa sababu viongozi wengi wamekuwa wakikwepa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze *CAG* wetu ambaye najua kabisa sasa hivi ni awamu yake ya

kwanza, mimi toka nizaliwe sijawahi kuona mtu *committed* kama *CAG* tuliyenae sasa hivi. Kazi kubwa anafanya, anaandika mambo makubwa ambayo ni ya kujitegemea na haogopi kitu. Nampongeza sana na nimwombee kila la kheri, Mungu ambariki katika shughuli zake zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni hili la misaada na mikopo. Mawaziri hapa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Nikushukuru sana, hakuna mwanasiasa atakayenitumia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mpina kwa mchango wako. Nilisema sasa namwita Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Khalifa ajiandae.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Tayari.

**MWENYEKITI:** Tayari umeshajiandaa?

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Ndio.

**MWENYEKITI:** Haya, sasa namwita Mheshimiwa James Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami nichangie bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nianze kwa kutoa pole kwa maafa yaliyotokea Arusha tarehe 15 Juni, 2013, waliopoteza maisha, Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi na majeruhi waweze kupona haraka. Nitoe pole kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo kwa waliyoyapata huko Jijini Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti. Kazi kubwa ya kuisimamia Serikali na kuishauri hasa

kwenye masuala ya bajeti na ukizingatia huu ndio mwaka wetu wa kwanza tangu uhuru wa Taifa letu kuanza mzunguko huu mpya wa kibajeti, ni hatua kubwa sana ya maendeleo kwa Taifa letu na inabidi tukubali kupongeza kwamba Bunge limefanya kazi kubwa kutoa mawazo kabla ya bajeti kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pato la Taifa ni takribani shilingi trilioni 55.5. Bajeti ya mwaka huu unaoanza mwezi ujao ni shilingi trilioni 18.2 ambapo wataalam wanatuambia bajeti inatakiwa angalau iwe kwenye wastani wa asilimia 20 wa pato la Taifa. Bajeti ya mwaka jana ilikuwa ni shilingi trilioni 15 na ya mwaka huu ni shilingi trilioni 18, imeongezeka kwa asilimia 29. Pato la Taifa limeongezeka kwa asilimia 6.9, uwiano unakuwa sio mzuri na mwisho wa siku hali ya Mtanzania haitakuwa na maisha yale ambayo tungetegemea Watanzania waweze kuwa nayo kwa ajili ya kuweza kuleta maendeleo kwenye Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako matatizo makubwa pia katika bajeti zetu. Bajeti yetu tukiangalia nidhamu ya matumizi na hasa matumizi ya Serikali, matumizi ya Idara mbalimbali za Serikali, matumizi kwa mfano ya Shirika la Umeme *(TANESCO)*, makusanyo yote ya ndani ya mwaka huu tulitegemea yawe shilingi trilioni tisa lakini Waziri alituambia shilingi trilioni saba, wakatuambia matumizi yote ya *TANESCO* shilingi trilioni 1.2 ambayo ni takribani asilimia 17 ya mapato yote yanaenda kwenye Shirika hili moja au *department* hii moja. Ni kweli umeme tunauhitaji kwa ajili ya uchumi wa Taifa letu lakini inabidi tujitahidi na kuwa makini sana katika kuhakikisha sekta ya nishati inapewa nafasi yake, tunatumia uwezo wetu, tunatumia uwezo wa Taifa katika kuwekeza kwenye sekta hii, lakini sio kuikubalia sekta kama hii kutumia takribani asilimia 17 ya makusanyo yote ya ndani kwenye sekta moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukazungumzia matumizi lakini je mapato? Viko vyanzo vingi vya mapato kwa mfano sekta ya uvuvi, hatujaona namna gani sekta ya uvuvi na hasa uvuvi wa bahari kuu umechangia kwenye bajeti ya mwaka huu. Kamati ya Mheshimiwa Chenge ya

kuishauri Serikali kuhusu mapato iliorodhesha kwa undani kuhusu sekta ya uvuvi na tukaweza kuonyesha na mimi nilikuwa mjumbe tukaonyesha sekta ya uvuvi ingeweza ikaliingizia mapato Serikali zaidi ya shilingi bilioni 821 kama tunakubali kuwekeza kidogo kwenye sekta hii, tukawapa nyenzo au vitendea kazi kwenye sekta hii ili tuweze kupata mapato, lakini sekta hii haijaguswa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano bajaji na pikipiki zimesamehewa kodi. Tunajua hii ni siasa zaidi na wala kweli sio uchumi kwa sababu bajaji na pikipiki hizi sio za wale wanaoendesha, sio za hawa madereva. Wako watu ambao wana pikipiki 10, pikipiki 100, wale wanaoendesha hizi pikipiki wanatumika tu ili kuleta shilingi 10,000, 10,000 kila siku na bodi ya pikipiki hizi ni wewe mwenyewe. Naishauri Serikali iangalie wamiliki wa pikipiki hizi, bajaji hizi, nayo ni sekta ya mapato, huwezi ukawasamehe tu mapato kwa sababu sio unasaidia wale vijana sanasana wale vijana unawaangamiza, wale vijana wako hospitalini kila siku, wanavunjika miguu, kila siku hali zao ni mbaya, tunaua Taifa, tunaua nguvukazi ya Taifa namna gani tunawaandalia maisha mazuri zaidi katika ajira yao badala ya kuonekana kana kwamba tumewasaidia wao, la hasha hatujawasaidia wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi kutokana na ukubwa wa injini za magari yameongezwa shilingi 50,000 kila moja. Napendekeza zibaki kama zilivyokuwa, Serikali itafute chanzo kingine cha mapato. Kwa sababu kuongeza tu kwenye sekta hii inazidi kukatisha tamaa, kodi, kodi kwenye injini za magari hizi hata wale wamiliki wa magari yenyewe, unapandisha hata teksi zenyewe, kwa hivyo maisha yanazidi kuwa magumu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza bei kwenye mafuta, dizeli shilingi mbili na petroli takribani shilingi 61, ni kwamba inaathiri sekta nyingine zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ile tozo kwenye *REA* na kwenye barabara, hiyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie vipaumbele vya Taifa. Vipaumbele viko vingi sana, tunavyo zaidi ya sita hapa lakini tungewekeza angalau kwenye vipaumbele viwili au vitatu na tuone matunda yake kwa kipindi kifupi ndio twende kwenye vipaumbele vingine. Kwa mfano kipaumbele cha miundombinu, tunawekeza sana kwenye barabara lakini je, kwenye reli tukoje, kwenye bandari tukoje. Bila ya kufungua lango kuu la uchumi ambalo ni reli ya kati, tukahakikisha tunawekeza vya kutosha kwenye reli ya kati tutakuwa tunajidanganya kuwekeza tu kwenye barabara zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano bandari ya Dar es Salaam, tukiwekeza vizuri kwenye bandari ya Dar es Salaam tukaunganisha na reli, uchumi wa Taifa letu utaenda kwa kasi kubwa. Nitatoa mfano, nchi kama ya Uholanzi, vyanzo vyao vikuu vya mapato ni bandari na usafiri wa anga, Shirika la *KLM*. Ni nchi ndogo ina watu 16,000 lakini kilomita za mraba 36,000, Tanzania tuna kilomita za mraba zaidi ya 900,000, ni kama Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Kagera ina kilomita za mraba 40,000, mji wa Uholanzi ni mdogo kuliko Mkoa wa Kagera, lakini watu 16,000 wamewekeza kwenye akili za binadamu, kwenye ubongo wa mwanadamu vizuri wameweza kupata akili vizuri wameweza kuwekeza kwenye bandari ya Rotterdam, wamewekeza kwenye Shirika la Anga la *KLM* na ndio linaongoza uchumi wa Uholanzi na wanawapa misaada nchi zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze kwenda kwenye uchumi wanasema wa kipato cha kati lazima tuangalie ufanisi wa utendaji. Kwa mfano mishahara ya wafanyakazi, wafanyakazi wetu kwenye bajeti hii wanachukua shilingi trilioni 4.7 ambayo ni asilimia 25.8 ya bajeti yote. Sawa, lakini bado Walimu hawatoshi, Madaktari hawatoshi na katika sekta zote, lakini ufanisi uko wapi, utendaji uko wapi, uwajibikaji uko wapi, bila kuchapa kazi kwelikweli tutakuwa tunajidanganya kwa sababu ndio uzalishaji mkubwa. Nishauri na tushauri tena kwamba ni vyema Serikali ikajitathmini yenyewe, ikaangalia ukubwa wa matumizi yake kwa sababu tutaongeza bajeti na Serikali nayo

inaongeza matumizi yake, siku ya mwisho kilio kinarudi palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kwenda kwenye uchumi wa kipato cha kati lazima tuwekeze kwenye elimu. Vijana wetu wajitambue, vijana wetu wawe na uwezo wa kufikiri yakinifu, *powerful reasoning,* tutawekeza leo, tutawekeza kesho hata miaka 10 ijayo ili Taifa letu liende kwenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tuwawezeshe wazawa wetu wa ndani ili tuweze tukawakamua zaidi kodi. Watu kama akina Bakhressa, akina Mengi tuwawezeshe ili waweze kuzalisha zaidi, tuwe na wazawa humu ndani hata zaidi ya mia moja ndio watakaolipa kodi na kulifanya Taifa letu kwenye sekta binafsi izalishe zaidi na tuweze kupata kodi zaidi badala ya kuangalia hizi kodi ndogo ndogo na ushuru mdogo mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie na kodi nyingine, mfano kodi ya pango. Kodi ya pango haijawekezwa vya kutosha Mheshimiwa Waziri kwa sababu ukiangalia Dar es Salaam Oysterbay yote, Msasani yote, Mikocheni yote, Mbezi *Beach,* kodi kutoka kwenye sekta hii ya majengo ikoje, bado ni finyu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mheshimiwa Khalifa Suleiman na ananiambia alishajiandaa sana toka jana halafu nitampa nafasi Mheshimiwa Aeshi, Mbunge mpya, atafuatiwa na Mheshimiwa Keissy.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na kimsingi nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake kwa kutuletea bajeti ambayo ina mabadiliko ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Ofisi ya Spika kwa kubadilisha mfumo wa bajeti au mjadala wa bajeti kama tulivyozoea na sasa tukaweza kujadili bajeti ya Wizara moja moja kabla ya kufikia mwisho, hii inasaidia kutoa mwanya kwa Serikali kufanya mabadiliko ya msingi. Naomba mfumo huu tuendelee nao pamoja na matatizo madogo madogo yatakayojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina maeneo machache nataka niyazungumzie, nianze na suala zima la misamaha ya kodi kama wenzangu walivyotaja. Mimi ninashindwa kuelewa, tuna ule mfumo wa kuwa wale wenye nacho ndiyo tunawaongezea zaidi, wale matajiri wakubwa na hasa makampuni ya uwekezaji waonatumia ujanjaujanja ndiyo wanaosamehewa kodi lakini wale wanyonge, akina Mama Ntilie na wengine ambao wanatumia jasho lao masaa 24 tunawaacha. Kama kweli tuna lengo la kuwasaidia watu wetu tungewatizama hawa kuliko kuwatazama hawa matajiri. Kwa sababu mwisho wa siku hizi fedha wala hatufaidiki nazo tunawasamehe kodi, wanakwenda kujenga katika nchi zao, matokeo yake tunaoumia ni sisi, wao wanapata fedha za bure. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama ulivyotuambia juzi hapa unasema sheria iletwe lakini huu uwezo ulionao sasa ninaomba uutizame vizuri kwa sababu mamlaka uliyonayo ukiyatumia ukiwa huna huruma utawaumiza Watanzania zaidi walio wanyonge na utawafaidisha watu wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la bandarini, nilishtuka sana juzi alipoeleza Waziri wa Fedha hapa, alisema kuna makontena 188 ambayo yaligunduliwa yana matatizo, walifanya *declaration* nyingine na bidhaa zilikuwa nyingine. Kama juzi ndio wamegundua makontena 188, huku nyuma ni makontena mangapi yalikuja kama hivi? Hawa watendaji ambao wamesababisha balaa hili mnawafanyaje, wako palepale? Hii ni sawasawa na kuwa timu imefanya vibaya unamfukuza kocha lakini wachezaji waliohujumu timu unawaacha palepale. Tumeona Mawaziri wa Fedha wameondoka, Mawaziri wa Nishati wameondoka,

wamekuja wengine lakini kweli ule uozo uliomo ndani ya Mawizara umeondoka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuna tatizo sana katika Wizara yako hasa sehemu ya kodi na hii mimi ninaamini inafanyika kwa sababu kuna watu fulani wanakula pamoja na matajiri *otherwise* isingekuwa hivi. Hivi kama juzi tu umekusanya fedha za ziada shilingi trilioni 1.2 *almost* umekusanya kwa *difference* ile uliyoipata, tumepoteza pesa ngapi huko nyuma? Hawa waliopoteza unawafanyaje? Tena matajiri wana kiburi. Nimemsikia mtu mmoja anasema alimuuliza tajiri mmoja kwa nini anafanya hivyo, akamjibu lugha moja mbaya kidogo lakini iliwahi kutumiwa na Mheshimiwa Juma Nkamia, naomba na mimi niitumie kwa sababu yeye aliitumia ikawa ni jambo la kawaida. Huyu Bwana mkubwa nasikia alisema yeye hasemi na mbwa anasema na mwenye mbwa, *that is very serious* kama anatoa kauli kama hiyo na anaachiwa. Siye wanyonge maana yake ndiyo mbwa na mwenye mbwa maana yake ni wakubwa wa nchi? Halafu watu hawa wanachekewachekewa tu, inakuwa ni vitu vya kawaida, wanadhulumu watu inakwenda hivihivi tu, lazima kuna watu wanakula nao. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, fanya *screening* katika Wizara yako *otherwise* watu wataendelea kukulalamikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka kukupa mfano hai. Leo ukileta gari kutoka nje, umelinunua wewe mwenyewe ukiwa na akili yako kwa dola 3000/=, pale kuna watu wako eti wao ndiyo wanajua zaidi kukisia gari kuliko nyie mlionunua, hivi ulimwengu wa leo kuna siri? Kampuni zote duniani zinajulikana, wanauza Toyota iliyokuwa *used* kwa pesa hizi, mimi nikija pale unaniambia hapana hili gari lina thamani ya dola 10,000 na siyo dola 3,000 ulizonunua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lengo la hiyo ni kumtisha aliyeleta gari ili ampe yeye rushwa Serikali ikose pesa. *Be transparent,* wekeni wazi kabisa, ni kwa nini watu wanadhulumiwa kiasi hiki na ninyi mnanyamaza na nyie mnawaachia watu wanafanya hivyo na mtaona pale

bandarini bidhaa zinachelewa msingi wake ni huo mtu anacheleweshwa anaambiwa nenda huku nenda huku madhumuni ni atoe pesa watu wale, wale watu watakula mpaka lini? Wengi wamekula na mwisho wameondoka tu, nilitaka niseme hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa nataka nije katika kodi za simu. Mimi ninapata taabu kidogo, makampuni ya simu hayajachangia katika pato la Taifa inavyotakiwa. Wewe unasafiri au wengi hapa tunasafiri, ukienda nje leo vocha ya simu unanunua kwa mtu maalumu siyo kama unavyokwenda kununua dagaa sokoni na ni kwa sababu zile vocha zote ambazo zinauzwa zinakuwa *programmed* kwenye komputa, Serikali inajua kuwa vocha zitakazouzwa kwa mwaka huu kwa mfano *projection* yetu ni hii na pesa tunayokusanya na yule mnunuaji wa vocha analipa *VAT* pale anaponunua vocha. Huo ndiyo utaratibu! Hamwezi kuachia vocha zinauzwa mpaka mje muambiwe na kampuni ya simu kwamba safari hii niliuza vocha milioni moja na nyie mnaridhika tu. Matokeo yake wanyonge wanaendelea kuumia kwa kutumia simu, wanyonge wanaendelea kuumia kwa kulipa kodi lakini makampuni haya yanachukua pesa yanapeleka kwao. Kwa bahati mbaya makampuni yote haya ni makampuni ya uwekezaji tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye *Bureau De Change,* nchi yenye uchumi mkubwa kama Afrika ya Kusini huwezi hata siku moja ukaenda kubadilisha pesa kienyeji, ni lazima ukabadilishe benki kwa kutoa *Identity,* utoe *passport* na vielelezo vingine. Hapa kwenye *Bureau De Change,* Mheshimiwa Waziri hebu fanya utafiti, ni ngapi zinazotoa risiti tu kwa mfano. Hivi uholela huu, uhuru huu, uhuria huu, mimi siiti uhuria ninaita uholela utatufikisha pabaya sana lazima eneo hili mliangalie kwa sababu mimi nina wasiwasi kuwa linatumika vibaya. Hawa watu wasingefanya vile, ni lazima kuna kitu wanafaidika nacho. Unakwenda unabadilisha fedha ama unanunua au unauza hakuna risiti yoyote. *Government is runned by papers* na siyo maneno, *Government* inafanya kazi kwa makaratasi, kwa maandishi na risiti ndio maandishi yenyewe, Mheshimiwa Waziri wa

Fedha mbona mnaachia vitu vya namna hii? Matokeo yake ndiyo hayo kama nilivyosema toka mwanzo likiharibika sana anayeondoka ni Waziri lakini uozo bado upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nataka sasa nije katika hoja ambayo inatuumiza tulio wengi sana. Bajeti iliyopita ya mwaka 2012/2013, ushuru wa ngano kwa mujibu wa bajeti hapa ulikuwa ni zero, mara hii umepandishwa kwenda 10% matokeo yake ni nini? Unga wa ngano utapanda kwa shilingi 228/= kwa kilo. Tena bahati mbaya sana keshokutwa kuna Mwezi wa Ramadhani jamaa wanaofunga watasema mnawaonea makusudi na mimi ni mmoja wao nitasema hawa jamaa wanapandisha makusudi kutuumiza sisi tusile unga wanataka tule mihogo kila siku. Hebu litazame eneo hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo siyo hapo tu, hivi viwanda ambavyo ulivizoesha mwaka jana hapakuwa na kodi leo unapandisha kodi ya ngano, unategemea nini? Hivi viwanda vyetu unategemea nini, wakati wao hawauzi hapa tu wanauza na sehemu zingine za jirani, maana yake ni nini? Unapopandisha bei ya mafuta *automatically* unasababisha mfumuko wa bei, ukigusa sekta mbili hizo maana yake unasababisha mfumuko wa bei. Naomba uliangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa nirudi katika hali halisi iliyoko bandarini hivi sasa. Bandarini hivi sasa utaratibu mpya ulioanzishwa wa kufungua bidhaa au kufungua makontena ambao naunga mkono sana kwa sababu utatusaidia, lakini hao wanaofanya kazi wafanye kazi kwa uungwana, siyo wanafungua bidhaa za watu halafu wanaacha shaghalabaghala, bidhaa ya mtu A anaipata mtu B, bidhaa ya mtu B anaipata mtu C, *why* mnawaadhibu watu wasiohusika? Hivi nani aliyekuwa hawezi kufungua kontena akajua bidhaa hii ilifungwa hapa akaweza kuifunga ilivyokuwa. Au walioko bandarini wamekereka kwa kufungua makontena wameamua kuwaadhibu watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho usichukue muda mwingi, wale wanyonge wajasiriamali walio na dola 3000 au

4000 waliokwenda kuchukua bidhaa, wanataka watoe, wauze wapate kwenda tena. Leo likikaa kontena siku chungu nzima pale bila kumalizika masuala ya kupata mtu mzigo wake unamtesa bure tu, mtawapandisha watu sukari, mtawapandisha watu *pressure* na mwisho wa siku watakaoumia ni wanyonge lakini wale Mabwana walioko pale Bandarini wanaendelea kufaidika kwa vitendo vyao hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendesha nchi kunahitaji busara ambayo mie nina hakika mnayo lakini kitu cha msingi, suala la kuoneana haya siyo zuri sana kwa sasa. Tunahitaji kufanya maamuzi magumu kwa sababu ukimtoa rafiki yako aliye Bandarini unaumia wewe lakini ndiyo maamuzi yenyewe hayo. Zenawi aliyekuwa Waziri Mkuu wa Ethiopia alimfunga jela *righthand men* wake kwa sababu alimgundua amefanya vitendo ambavyo siyo vya kawaida. Hakuchukua muda bahati mbaya na yeye amekufa lakini ame-*act,* kila mtu ameona. Sasa na sisi tusione haya Mheshimiwa fukuzeni watu wanaoharibu, ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Khalifa, Waheshimiwa Wabunge ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Aeshi na Mheshimiwa Keissy ajiandae.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii kuongea kwa mara ya kwanza tena kuwakilisha wananchi wa Jimbo la Sumbawanga Mjini. Niwashukuru wananchi wote wa Jimbo langu na Watanzania wote kwa ujumla kwa Dua zao na Sala zao. Pia nawashukuru Wabunge wote pamoja na Mheshimiwa Spika, pamoja na wewe kwa kunipa nafasi hii siku ya leo kuweza kuchangia ili kuwawakilisha wananchi. Ni muda mrefu, kwa mara ya kwanza, naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake kwa bajeti nzuri waliyotuletea mwaka huu, nawapongeza sana. Pili,

niwapongeze *TRA* kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kukusanya kodi, niwapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakwenda moja kwa moja kuzungumzia masuala ya umeme, kwetu sisi ilikuwa kero lakini ninaomba niipongeze Wizara ya Nishati na Madini kwa kutusambazia umeme vijiji vyote lakini nilikuwa ninaiomba tena Wizara hii kwa sababu kuna mpango wa umeme kwenda Kalambo, namwomba Waziri Vijiji vyote vile vilivyoko njiani Mtimbwa, Matanga na Kisumba umeme uweze kushuka pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda moja kwa moja kuzungumzia kuhusu dizeli. Dizeli hii tumeipandisha bei shilingi 200/=. Kabla sijavuliwa Ubunge tuliwahi kuliongelea hili, tukakubaliana tuongeze bei ya mafuta ya taa na ya dizeli zifanane ili tuzuie uchakachuaji wa mafuta lakini tumelirudisha tena. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, hii bei ya mafuta iliyopanda, hizi Sh.2/= naomba uziondoe, tunarudi kulekule kwenye uchakachuaji na uharibifu wa mitambo na hususani magari ya mizigo. Magari yale wafanyabiashara wanayakopa lakini *unit* moja ikiharibika ni milioni moja na laki tano kwa hiyo *unit* ya gari sita ni karibuni milioni tisa huyu mtu aliyekopa gari benki hawezi kulipa matokeo yake uharibifu unaongezeka siku hadi siku. Nakuomba Mheshimiwa Waziri hili mliangalie upya hii Sh.2/= itafutieni pa kuipeleka kwenye mafuta ninaomba muitoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilihili la mafuta ambalo ningeomba nipate maelekezo kidogo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba jumla ya tozo zote za kodi kwenye dizeli ni shilingi 530/=lakini pale kuna *JetOne* na tusipoiangalia itaingia moja kwa moja kwenye uchakachuaji wa mafuta. Vilevile kuna msamaha wa kodi ya dizeli kwenye migodi, yote ile itaingia moja kwa moja kwenye dizeli. Sasa mtueleze *EWURA* na *TRA,* mmepanga *formula* ipi ambapo mtaweza kudhibiti haya mafuta yasiweze kuchakachuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo,

nitakwenda moja kwa moja kwenye hizi *NGOs* zetu. Naomba Mheshimiwa Waziri hili aliangalie kwa makini sana. Hawa watu wenye *NGOs* sijui FUNIKA, TUNAKOPESHA, *PRIDE* wanawakopesha wananchi wetu hususan Walimu kwa maneno mazuri sana lakini wakati wa kuja kudaiwa riba yao ni kubwa mno takribani 25% mpaka 30% matokeo yake huyu Mtumishi wa Serikali atadaiwa miaka yote mpaka miaka 30 hajaweza kulipa lile deni. Kwa hiyo, niwaombe hizi riba za kwenye hizi *NGOs* zimekuwa kubwa, zidhibitiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara ya Fedha na *TRA* kwa kukusanya kodi lakini matumizi yake tumeshindwa kuyadhibiti. Matumizi ni makubwa kuliko makusanyo. Wizara inajitahidi sana kukusanya pesa lakini utumiaji wa zile fedha hautekelezeki, nitatoa mfano. Kule Sumbawanga kuna nyumba zetu za Serikali, zipo nyumba 18, ziliachwa na mradi wa *RUDEP*. Zile nyumba zimechukuliwa na mtu binafsi matokeo yake mtu binafsi huyo amepanga Serikalini na yeye anawapangisha Watumishi wa Serikali kwa bei kubwa ambayo haiwezi kuvumilika. Leo hii tunapata Mawaziri wanakuja katika Majimbo yetu wanaenda kukaa hotelini lakini tuna nyumba 18, nyumba mbili tunaweza kuzifanya *rest house* viongozi wakafikia pale tuka–*save* gharama. Leo hii Majaji wetu wanakuja Sumbawanga hawana pa kukaa wanakaa uswahilini nyumba ya Serikali amepewa mtu binafsi, hainiingii akilini. Hizo nyumba zina miaka takribani 15 amepewa Mzee Mzindakaya anazimiliki, yeye ni nani wa kumiliki nyumba za Serikali? Watu wa Serikali anawapangisha yeye kwa nini Serikali isipangishe moja kwa moja? Hili linanipa shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Magufuli baada ya kupata taarifa hizi jana ametoa maagizo na mkataba huo umevunjwa, Mheshimiwa Magufuli ninaomba nikupongeze sana. Ndiyo mfano tunaotaka, ndiyo Mawaziri tunaowataka baada ya kupata taarifa wanachukua hatua hapohapo. Mheshimiwa Magufuli, sina cha kukulipa, naomba nikupongeze sana, tunawahitaji sana Mawaziri kama nyie. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mungu atamlipa.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbali, tuna kero ya maji lakini naomba niipongeze Wizara na Serikali kwa kuogeza bajeti. Tuna bwawa letu la maji la Serikali limechimbwa ndani ya shamba la Mheshimiwa Mzindakaya. Sasa nataka nimuulize Waziri wa Maji akifika hapa atueleze, wananchi wa Jimbo langu hususan Fyengelezya, Jimbo la Mheshimiwa Mipata, ni lini wataanza kutumia maji yale kuliko sasa hivi wanaoshea ng'ombe na kunywa maji ng'ombe. Namwomba Mheshimiwa Waziri akirudi atuelekeze na atuambie ni lini wananchi wa Fyengelezya wataanza kutumia maji yale ambayo ni bwawa la Serikali limechimbwa kimizengwe ndani ya shamba la mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitaomba sana katika haya mawili kwanza nipatiwe majibu hususan la kwanza Mheshimiwa Waziri ameshavunja mkataba ule na naomba kabisa Mheshimiwa Waziri zile nyumba zikirudi, wapewe viongozi wetu, wapewe Majaji, wapewe Wakuu wa Idara lakini nyumba mbili ziweze kujengwa *rest house* kwa ajili ya viongozi wanaofika ndani ya Mji wetu wa Sumbawanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kwenye kilimo. Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa Mkoa minne inayolima na kuzalisha mazao mengi ndani ya nchi yetu. Nasikitika sana. Katika Mkoa ambao hauna trekta, hauna vifaa vyovyote vya kilimo, ni Mkoa wa Rukwa. Hainiingii akilini, Mkoa wa Rukwa una trekta sita tu ambazo zililetwa na Serikali, mimi hainingii akilini sana. Mikoa mingine ambayo hata hailimi ina trekta 100 mpaka 200 sisi Sumbawanga tumelogwa? Nini tatizo la Sumbawanga? Hii inanipa shida sana. Nadhani Waziri wa Kilimo na Waziri wa Fedha wanalisikia hili kuwa wakulima wetu wana trekta sita na trekta zilikuja kwa masharti magumu, wakulima wameshindwa kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hakuna mtu mwaminifu, mkarimu kama wananchi wa Mkoa wa Rukwa

lakini matrekta haya hawajakopeshwa na ninaamini kabisa kuwa wakikopeshwa watalipa lakini mpaka leo tangu tumeanza Kilimo Kwanza tuna matrekta sita, mawili yamewekwa kama *show,* manne yamekopeshwa kwa watu waliokuwa na uwezo, siyo kuwa ilikuwa ni *target* kuwakopesha hata wasiokuwa na uwezo. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri unayenisikiliza hili liangaliwe kwa umakini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nilikuwa nimelenga maeneo yote ambayo ni muhimu, kwa sababu ndiyo mara ya kwanza kuingia Bungeni, nitajipanga upya, nitawaletea na mengine. Mwisho, niwapongeze wote kwa kuniombea Mungu lakini ninarudia tena Mheshimiwa Waziri Magufuli ninakupongeza sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Aeshi na nafikiri Mheshimiwa Magufuli amesikia kule nyuma alikokaa leo, namwona yupo kule nyuma anapongezwa, sasa sijui anapongezwa kwa pongezi hizi ama kuna pongezi nyingine. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo. Mimi hii bajeti ya Wizara ya Fedha siiungi mkono mpaka nipewe maelekezo ya nitakayoyasema hapa mbele ya Bunge lako Tukufu. Tumechoka Watanzania kufanywa kama vikaragosi huku wengine wanastarehe kama wapo peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia hizi pesa walizowa-*guarantee* watu wenye viwanda na mashamba makubwa, shilingi trilioni 1.25. Mpaka sasa shilingi bilioni 253.9 zimepotea, hazitalipwa. Wapo, wamestarehe katika nchi hii na watoto zao. Hizi pesa shilingi bilioni 253.9 ni sawa na bajeti ya Polisi, mishahara ya Polisi na pamoja na matumizi ya Polisi lakini ziko kwa watu wachache wamestarehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa zingine nataka kujua *import support,* shilingi bilioni 300, hizi pesa na Wabunge na Mawaziri wengine wanahusika, leo ajabu eti nyaraka zimepotea Hazina! Ni jambo la kushangaza kabisa hata muuza nyanya hawezi kupoteza *documents*. Leo tunahangaika hapa tuwanyonye wananchi kwa kuwadai kodi wakati mabilioni ya hela zililetwa na Japan kupitia Mitsubishi Bank! Serikali leo inakaa inawalipia watu wachache, wengine wamekaa humu Bungeni, wengine wamejenga baa, wamejenga hoteli na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana. Bila majibu sahihi, sitakubali na Wabunge mniunge mkono. Wabunge wengine wamo humuhumu walikuwa wanapeleka maombi Hazina kuchukua hizo dola laki mbili, wanaandika wake zao, watoto wao wanapata mabilioni ya hela, leo wanasema *documents* zimepotea! Ni uchungu unaweza kulia! Watu wanabaki wanastarehe, tunawakamua wananchi wenye vioski vidogovidogo kwa kuwatoza kodi, akina Mama Lishe lakini watu wameteka hela benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo Mbunge jana amesema tuzalishe mabilionea Tanzania, ndugu yangu, tuliwawezesha hizo shilingi trilioni 1.25 zipo wapi? Waziri ninataka hizo pesa zirudi kwa wananchi. Tunakaa tunatafuta misaada kwa Wazungu, tunalia kwa Wazungu, mwisho watupe masharti magumu ambayo hatuyawezi, tutaumizana. Tutafutieni hela zetu ambazo zimechukuliwa na baadhi ya Wabunge, baadhi ya Mawaziri na baadhi ya ndugu zenu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hapa Wabunge wanazungumza ufujaji wa hela za Serikali kuhusu magari aina ya Shangingi. Ndugu zangu si kweli. Waziri hawezi kutoka Dar es Salaam mpaka Namanyere kule atumie gari yenye CC 3000, hawezi! Hizi gari Shangingi nilizungumza hata na Waziri wa Fedha alipokuwa Mkulo, nilimwambia hizi gari bei yake ni dola 83. Mimi mwenyewe nimenunua mpya.

**MBUNGE FULANI:** 83?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Dola 83 na hela ya Tanzania ni shilingi milioni 88. Leo mnamsema kuna gari ya shilingi milioni 300, iko wapi? Hakuna gari ya shilingi milioni 200 wala gari ya shilingi milioni 300. Mimi nina ushahidi na risiti nitakuletea na *documents* ninazo, gari ni mpya kwa shilingi milioni 88. Leo mnatudanganya magari bei kubwa kumbe mna mkate wa watu wakubwa na Wizara ya Fedha imekaa tu. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vipaumbele sita. Ndugu zangu twende Kigoma, Tabora, Mwanza, Shinyanga na Mpanda, tuwaulize watu wa Mpanda, Kigoma na Mwanza mnataka reli au viwanja vya ndege? Mtashangaa wenyewe. Vipaumbele gani mnapeleka viwanja vya ndege, mtu wa Tabora gani anapanda ndege kama siyo Mbunge na Mkuu wa Mkoa? Mtu gani wa Kigoma anapanda ndege kama si Mbunge au *DC* au Mkuu wa Mkoa? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kigoma kipaumbele chao ni treni, wananchi wa Mwanza ni treni, wananchi wa Tabora ni treni, wananchi wa Mpanda ni treni, hawataki viwanja vya ndege, viwanja vya ndege baadaye, kwanza ndege zenyewe zipo wapi? Mna ndege nyie? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaweka vipaumbele mabilioni ya hela mnajenga viwanja vya ndege kuvitunza kwenyewe gharama, ndege zenyewe hatuna, wapanda ndege ni nyie peke yenu Wabunge na Mawaziri. Leo Mama wa kule Igungu atapanda ndege, mama wa Mwanga atapenda ndege, mama wa Mwandiga atapanda ndege, mtu wa Kale atapanda ndege? Jamani, tututulie, tuweke vipaumbele ambavyo vinaweza kusaidia wananchi na uchumi wa nchi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtapakia madebe ya mawese kwenye ndege? Mtapakia migebuka kwenye ndege? Kipaumbele cha kwanza ni reli. Acheni mambo ya kurukiarukia, ndege zenyewe hamna. Mmefilisi Shirika la Ndege tunawaambia tuwakamate waliofilisi tuwafunge

pingu zao, sasa sheria mpya ije kama wamekufa tuwafufue, tuwasage mifupa yao. Tunawaangalia tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge hapa sijui Kamati gani itakayoipongeza Kamati iliyokataa *National Housing* wasitolewe *VAT*. Ndugu zangu, tutaandamana nchi nzima. Wananchi wa Nkansi hawategemei nyumba za *National Housing*, tunategemea kujenga nyumba zetu wenyewe, hili wazo la kusema *National Housing* wafutiwe *VAT* liacheni, hatutalikubali. Kama kufuta *VAT* iwe ni kwa nchi nzima na mkifuta kwa nchi nzima Serikali itapata wapi pesa? Mimi nashangaa baadhi ya Wabunge wanakuja hapa wanasema tuondoe hela hii, utapata wapi hela ya kuendeleza nchi yako? Wewe unasema tu toa hela hii, eleza tupate wapi pesa. Mnataka Wazungu wakamuliwe kodi wakuletee wewe Tanzania hapa, umekaa unastarehe, ukiletewa unazila. Ni lazima tukamuane kwenye kodi hapa ili nchi yetu isitegemee Wazungu. Tujikamue, tufunge mikanda wenyewe. Wewe unasema tutoe shilingi mbili huku tafuta hiyo shilingi mbili utairudishaje huku, ndiyo tukusifu. Wakati huohuo unadai barabara, unadai maji, unadai kila kitu, leo unasema tufute hiki, watapata wapi hela? Eleza baada ya kufuta, watoe wapi hela, tuna Wajomba lakini Wajomba watachoka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Ethiopia wamekubaliana kujenga bwawa kubwa la pili katika Afrika kutoka Congo, lakini wamekubaliana wenyewe kwamba kila mtumishi achangie mshahara wake wa mwezi mmoja wajitegemee wenyewe. Leo sisi tunakurupuka hapa hatuna cha kueleza Serikali, unakuja hapa unasema toa hiki toa hiki. Faida ya bajeti ni kuieleza Serikali tupate wapi pesa, tumejaza televisheni. Leo Uingereza nchi tajiri ambayo tunaitegemea sisi hakuna *TV* isiyolipiwa, kodi ya *TV* ukiwa nazo tatu utalipia, ukiwa nazo nne utalipia na ndiyo tunaenda kuomba hela kwao. Wewe una *TV* kumi mpaka chooni umekaa hulipii chochote, nani akudai? Ni lazima tuongeze kodi na *TV* zote zilipiwe. Chochote kinachowezekana tuongeze, tujenge nchi yetu sisi wenyewe. Hii bajeti tegemezi tuiache ndugu zangu. Deni litaongezeka mwaka hadi mwaka. Ni lazima tujifunge

mikanda tutafute sisi wenyewe cha kuongeza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yeyote anayechezea pesa zinapoongezeka adhabu yake ni kifo na kunyang'anywa mali yake. Kwanza, tunamnyang'anya mali yake na kifo kinamfuata, tuwe wakali. Hatuwezi sisi kujikaza mikanda na wengine wanakaa Kilimanjaro Hoteli, hakuna hicho kitu, ni lazima tubane, tuwe madhubuti na tuwe waadilifu. Uadilifu ukianza kwa adhabu, nimeshukuru baada ya kusema adhabu ya kifo, Wabunge wengi wameanza kuniunga mkono kila nikiwasikia wanatanguliza adhabu ya kifo. Hata Mzee Samuel Sitta siku moja nimemsikia anasema hawa dawa yao ni kuwanyonga. Kwa hiyo, msidhani ni mimi peke yangu, wengi wanataka hiyo sheria iletwe hapa ili tuwadhibiti wanaochezea mali ya umma na mali inaonekana, mafisadi wanajulikana ndugu zangu, mimi Mbunge hapa baada ya mwaka nina ghorofa kumi nimepata wapi hela? Sijakwenda benki, sijakwenda popote, hapohapo ndipo pa kunibana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi pesa zinazochangiwa kwenye maharusi mabilioni ya hela, kwenye misikiti na makanisa zikatwe kodi asilimia thelathini palepale. Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mgimwa, hela zote zinazokwenda kufanyiwa harambee, ni lazima zikatwe asilimia thelathini ili tupate kodi. Michango ya harusi siyo michango ya shule, ni starehe zako mwenyewe na yenyewe ikatwe kodi asilimia thelathini. Wauza madawa ya kulevya kama hawajakamatwa lakini wana majumba wakatwe kodi. Shida yetu sisi ni kodi hatujui dawa zako unapeleka wapi huko na tumeshindwa kukukamata lakini tulipe kodi, hamna kuwaachiachia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tujitegemee hakuna kusema bajeti hii mbaya, bajeti hii endelee ili na sisi kesho na keshokutwa tusiombe msaada, waje wengine watuombe msaada. Miaka hamsini na sisi watuombe na wengine msaada. Siyo tunaenda kuomba msaada wa barabara, tunalia maji, tunalia dawa na sisi wengine waje

kutuomba msaada. Tukipata maafa kidogo misaada, leo tukisema kodi mnapiga kelele ninyi Wabunge, ebo! Itakuwaje? (*Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani ameoa mwanamke nyumbani kwake anakwenda kuomba msaada kwa jirani, watakuchukulia mke wako! Jitegemee! Unaanza kuoa, una nyumba unajitegemea. Chumvi unaomba kwa jirani, maji unaomba kwa jirani, chai unaomba kwa jirani, ni mke wako huyo? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na sisi ni lazima tuwe na bajeti ya kujitegemea ili tusiendelee kunyanyaswa. Leo masharti yameshaanza kuwa magumu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, ni kengele ya pili.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Tutakutafutia muda mwingine baadaye.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Nimalizie mengine. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge huyo ndiye Mheshimiwa Keissy, amemaliza kuchangia mchango wake, tunaendelea na mchangiaji anayefuata Mheshimiwa Sara Msafiri.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuipongeza Serikali yangu kwa kuwa sikivu, imeweza kuongeza shilingi bilioni 513 kwenye Wizara mbalimbali kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Wizara ya Maji imeongezewa

shilingi bilioni 184, Umeme Vijijini wameongeza shilingi bilioni 186. Pia wameweza kuongeza pesa kwenye Mifuko ya Maendeleo ya Vijana ambapo kwenye Mfuko wa Vijana wameongeza shilingi bilioni tatu na Mfuko wa Akina Mama wameongeza shilingi bilioni mbili. Napenda niipongeze sana Serikali na niwaombe vijana wenzangu wajiunge na vikundi vya ujasiriamali ili waweze kukopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali imeweza kutenga vikundi zaidi ya 200 kwa ajili ya kujishirikisha kwenye miradi ya kilimo na wameweza kuchukua vijana ambao wamemaliza Chuo Kikuu hasa Chuo cha Sokoine Morogoro ambacho kinajishughulisha na Kilimo. Huu ni mpango mzuri sana kwa sababu ninaamini kabisa tatizo la ajira litaweza kutatuliwa kama vijana ambao ni wasomi watajikita kwenye sekta ya kilimo na tunajua ardhi ni mali na kilimo ni mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niende sasa kwenye ukuaji wa uchumi wa nchi. Sekta ya mawasiliano kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tumeona imekua kwa asilimia 20.6 kwa mwaka 2012 na imechangia kwenye pato la Taifa asilimia 2.3 tu. Ukiangalia kwenye sekta ya kilimo ambayo inakua kwa kiasi kidogo sana, imeweza kuchangia asilimia 24.7. Kwa kweli, hii ni *indication* mbaya sana, kwa sababu tunajua kwamba wakulima wa Tanzania ni *peasant farming,* wanalima kwa kutumia jembe la mkono na mazingira ya kilimo tunayajua wote. Sekta za mawasiliano ambazo zina uwekezaji mkubwa na tunaambiwa zimekua kwa kiwango kikubwa, lakini mchango wao kwenye pato la Taifa ni asilimia mbili, hii si sawa kabisa. Hii inaonesha kwamba maskini ambao ni wakulima ndiyo wanaolipa kodi lakini makampuni makubwa ya uwekezaji yanakwepa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu Wabunge watakuwa ni mashahidi, haya makampuni ya madini, kwa mfano kuna viwanda vya sukari kule kwetu Mvomero, hawalipi ile asilimia tatu pamoja na kwamba ipo kisheria. Imekuwa ni mgogoro kati ya Halmashauri na imekuwa ni

mgogoro kati ya wenye kiwanda na wakulima. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijielekeze kukusanya mapato ambayo tumeshayapitisha na yapo kisheria ili tuweze kufanya *enforcement* kwenye sheria tulizoziweka, waweze kulipa kodi hawa Wawekezaji. Haiwezekani tukaendelea kutegemea kodi kupitia kwa mkulima wa jembe la mkono, tukaambiwa hapa wanachangia asilimia 24.7 wakati kilimo chao bado hatujakikomboa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, niweze kwenda kwenye pato la Taifa. Kwanza, niipongeze Serikali imekuwa na mipango mingi sana ambayo imelenga kunyanyua pato la nchi na kipato cha Mtanzania mmojammoja. Ukisoma takwimu zinavyoonesha, mwaka 2011 pato la Taifa lilikua kwa asilimia 6.4, mwaka 2012 asilimia 6.9, mwaka 2013 tunatarajia pato la Taifa likue kwa asilimia saba (7%) ambayo ni *decimal* moja tu kutoka mwaka 2012 ambayo ilikuwa asilimia 6.9. Mwaka 2014 tunatarajia pato la Taifa likue kwa asilimia 7.2 ambayo ni *decimal point* mbili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuwa na mipango mizuri, tuna mpango wa kitaifa wa maendeleo wa miaka mitano ambao ni mpango unatekelezwa kila mwaka, pamoja na kuja na mpango wa *Presidential Delivery Bureau* ambao tunasema *Big Result Now*, lakini bado tunakuwa na *projection* ndogo sana ya kukua kwenye pato la Taifa kwa *decimal points* na tumelenga kusimamia kukusanya kodi, kuwa na ufanisi kwenye kazi na kuhakikisha miradi ya maendeleo inakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona kwamba hapa tumekuwa na mipango mizuri lakini tunaanza na *wrong step* kwenye *projection* zetu. Kuendelea kutegemea pato la Taifa likue kwa *decimal points* mbili au moja wakati tuna mipango mikubwa mizuri ya nchi, sisi hatutegemei kuambiwa kwamba inapofika mwaka 2014 tumeweza kufikisha malengo yetu kwa asilimia mia moja kama *projection* zinakuwa ndogo hivi. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ifanye *review,* iangalie upya kwenye *projection* zake kwa sababu tuna mipango mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende katika suala ushuru wa bidhaa katika huduma za simu, *all mobile services*. Hapa tupo kwenye masuala ya E*ast Africa,* wenzetu nchi zote za *East Africa* wao wanatoza asilimia 10 tu kama *excise duty.* Mwaka jana tuliongeza kutoka asilimia 10 mpaka asilimia 12 kwenye *airtime* leo tunaambiwa kwamba ni asilimia 14.5 kwenye huduma yoyote ile inayotolewa na huduma za simu za mkononi ikijumlishwa na huduma za *Tigopesa* na *Mpesa* ambapo mimi najua msingi wa kuanzisha hizi huduma ilikuwa ni kuwafikia Watanzania ambao ni maskini, wapo vijijini, hakuna huduma za pesa, hakuna mabenki. Leo tunawakata kila huduma asilimia 14.5, hapa hatuwatendei haki Watanzania, tunawanyima uhuru wa kupata mawasiliano hasa huduma za *internet*, huduma za fedha ambazo ni ndogondogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tumeamua kuongeza Mfuko wa Elimu, tuchangie elimu, imekuwa huyu mkulima wa kijijini ndiyo anatakiwa achangie mfuko wa elimu? Watu wana pesa benki, wana-*account* benki, wana-*transfer* hela *free*, ku-*deposit* hela, kuhamisha hela upande mwingine ni bure, hakuna kodi kubwa kama hizi, kwa nini wakulima na wananchi wa kipato cha chini wanaotumia huduma hizi za Mpesa ndiyo wachangie kodi hii kwenye masuala ya elimu, halafu wale *Big Fish,* wale wenye akaunti benki hawakatwi na hawachangii chochote? Naomba Serikali iache kuongeza kodi kwenye huduma hizi, kwanza zinasaidia wanafunzi kutafuta mawasiliano na *data* mbalimbali kwa ajili ya elimu kwenye huduma za *internet*. Hii siyo sawasawa na mimi ninaamini kabisa ukipitisha hili huduma za Mpesa zita-*collapse* na hazitaweza kuendelea. Huwezi ukamtumia mtu kijijini Sh.20,000 anakatwa asilimia 14.5, *then* atapata nini? Gharama yote inaenda kumlalia mlaji ambaye yupo kijijini, siyo sawasawa. Naomba huduma zikatwe kwenye mabenki makubwa, watu wenye akaunti kule ndiyo wakatwe hizi huduma lakini siyo wananchi vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie kwenye kupunguza kiwango cha chini kutoza kodi kwenye masuala

ya ajira. Kupunguza asilimia moja tu ni ndogo sana, haina *impact* yoyote kwa mfanyakazi. Wafanyakazi hawa tunajua wana madai mbalimbali wanaidai Serikali, kama Serikali inadhamiria kuleta unafuu, kuwapunguzia gharama mbalimbali, hebu tupunguze hata iwe kwenye asilimia nne itoke kwenye asilimia 14 ije kwenye asilimia 10 ili yule mfanyakazi wa chini aweze kuona mabadiliko kwenye mshahara wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuliongelea ni suala la kilimo. Wakulima wamekuwa wanachangia sana kwenye hili pato la taifa lakini kuna mazingira yanawabana kwenye kilimo. Kwa mfano wananchi wangu wa Wilaya ya Mvomero wanalima miwa. Miwa mingi inaharibika, kile Kiwanda cha Turiani cha Mtibwa hakina uwezo wa kununua miwa ya wakulima. Wakulima mwaka juzi wamepata karibia hasara shilingi bilioni mbili, miwa imeoza shambani. Kiwanda hakiwezi kununua miwa yote lakini wakulima wanapohitaji kiwanda kingine kwa ajili ya kuuza miwa yao wanayozalisha tena wanakopa kwenye *SACCOS* na kwenye mabenki, miwa inaharibika wanaambiwa na Serikali, sheria hairuhusu kujenga kiwanda karibu na kiwanda kingine eneo moja. Hii sheria haiko rafiki kwa wakulima. Wakulima wameamua kujitegemea, wameamua kulima kisasa, analima eneo dogo, anapata miwa mingi. Kwa nini tunaendelea kuzitegemea hizi sheria, hatutaki kuzibadilisha ili zilete unafuu kwa mkulima ambaye ameamua mwenyewe kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba kabisa pamoja na kukuza pato la Taifa lakini tuangalie yule mwananchi wa chini mkulima kero gani anaipata kwenye masuala ya kilimo. Mimi naamini kabisa tukiweza kubadilisha sheria kama hizi, wananchi watalima miwa ya kutosha, watakuwa na uhakika wa soko, watakuwa na uhakika wa kurejesha hela walizokopa kwa ajili ya kilimo lakini kuendelea kukumbatia sheria ambazo haziko rafiki kwa mkulima, haziko rafiki kwa mabenki, wanashindwa kuwakopesha wakulima kwa sababu wanajua kiwanda hakina wazo la kununua miwa. Mimi naomba kabisa, tubadilishe hizi sheria ili ziwe rafiki kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Kidawa Saleh atafuatiwa na Mheshimiwa John Mnyika ambaye simwoni, kwa hiyo atazungumza Mheshimiwa Machali.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naanza kwa kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwa sikivu. Wabunge wengi waliomba baadhi ya mafungu yaongezewe bajeti, Serikali imefanya hivyo, imeongeza fedha katika sekta ya maji karibu shilingi bilioni 184. Hii ni sekta muhimu sana, watu wote wanategemea maisha yao katika sekta hii. Akina mama walikuwa wanateseka sana katika kutafuta maji. Wengine ndoa zimevunjika kwa sababu ya kutafuta maji. Anahangaika kutafuta maji usiku na mchana, akifika nyumbani anapigwa magumi na mateke, ulikuwa wapi, kwa nini umechelewa na ndoa zinavunjika. Hapa tunashukuru Serikali imesaidia sana kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeongeza fedha katika sekta ya mifugo na uvuvi na hapa tunajua kama watu wengi wanategemea maisha yao katika sekta hii. Hakuna mabwawa, majosho, kwa hiyo, kuongezwa fedha katika sekta hii kutasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile *TBC* imeongezewa fedha. Tunalalamika hapa usikivu haupatikani katika maeneo mengine, nao wameongezewa fedha, Serikali tunakushukuru sana kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachoomba, Serikali mnadaiwa sana na *TBC*. *TBC* ina madai mengi kwenu, mnajikopesha wenyewe. Taasisi za Serikali pamoja na Wizara mnapeleka matangazo yenu *TBC,* yanatolewa halafu hamlipi. Kwa hiyo, tunakuombeni sana Serikali mlipe fedha hizi kwa *TBC* ili iweze kutekeleza majukumu yake kama yalivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya bajeti. Bajeti ya mwaka 2013/2014, imepanga kukusanya fedha shilingi trilioni 18.2 mapato yote lakini mapato ya nje ni shilingi triliioni 3.2, huu ni utegemezi wa asilimia 20.8. Nilijaribu kulinganisha na utegemezi kwa mwaka huu wa fedha unaomalizika kwa maana mwaka 2012/2013 ambapo utegemezi ulikuwa ni asilimia 21. Kwa hiyo, hapa ukiangalia hakuna upungufu wowote ambao tunaweza tukajivunia kuwa Serikali imepunguza utegemezi, ni *just* asilimia 1.8 ndiyo upungufu uliotokea. Kwa hiyo, kuna kazi kubwa sana ya kufanya kukusanya mapato ndani ya nchi yetu ili kuweza kujitegemea kupata fedha za kutosha kugharamia matumizi yetu ya kawaida na ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa mapato baina ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanachukua mara tatu zaidi ya matumizi ya maendeleo. Kwa maana ya matumizi ya kawaida ni asilimia 69 na matumizi ya maendeleo ni asilimia 31. Tunashukuru kuwa kuna kiwango kimeongezeka kidogo kulingana na mwaka jana lakini malengo hasa ni kufikia walau kwenye matumizi ya maendeleo asilimia 35. Mwaka jana tulipigia kelele sana tukasema Serikali ijitahidi ifikie kiwango hicho lakini kuna mwelekeo kwa sababu mwaka huu ni asilimia 31, tujitahidi mwakani ifikie walau asilimia 35 ya lile lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hayo matumizi hayawezi kufanikiwa kama hatukukusanya mapato ya kutosha. *TRA* tunaipongeza inafanya kazi mzuri na Idara moja tu ya Forodha inategemewa kukusanya asilimia 20 ya mapato yote ya nchi hii. Kwa hiyo, ikizembea kidogo tu mapato ya nchi yetu yatatetereka na maumizi yatatetereka. Kwa hiyo, yale madai ambayo tunasema yaongezewe fedha na mengineyo hayataweza kupatikana. Kwa Idara moja tu. Siwezi kueleza sana hapa kwa sababu wengi wameshaelezea madudu yanayotokea katika Idara ya Forodha. Tunaomba viongozi wa Serikali pamoja na wale wa *TRA* wasimamie na watekeleze haya yote yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa sababu hayo yaliyotokea sasa hivi, hayo makontena yaliyokuwa

yanadanganya hawalipi kodi, yanapitishwa tu, wana-*under declare; force declaration* yote ni kupoteza fedha za Taifa hili. Kwa hiyo, wasimamie na huu utaratibu waliouanzisha wa kupekua kila kontena sawa, uendelee lakini uandaliwe utaratibu mzuri ili makontena yasirundikane pale, tukarudi kule nyuma tulikokuwa, tuka-*loose competition,* wafanyabiashara wanapitisha bidhaa zao katika bandari za Mombasa na nyinginezo lakini wajitahidi hapa watafute utaratibu wa harakaharaka kufanya uchunguzi na makontena yaondoke ili tusi-*loose competition* uchumi wetu ukazidi kudidimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupata mapato kunategemea zaidi na kupanua wigo. Ni nyimbo yetu hapa, *TRA* lazima ipanue wigo wa mapato. Moja, ni kuzuia huu ukwepaji wa kodi. Ukizuia tu ukwepaji wa kodi, kodi zinaingia, ina maana umepanua wigo. Vilevile kutafuta vianzio vipya vya mapato, wengi wamepiga kelele. Kuna Kamati ya Mheshimiwa Chenge hapa, imefanya uchambuzi wa kina, kipengele kwa kipengele, sekta kwa sekta, ikaainisha maeneo gani ambayo tunaweza kupata mapato. Kwa hiyo, tunaomba Serikali, tunajua ni muda mfupi huwezi ukayachukua yote lazima na ninyi Serikali mfanyie uchambuzi, muone namna gani yatakusanywa yale mapato na kwa utaratibu gani, humuwezi kuvamia tu. Kwa hiyo, tunakupeni mwaka huu mfanye kazi hiyo ili bajeti ya mwakani muwe mmeshakuja na hivyo vianzio vipya ili mapato mengi zaidi yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo moja ambalo tunaweza kupata kodi ya mapato na nchi nyingine wanapata, ni hili eneo la sekta ambayo siyo rasmi. Tulielezwa hapa kuwa zikipatikana vitambulisho vile vya uraia, ikajulikana nani anaishi wapi, anafanya biashara gani, basi mapato yanaweza kuongezeka lakini sikuona katika bajeti hii umuhimu wowote uliowekwa katika kuendeleza utoaji wa hivi vitambulisho vya utaifa. Kwa hiyo, tunaomba sasa *NIDA* ipewe bajeti ifanye kazi hii ili kila Mtanzania aweze kupata hiki kitambulisho cha Utaifa kwa sababu ni njia moja ya kuweza kupatia mapato ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la utafiti. Hakuna nchi iliyoweza kuendelea katika ulimwengu huu bila utafiti na makubaliano ya nchi za *SADC* kila nchi ichangie asilimia moja ya *GDP* yake iende katika utafiti. Hatukuona! Tumeangalia takwimu zinasema mwaka 2012/ 2013 ambao ndiyo huu unamalizika ni asilimia 0.4 lakini mwaka ujao 2013/2014 ni asilimia 0.42, ile asilimia imezidi kudidimia. Hapa bado hatujaweka nia zaidi ya kuendeleza utafiti kwenye sayansi na teknolojia na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidhamu ya matumizi. Bajeti ikishapitishwa na Bunge, inakuwa ni sheria, kwa hiyo, unatakiwa uifuate kama vile ilivyopitishwa lakini sivyo ilivyo. Utaratibu mwingine kabisa watu wanautumia, unatoa fungu hapa unaupeleka hapa, unatumia unavyotaka, hakuna nidhamu. Kwa hiyo, ni lazima nidhamu ya matumizi iwepo. Kuna matumizi mengine ni lazima yawe *ring fenced* kwa mfano matumizi yanayokwenda kwenye umeme vijijini, yanayokwenda kwenye reli, yanatakiwa yasiguswe vinginevyo yale matarajio ya kiuchumi hayataweza kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekkiti, Maafisa Masuuli wamepewa dhamana, wanapewa *ceiling* na Wizara ya Fedha wajipangie lakini kwa bahati mbaya sana wanapanga katika vipengele ambavyo si muhimu kwa Wizara. Wataweka katika *other operating expenses*, sijui kwenye *hospitality* lakini ile *core function* ya ile Wizara, fedha zinakuwa kidogo kwenye kasma zile. Kuna mfano mmoja hapa, kuna Wizara moja ununuzi wa magazeti umewekewa fedha nyingi kuliko upimaji wa ardhi, hii ni nini? Haifahamiki Mheshimiwa Mwenyekiti!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira. Tuna tatizo la ajira katika nchi yetu. Kwa hiyo, Serikali isimamie uanzishwaji wa viwanda mbalimbali ili watu wetu wapate ajira na hasa zinazoweza kutumia malighafi zinazotokana na kilimo, uvuvi na mifugo ambazo zitaongeza ajira kwa watu wetu, umaskini utapungua, watakuwa watu wamefikiwa na wataona huo ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza, naomba kuongelea Chuo cha *Marine Science* kule Zanzibar. Tunaomba sana, hiki chuo ni muhimu sana. Kwa hiyo, nacho kipangiwe bajeti, kiongezewe fedha. Ushauri wa jumla, miradi yote ya maendeleo ambayo inapangiwa fedha, ipatiwe fedha zake za kutosha, mwaka huu ni asilimia 33 tu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kidawa Saleh kwa mchango wako mahiri kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Machali na Mheshimiwa Dkt. Chami ajiandae.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami nichangie bajeti kuu ya Serikali au ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachumi siku zote wanasema *no piece no production,* kama hakuna utulivu au amani basi uzalishaji hauwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kuzungumzia sana hali ya utulivu wa nchi yetu nikihusianisha na suala zima la uwezekano wa kuweza kujenga uchumi wetu. Hivi sasa ukweli usiopingika ukijaribu kuangalia, watu wengi wanakuwa na hofu ya kusema ngoja wajikite kwenye shughuli za uzalishaji kutokana na siasa chafu ambazo zimeanza kujitokeza kwenye nchi yetu. Jana nilizungumza jambo moja nikasema, baadhi ya wanasiasa ndani ya vyama

vyao, wanadiriki kutumia fursa walizonazo vibaya kwa maslahi ambayo wanayajua wao. Matokeo yake inakuja kuwatia hofu au inakuja kuwafanya watu wasijikite kwenye shughuli za uzalishaji kwa sababu ya siasa chafu ambazo zinaendelea ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba moja kwa moja tu nivitupie lawama vyama vya CCM na CHADEMA, ni lazima vijisahihishe. Haya yanayotokea Arusha, haya yanayotokea Iringa, baadhi ya watu wataendelea kuumizwa kwa sababu ya mivutano ya vyama hivi viwili. Watakalia kuwauguza ndugu zao ambao wameumia kwenye shughuli za kisiasa badala ya kwenda mashambani kulima, badala ya watu wengine waende kwenye biashara wakafanye biashara na Serikali ikaweza kukusanya kodi. Bado natoa wito kwa kumtaka na kumwomba Msajili wa Vyama vya Siasa aviangalie vyama hivi na tukio la Arusha liangaliwe kwa umakini ili kuweza ku-*harmonize* nchi yetu, chama kitakachobainika kama siyo kuwachukulia hatua watu ambao wamehusika basi vyama hivyo vifutwe mara moja kwa ustawi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuendelea kuangalia kwamba ni CCM ni CHADEMA, kila siku mivutano ni CCM ni CHADEMA, hii ni hali ya kihuni, haiwezekani tukawa tunafanya siasa za namna hii, haiwezekani! Tanzania siyo ya CCM na CHADEMA, narudia tena, Tanzania siyo ya CCM na CHADEMA. CCM wanasema wana wanachama milioni sita, CHADEMA labda watakuwa kwenye milioni tano au milioni nne, Tanzania ina watu zaidi ya milioni 44.9 leo hii tunapozungumza. Sasa watu ambao wanakuja kuiweka nchi yetu kwenye hali tete, Watanzania naomba tupime. Nasimamia kauli yangu, lazima Msajili wa Vyama vya Siasa aangalie vyama hivi. Tuanze pengine kuwazuia watu ku-*practice politics,* watu ambao wana-*practice* siasa chafu, umefukuzwa kwenye chama chako au unapigwa *stop*, nenda kakae kando, tusikuone tena unafanya siasa vinginevyo tutaipeleka nchi yetu kwenye machafuko ambayo hatukuyatarajia.

**TAARIFA**

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahaa, taarifa Mheshimiwa.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 28(7) pamoja na Kanuni ya 64(1)...

**MWENYEKITI:** Kanuni ya 28 ngapi?

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Kanuni ya 64(1)(a) kwamba Mbunge hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala. Mheshimiwa Mbunge aliyeketi hivi sasa mambo ambayo anayazungumza hayako katika mjadala huu unaoendelea hivi sasa. Kwa hivyo, naomba Mwongozo wako Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Kanuni ya 64 ngapi?

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Kanuni ya 64(1)(b, naomba tu kutoa taarifa kwamba anachozungumzia hakipo kwenye mjadala unaoendelea hivi sasa.

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Machali unaipokea?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme taarifa yake siipokei kwa sababu hajanisikiliza vizuri. Ni lazima ufanye *connection* kati ya utulivu pamoja na shughuli ambazo zinahusiana na uchumi. Huwezi ukaenda kuzalisha kama mahali hakuna utulivu, haiwezekani,

haiwezekani, watu wanapigana unawezaje kwenda kwenye *production area? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri namheshimu sana Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye kwa umri wake na naamini hili jambo analijua ila anataka kufanya siasa, *deemable politics* hazina nafasi kwangu na mimi ni *statesman.* Kwa hiyo, naomba taarifa yake tu akae nayo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuendelea na niombe ulinde muda wangu ambao ameutumia. *Message sent.*

**MWENYEKITI:** Muda wako umelindwa na baada ya kuanza kujibu taarifa muda wako unaendelea kuhesabika, endelea.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Baada ya kuzungumzia suala hilo la kuhakikisha kwamba utulivu unakuwepo ndani ya nchi yetu sasa naomba na mimi nijikite kwenye maeneo mengine. Moja, sikubaliani na pendekezo la Serikali la kutaka kuongeza tozo au kodi kwenye simu. Hili suala la kwenda kuwatoza watumiaji ambao tunawaita kwenye uchumi ni walaji asilimia 14.5 itakuwa ni uonevu. Hizi ni dalili za Serikali au mamlaka iliyopewa jukumu la kuweza kukusanya kodi kuwaogopa watu wenye makampuni ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia kwa kawaida, mimi sio mfanyabiashara, nina fedha zangu kwenye akaunti, leo hii tunatoa pesa kwenye akaunti kwa kutumia simu zetu, ninakutumia pesa wewe Mheshimiwa Mwenyekiti kwa ajili ya matumizi yako ya kawaida, nimefanya biashara gani? Nafanya biashara gani Mheshimiwa Waziri hadi uje unitoze asilimia 14.5? Mimi nachukua pesa yangu, namtumia yule pale na yule pale ni mlaji, anaenda kununua kama ni kalamu, kama ni daftari au chochote na akienda kununua kule tena analipa kodi, unanitoza mimi au unamtoza yule kwa misingi gani? Naomba suala hili mliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane pia na Mheshimiwa Serukamba, amezungumzia suala la asilimia kumi kwamba, nchi nyingine za *East Africa* wanatoza asilimia kumi; ni sababu gani ambazo zinawapeleka ninyi mwende kule kwenye asilimia 14.5 kama siyo kuja kumbebesha mzigo mkubwa mtumiaji wa simu hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo jambo kuna haja mkakae muweze kulifanyia mapitio mwangalie mnaliwekaje. Siungi mkono suala hilo, niseme tu kwamba, natangaza nia mapema ya kuja kutoa shilingi baadaye juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni pale kwenye kuongeza kodi kwenye petroli. Ni jambo la ajabu sana, kwa sababu unapoongeza kodi kwenye mafuta, utamwathiri mlaji moja kwa moja, bidhaa zitapanda bei. Sasa mnataka kwenda kumbebesha mzigo Mtanzania wa kawaida, ambaye ni mlaji, amepigika na maisha amechoka katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Naomba huo uamuzi muurejee upya na mwangalie, nina-*suggest* mrudi kwenye utaratibu wa zamani kwa sababu mnapopandisha kodi kwenye petroli mtasababisha kupanda kwa bei ya bidhaa mbalimbali kutoka *Point A* kwenda *Point B,* pamoja na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ambayo ningependa kujikita ni kwamba, Serikali bado haijawa *serious* kwenye kuziangalia *strategic areas* kwa ajili ya kuimarisha mapato ndani ya nchi yetu. Kwa mfano, tumeitelekeza bandari yetu, fedha ambazo Serikali imetenga kwenye bajeti kwa ajili ya kuboresha sekta ya bandari hapa nchini, bado haziwezi zikawa na matokeo makubwa kwa ajili ya kuimarisha uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuimarusha Sekta ya Reli hapa nchini, bado ni kidogo. Ni jambo la ajabu, naiomba Serikali, kama tunataka kuhakikisha kwamba, tunaufanya uchumi wetu unaimarika, uchumi wetu unapaa, ni lazima tukubali kuweka *pending* baadhi ya mambo tu-*suspend* tusifanye. Tufanye mambo

machache kwa wakati ili kuhakikisha kwamba, baada ya muda tunaweza tukawa na matokeo makubwa kwenye uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ziko sekta ambazo ni *very productive* kimkakati, kwa maana ukiweza kuimarisha sekta ya bandari pamoja na usafirishaji, kwa maana ya uchukuzi, reli ikaimarishwa, itakuwa ni rahisi kwa wafanyabiashara mbalimbali ambao wanaizunguka nchi yetu. Nchi kama za *DRC,* nchi kama za Burundi, nchi kama za Zambia, wataweza kupitisha mzigo kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam na wataweza kupeleka na Serikali itakusanya kodi ya kutosha kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia suala la kilimo, asilimia 80 ya Watanzania kati ya asilimia 75 na asilimia 80 ni wakulima wanaishi Vijijini na wanaendesha kilimo kwa kutumia jembe la mkono. Tunazungumzia KILIMO KWANZA; matrekta mnasema kwamba, mnawakopesha watu; ni Watanzania wangapi ambao wana uwezo wa kuweza kukopa hayo matrekta ambayo yanauzwa kuanzia milioni 16?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo mwalimu ambaye anapata mshahara wa chini ya shilingi 300,000 unamwambia aende akakope trekta; saa ngapi watamwamini kusudi waweze kumkopesha trekta na aende aka-*practise* kilimo huko kijijini? Inawezekana wapi na wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naishauri Serikali, kuweni na mkakati wa kutaka kuimarisha kilimo hapa nchini. Nunueni matrekta na muwapatie Wataalamu wa Kilimo huko kwenye Halmashauri zetu waende wakatambue watu. Wakabidhini matrekta hayo hapo, labda leteni pale Kasulu matrekta kumi mwaka huu hayo hapo tumewaleteeni, limeni na mtalipa baada ya kuvuna. Huu utaratibu na utamaduni wa sasa unaojengwa kwamba, watu waende wakakope SUMA JKT pamoja na maeneo mengine, ni usanii mtupu, naomba niitumie *term* hiyo. Haiwezekani, wangapi wataenda kukopa wakati hawana *collateral,* hawaaminiki

Watanzania kwa sababu hawana vitu ambavyo watavitumia kama dhamana ya kwenda kukopeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *focus* ingekuwa kwamba, tuangalie bandari, tuangalie Sekta ya Uchukuzi au Usafirishaji, tuone ni jinsi gani ambavyo tunaweza tukaimarisha maeneo hayo ikiwemo pamoja na kilimo. Nimestuka na bado nashangaa, mnataka kupunguza ile *skills development levy;* kama sikuelewa vibaya, kama mnapunguza mmetoa kutoka asilimia sita kwenda asilimia tano, hamna dhamira njema ya kuona kwamba, hivi Vyuo vya Ufundi kwa maana ya *Vocational Trainings* zinakua vizuri na zinakuwepo za kutosha kwa sababu hatuna vyuo vya kutosha. Kama dhamira yenu ni kutaka kupunguza ili wale watu wasiweze kupata fedha za kutosha na *VETA* nyingi tukaona zinajengwa, hamuwatakii heri hawa Watanzania, ambao wanajiunga na shule za sekondari, matokeo yake wengi wanamaliza hawana *qualifications* za kwenda Kidato cha V na cha VI, matokeo yake watakuwa mtaani, ni bomu lingine hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima mjaribu kuangalia. Mheshimiwa Waziri, usisote mkono hivi, kuwa na nidhamu. Naomba uwe na nidhamu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, hebu ongea na Kiti.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asinifanyie hivi Mheshimiwa Waziri Mbene. Namwomba na Mheshimiwa Naibu Waziri, awe na nidhamu, asinifanyie hivi, *no.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, hebu na wewe uwe na nidhamu ndani ya Bunge. Unapohutubia ndani ya Bunge, unaongea na Kiti. Kwa lolote linalotokea, utaelekeza michango yako na kila kitu kwenye Kiti na Kiti ndicho kitakachofanya maamuzi.

Anapochangia Mbunge humu ndani na yeye sasa

anaanza kuropoka vitu ambavyo havina msingi na tija katika mjadala na yeye ni Mbunge ambaye anakuwa hana nidhamu. Kwa tatizo lolote, Mbunge yeyote, kwa tatizo lolote ndani ya Bunge, aelekeze kwenye Kiti na kama kuna tatizo la kinidhamu, aelekeze kwenye Kiti na Kiti kitachukua hatua, lakini siyo kupotosha nidhamu na wewe unaanza kutokuwa na nidhamu kwa kuropoka vitu ambavyo havina tija kwenye mchango. Kwa hiyo, naomba umalizie dakika zako za mwisho, ujikite kwenye nidhamu na kama una hoja yoyote ya kutokutokea kwa nidhamu ndani ya Bunge, utaielekeza kwenye Kiti.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru japo hata Kiti kimetumia neno kuropoka, sijalipenda, naomba na Kiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, nimesema endelea na kama hutaki kuendelea, kaa chini nimwite Mbunge mwingine aendelee na mchango wake.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Basi sitaki kuendelea. Naomba na wewe uache kuropoka vilevile.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, kaa chini na ninamwita Mheshimiwa Mbunge mwingine, acha kuendelea na huo mchango wako, tutaendela na hoja nyingine. Usituvurugie shughuli za Bunge na shughuli za uchangiaji kwenye Bajeti hii. Kwa hiyo, sikupi tena nafasi ya kuendelea, namwita Mbunge mwingine anayefuata.

Nilisema nitamwita Dokta Chami, kwa hiyo, Mheshimiwa Machali, dakika zako hizi hutazipata tena na sitashughulikia hilo suala lako. Mheshimiwa Dokta Chami!

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha, kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kushauriana na Serikali katika bajeti mbalimbali za Wizara. Kama ambavyo wenzangu wamesema, kwa kweli Waziri huyu na wasaidizi wake ni

wasikivu; matumaini yetu ni kwamba, fedha ambayo tunapitisha hapa, basi itafika kwenye Mawizara na TAASISI mbalimbali ili kazi ifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naomba nisimame hapa kwa niaba ya Wananchi wa Moshi Vijijini, kumshukuru Gavana wa Benki Kuu, Profesa Benno Ndulu, ambaye kwanza, Sera zake za Uchumi na hasa katika uchumi wa mambo ya fedha ni imara sana. Tangu Gavana Ndulu achukue nafasi yake, mabenki ambayo yamewekeza Tanzania sasa hivi yameongezeka mara dufu kwa kipindi kifupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tunafahamu sote, mabenki haya siyo rafiki wa mlalahoi. Kwa sababu hiyo, Profesa Ndulu, amebuni utaratibu mwingine sasa wa kuhakikisha kwamba, wale wote ambao wana nia ya kufungua Benki za Maendeleo ya Wananchi, wanapata fursa hiyo. Nasi Wananchi wa Moshi Vijijini, tuliomba Benki Kuu, Wizara ya Fedha na ninafurahi kusema kwamba, Mheshimiwa Profesa Ndulu, baada ya kutuangalia kwa makini na kuangalia uwezo wetu, ametupa leseni sasa, kwa hiyo, Wananchi wa Moshi Vijijini watafungua nao Benki ya Maendeleo ya Moshi Vijijini, ambayo itakuwa ni Benki ya nne katika Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki hii itasaidia kuwafikia watu ambao wako katika *SACCOS,* kufikia Vikundi vya Wekeza, kuwafikia watu ambao wako katika vikundi vidogovidogo, ambao wasingeweza kufikiwa na mabenki makubwa, ambayo kama nilivyosema siyo rafiki wa mlalahoi. Kwa hiyo, namshukuru Profesa Ndulu, naishukuru Wizara ya Fedha, lakini natoa wito kwa wale wadau wa maendeleo Moshi Vijijini, tununue *share.* Tumepewa muda wa mwezi mmoja tununue zile *share,* tufikishe bilioni 2.5, benki ianze pale Moshi, tuwe na Benki ya nne ya Maendeleo katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, napenda

nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, Mheshimiwa Rais, akishatoa ahadi ya maendeleo katika Jimbo lolote na katika mradi wowote, moja kwa moja iingizwe kwenye Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Wabunge wanakuja hapa kulalamika kuhusu ahadi ambazo Mheshimiwa Rais ametoa. Mheshimiwa Rais, anaahidi Mradi wa Barabara, Wabunge inabidi waje hapa waulize siyo mara moja, mara mbili, mara tatu, inakuwa tena ni shida. Nataka niseme kwamba, nafikiri ahadi ya Mheshimiwa Rais ni kama amri; isiwe tena sasa Mbunge nakuja kuanza kusukuma ile ahadi kana kwamba ni ombi la Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na-*declare interest,* mimi natokana na Chama cha Mapinduzi, ningependa Mgombea wa Chama cha Mapinduzi 2015, anapoenda katika kujinadi asiulizwe kwamba, mbona mwenzako aliyekutangulia alitoa ahadi na hazikutekelezwa. Wabunge hapa, awe ni wa Chama Tawala au Chama cha Upinzani, ahadi inapotolewa katika Jimbo lake, Wananchi wanamtaka yeye asimame ahakikishe ile ahadi inatekelezwa. Kama ile ahadi haitekelezwi, yule Mbunge anapata wakati mgumu, bila kujali kwamba ni wa chama kipi. Rais ametoa ahadi, Mbunge kazi yake ni kufuatilia. Mimi nataka nimwombe Waziri wa Fedha atusaidie, hizi ahadi za Serikali ziingizwe. Kwa miaka hii miwili iliyobaki, tuhakikishe kwamba, zinakamilika ili tuache kulaumiwa katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wameongea sana kuhusu fursa mbalimbali ambazo zingeweza kuongeza mapato ya Taifa na mimi sitapenda kurudia. Nataka nitaje chanzo kimoja tu ambacho pengine kimesahaulika lakini kipo, nacho ni chanzo cha Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlima Kilimanjaro ni chanzo kizuri sana cha mapato ya Taifa, ambacho kikitumika vizuri kinaweza kuiongezea nchi hii mapato mengi sana.

Tulishaambiwa hapa kwamba, Mamlaka ya Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ya *KINAPA,* inachangia asilimia 38 mpaka asilimia 40 ya mapato yote ya *TANAPA. TANAPA* inazo Hifadhi za Taifa 13, lakini hiyo moja tu ya *KINAPA* inachangia karibu asilimia 40 na mchango wake unatokana na njia mbili tu; njia ya Machame na Njia ya Marangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe ushauri ufuatao kwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Maliasili na Utalii; mkitaka Mlima ule ulete watalii wengi zaidi, fungueni zile njia nyingine ambazo hazipitiki. Fungueni njia ya Umbwe, Geti la Umbwe pale lifunguliwe; namna ya kufungua, malizieni Barabara ya Kibosho ambayo Mheshimiwa Rais, ameahidi kwa miaka zaidi ya mitano iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Uru – Njari ni muhimu sana ambalo watalii wanapenda sana kupita, lakini barabara inakuwa mbovu. Namna ya kuifungua, malizieni ile barabara, bado kilometa tatu tu ili watalii waweze kufika Mlima Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Old Moshi, barabara ile ni mbovu kabisa, lakini ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, mpaka sasa hivi haijajengwa. Ikifunguliwa watalii watakwenda kwa wingi kabisa katika eneo lile; namna ya kumaliza kilometa kumi zile, wekeni fedha pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi wala hazifiki kilometa 50, lakini ukizijenga zile, ninahakika mapato ya Mlima Kilimanjaro yatazidi labda mara dufu au zaidi. Kwa hiyo, ni chanzo cha fedha ambacho kiko pale. Wenzetu Wakenya wanafahamu Kilimanjaro faida yake, sasa hivi wanajenga uwanja wa ndege karibu na Holili, ili watalii washuke moja kwa moja pale waje wapande upande wa Kenya, waangalie Mlima Kilimanjaro, waingize mapato pale na sisi tuwekeze kidogo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo Mlima Kilimanjaro unaweza ukaiingizia nchi hii mapato ni kwamba, watalii wanaopanda mlima ni wale vijana wenye nguvu,

ambao wanaweza wakapanda katika ile miinuko. Wapo pia watalii wenye fedha nyingi, ambao wengine ni wastaafu, wangependa kupanda Kilimanjaro, lakini hawana nguvu za mwili za kuweza kupanda pale, lakini ndiyo wenye fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinaitwa utalii kwa kutumia lifti kwa kuweka reli. Pale Afrika Kusini kuna *Table Mountain,* ambapo kwa wale watalii ambao hawawezi kupanda kwa miguu wameweka reli ambayo inaweza kuwapandisha wakafika mpaka kileleni wakaweza kuona mandhari yote wakarudi na wanalipa fedha nyingi sana. Nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Maliasili na Utalii, waangalie *option* hiyo ya kuweza kuwekeza na wasingojee tu mtu kutoka nje aje awekeze, isipokuwa wao waje wafanye vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la Kilimanjaro ni *Golf Tourism*. Mkuu wa Mkoa ameshaanza mawazo hayo. Mimi naomba Wizara ya Fedha na Wizara ya Maliasili na Utalii, wasaidiane na Uongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa ajili ya kutengeneza *Golf Tourism* katika eneo la Siha, ambapo eneo limepatikana ekari zaidi ya 2,000, ambalo litasaidia kuwafanya watalii waje kucheza *golf,* wakitoka kwenye *golf* wanapanda mlima, wakitoka kwenye mlima wanakwenda Serengeti, Manyara na maeneo mengine; tutapata fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye kilio cha Wakulima wa Kahawa wa *KNCU,* Kilimanjaro. Miaka michache iliyopita kulikuwa na mdororo wa uchumi na Serikali yetu ikatoa shilingi trilioni 1.7 kwa ajili ya kuyaokoa makampuni na wale watu binafsi ambao walipata hasara kutokana na ule mdororo. Chama cha Kahawa cha *KNCU,* kilikuwa kinadai shilingi 1,230,000,000; wameomba zile fedha, yametokea mambo yaliyotokea, wamelipwa kidogo sana, sasa hivi wanadai milioni 855. Majibu tunayoyapata Wizara ya Fedha ni ya kuzungusha. Nataka niombe kwa niaba ya Wananchi Wakulima wa Kahawa Mkoa wa Kilimanjaro kwamba, Mheshimiwa Waziri

wa Fedha, hebu saidia kuwapa Wakulima wa Kilimanjaro hizo fedha, ili wakazalishe kahawa nyingi zaidi, tuongeze mapato mengi ya fedha za kigeni na bajeti ya nchi yetu iweze kukua zaidi, mwaka kesho ukija hapa na mwaka keshokutwa ukija hapa, uongelee trilioni 30 badala ya trilioni hizi 18 ambazo tunaziongelea sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea suala la *TRA.* Kwanza, niungane na wenzangu kumpongeza Kamishna wa *TRA* na Timu yake, kwa jinsi ambavyo wanaboresha mapato ya Serikali, lakini kuna eneo moja ambalo limekuwa kero kubwa kwa watu ambao wanaingiza mizigo hasa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye mtandao, unaweza ukanunua gari kwa mtandao, *www.tradecarview.com.* Unaweza uka-*negotiate* kabisa na yule mwuzaji ukalipia na gharama, gari likafika bandarini. Linafika pale, kwenye ile *Bill of Lading,* unapata pale labda dola 10,000, lakini mtu wa *TRA* anakataa anasema siyo 10,000 anasema ni 15,000 au 20,000. Sasa hiki kitu umenunua kwa njia halali, ume-*negotiate,* wewe ni mtu ambaye unapata mshahara wako, ni mtu wa kima cha kati au kima cha chini, umejitahidi hata umeenda kukopa; unatafuta dola zako 10,000, gari linafika bandarini, mtu wa *TRA* anakataa anasema siyo 10,000 na wakati *documents* zote zinaonesha ni dola 10,000, analazimisha ni 15,000 anakuwekea kodi ya dola 15,000!

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni kwamba, kama *round* hii nimeleta magari nyangu nikaongezewa, *round* ijayo na mimi nitafanya ujanja wa kuongea na mtu wa *TRA,* ili kumhonga kidogo halafu nipunguziwe. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba, inakuwa ni *zero sum game.* Inakuwa ni mchezo ambao hauna matokeo; kwamba, wale wajanja wanafanya mpango kwa sababu tumeshampa yule mtu wa *TRA* uwezo wa kuongeza ama kupunguza thamani ya mzigo unaokuja, basi ndiyo unatoa fursa ya rushwa. Anaongea na wale wafanyabiashara na wengine wamesema wafanyabiashara wakubwa, lakini nasema

hata mfanyabiashara mdogo tu na yeye anaweza akafanya hilo, matokeo yake nchi yetu inakosa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uaminifu unakosekana; kama mtu ameagiza gari lake, amelipa kiasi ambacho ni halali, unapokuja kusema ni zaidi unaumiza watu. Naomba *TRA* katika hilo, iache kuonea watu. Kazi ni nzuri ya kukusanya mapato, lakini uonevu kwa watu siyo mzuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni ya kwanza ya pili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ni kengele ya pili.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Bajeti ya Wizara ya Fedha. Kwanza, nashukuru na kuipongeza Serikali na Wizara ya Fedha kwa ujumla, kwa kuweza kupokea mapendekezo ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge kwenye Wizara tulipokuwa tumechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Nimefarijika kwa kiasi kikubwa, kuona Wizara hii imeongezewa kiasi cha bilioni mbili, lakini jambo ambalo linanisikitisha ni kwamba, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ilianzishwa Kisheria mwaka 1993 na Mfuko huu ulikuwa una Namba yake ambayo ilikuwa inapewa fedha kutoka Hazina. Kuanzia mwaka 2005/2006 Namba hiyo ilipewa Benki ya Wanawake na kuanzia hapo Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, haukuweza kutengewa tena fedha kutoka Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Waziri wa

Fedha, atambue kwamba, Benki ya Wanawake, inahudumia zaidi wanawake walioko mijini na siyo wa vijijini. Kuondoa fungu hili kulipeleka Benki ya Wanawake ni kuwanyima haki wanawake wengi walioko Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana na namsihi sana Waziri wa Fedha na Manaibu wake ambao ni akina mama, wawaone wanawake walioko vijijini na waweze kuliangalia Fungu hili, walirudishe na kwa kiasi kikubwa waweze kufidia fedha zote ambazo hawakuweza kuzipeleka kuanzia 2005 mpaka hapa tulipofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa kiasi kikubwa unasaidia sana akina mama na akina mama hawa wanakuwa waaminifu sana. Tatizo lililopo, kuna mchangiaji mmoja jana alisema kwamba, unakuta labda ni mtu binafsi anakuwa amejiandikisha kwamba ni kikundi. Mimi niwaombe na niwasihi Maafisa Maendeleo ya Jamii, wavikague vikundi hivi, siyo wote wanaofanya hivyo. Nawaomba sana Maafisa Maendeleo ya Jamii wakague vikundi hivi ili tuweze kufikia pale ambapo tunatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia Wizara kwa kuweza kuongeza fedha kwenye Wizara ya Maji. Tatizo kubwa tulilonalo ni maji, kila unapokwenda ni maji, akina mama hawakai majumbani kwa sababu ya maji na kwa namna hii nafarijika sasa kusema kwamba, hata matatizo ya maji yaliyoko Mkoa wa Shinyanga ambako tunasema tuna maji ya Ziwa Victoria wakati siyo kweli kwamba Wananchi wote wa Mkoa wa Shinyanga wanapata maji ya Ziwa Victoria, siyo kweli kwamba, Wananchi wa Mwanza wanapata maji ya Ziwa Victoria, siyo kweli kwamba Wananchi wa Mara na wa Bukoba wanapata maji ya Ziwa Victoria wakati wamezungukwa na Ziwa siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ongezeko hili, naomba sana, Mheshimiwa Rais wakati anafungua Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria pale Ihelele alisema, vijiji vyote vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka bomba kuu lazima vipate haya

maji, lakini mpaka hivi tunavyoongea vijiji hivyo havijapata haya maji. Nina imani kwa ongezeko kubwa la fedha hizi, vijiji vyote hivi vitapata maji. Nawaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, Waziri wa Fedha, hebu utazameni Mkoa wa Shinyanga kwa jicho la huruma, kwa sababu hayo maji tunayosema yako Mkoa wa Shinyanga siyo maeneo yote yaliyopata haya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo makubwa ya maji, matokeo yake ni uharibifu ambao unaweza ukafanyika kwenye bomba hili, kwa sababu watu hawawezi kukubali kuona bomba linapita pale halafu wao wana tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ongezeko hili, nina imani kabisa Waziri wa Maji anatambua tatizo kubwa la maji lililopo Mji Mdogo wa Tinde. Nakuomba sana kwa ongezeko hili uutazame Mji Mdogo wa Tinde kwa huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ongezeko hili la fedha lililopo, niende kwenye kilimo, bilioni 21 zilizoongezwa kwenye kilimo, sijaona Mkoa wa Shinyanga na Kanda ya Ziwa mmetutazama kwa namna gani. Kila siku tunasimama humu ndani tunalia njaa mnasema hatulimi, tunalima lakini tatizo hatuna mvua za kutosha. Ukiangalia fedha hizi zote hazijaletwa Shinyanga hata kidogo, tumewakosea nini Mkoa wa Shinyanga? Ninaomba sana ili tuache kusimama humu ndani na kuomba chakula cha njaa mtuchimbie mabwawa ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kusema, Serikali iliahidi Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Jimbo la Solwa, Kijiji cha Masengwa, itachimba bwawa la umwagiliaji toka mwaka 2007 mpaka hivi ninavyoongea halijawahi kuchimbwa. Sasa kwa ongezeko hili la fedha, nawaomba sana Waziri wa Fedha na Waziri wa Kilimo, hebu ahadi hiyo itekelezwe. Haiwezekani ahadi toka mwaka 2007 mpaka hivi tunavyoongea haijawahi kutekelezwa. Hivi unasimama unawaambia nini Wananchi wale; tutasimama mpaka lini kuomba chakula hiki? Hebu tutekelezeeni haya

ambayo tunayahitaji ili hata kama mnatushutumu kwamba hatulimi, tuone kweli mnatushutumu kwa vitu ambavyo ni sahihi. Hakuna mtu anayelima kama Msukuma; hayupo katika nchi hii. Sasa ninashangaa tunapowaomba mahitaji yetu hamtutimizii, kwa ongezeko hili la kilimo naomba mtutazame Mkoa wa Shinyanga na hususan Bwawa la Masengwa ambalo ni ahadi ya Serikali toka mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye mifugo, mifugo imeongezewa fedha nyingi. Kila siku humu ndani tunatukanwa Wasukuma kwa kuhama na mifugo yetu, hatukupenda; tuwekeeni miundombinu mizuri ambayo haitatufanya tuhamishe mifugo ile. Kwa ongezeko hili, naiomba Serikali ili mwache kusimama humu ndani na kutuambia tuache kuhama kwenda Morogoro kwenda wapi, tuchimbieni mabwawa kwa ajili ya mifugo yetu. Tujengeeni majosho kwa ajili ya mifugo yetu, hamtatuona tunatangatanga katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niende kwenye viwanda. Serikali hii hii iliahidi Mkoa wa Shinyanga itajenga kiwanda cha saruji. Inanishangaza sana na inanisikitisha sana, Kanda ya Ziwa yote tunatoa simenti Tanga, Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani. Hivi sisi tuna matatizo gani; tumekosea nini; hii ahadi iliyotolewa kujenga kiwanda cha simenti Manispaa ya Shinyanga itatimizwa lini? Madini ya chokaa yalionekana yapo pale Old Shinyanga, yako pale Kizumbi na Serikali ikaahidi kujenga kiwanda cha simenti pale Shinyanga Manispaa, ahadi hii itatekelezwa lini tuepukane na kununua mfuko wa simenti 17,000 au 18,000? Kwa sababu gharama za usafiri ni kubwa hebu tuoneeni huruma, hicho kiwanda cha simenti kijengwe pale Manispaa ya Shinyanga, hii ni ahadi ya Serikali, hebu naomba hizo ahadi zilizoahidiwa basi mzitekeleze ili tuache na sisi kulalamika hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kiwanda cha simenti Mkoa wa Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga, kijengwe kwa sababu ni ahadi ya Serikali na ni tatizo kubwa

kwa Kanda ya Ziwa, kwa sababu hatuna kiwanda cha simenti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi Wizara ya Fedha. Naomba Waziri utakapoinuka unijibu; hivi Halmashauri inapoomba ombi maalum mnatumia vigezo gani kuwapa? Nakumbuka Mheshimiwa Rais alipokuja kuzindua Mradi wa Maji tulitoa matatizo yetu na yeye alituambia kwamba, anaomba tuandike ombi maalum kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Tumeshaandika ombi hilo mpaka tumechoka, hata kama mnafoleni kubwa kiasi gani, hebu angalieni hayo matatizo tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga inahudumia Wilaya tatu ambazo hazina Hospitali ya Wilaya. Sasa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kwa maana ya Jimbo la Solwa, tumeanza kwa nguvu zetu ujenzi huo, ujenzi wa Hospitali ile una gharama kubwa ambapo kwa hali ya kawaida Halmashauri haiwezi kumaliza. Tulishaomba ombi maalum, kila mwaka tunaomba ombi maalum, hamtutekelezei mnategemea tufanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anijibu kupewa ombi maalum mpaka uwe na vigezo gani; ni kwa nini Halmashauri ya Shinyanga hamtupi ombi maalum ambalo tunaomba kila mwaka kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya? Akina mama wanahangaika, wajawazito na watoto wanahangaika mpaka waende Hospitali ya Mkoa, ukifika Hospitali ya Mkoa msongamano wa wagonjwa ni mkubwa, Hospitali yenyewe haikidhi kupokea wagonjwa wote hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ituangalie kwa jicho la huruma. Nimalizie kwa kusema kwamba, naiomba sana Wizara ya Fedha kwa maana ya Hazina, muwaangalie watumishi; watumishi wanalalamika sana, walimu wanalalamika, Watumishi wa Idara ya Afya wanalalamika, hakuna mtumishi ambaye halalamiki. Unakuta mtumishi ana madai yake ya mshahara labda miezi

mitatu, miezi sita, hajalipwa ukiuliza unaambiwa Hazina. Kule kwangu kuna walimu wanadai mishahara miezi mitatu hawajalipwa; mtawalipa lini mishahara yao na tatizo kubwa hasa ni nini? Kama mshahara wa mwezi huu anaweza kupokea lakini nyuma anadai mishahara ya miezi mitatu, miezi minne; kuna tatizo gani huko Hazina?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Waziri awaangalie watumishi hawa, kwa sababu mtumishi kukaa pasipokuwa na mshahara wake wa miezi mitatu, miezi minne, tunamnyima haki yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, nirudie kusema naunga mkono hoja. Kwa yale niliyoyasema, naomba Waziri anijibu kwamba mna kigezo gani cha kupewa ombi maalum?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi na Chama cha Mapinduzi, kwa kunituma Mtwara kwenda kukomboa Kata iliyokuwa kwa Wapinzani, Kata ya Mnima ambayo sasa ipo chini ya CCM; ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia, kwa sababu nina imani na Mawaziri wote watatu; Waziri mwenyewe na Manaibu wake Mawaziri, pamoja na Watumishi katika Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopenda kuomba katika Wizara hii ya Fedha, fedha zinazopangwa katika Wizara mbalimbali hasa katika Wizara inayohusika na barabara ziwe zinatolewa kwa wakati unaotakikana. Hivi sasa Tabora makandarasi wale waliokuwa wanatengeneza barabara, baada ya kulipwa wameanza kufanya kazi kwa juhudi kubwa. Ninafurahi kusema kwamba, ndani ya saa

72 kutokea leo, Barabara ya kutoka Tabora kwenda Urambo kwa kupitia Ndono, wataanza kuweka lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni dhahiri kabisa kwamba, Hazina wakiwa wanatoa pesa kwa wakati unaotakikana, basi shughuli za maendeleo katika mikoa mingine ambayo ilikuwa imesahaulika itakwenda vizuri. Siyo hivyo tu, hata katika Barabara ya kutoka Tabora kwenda Nzega ambayo imebakia madaraja saba tu kati ya madaraja 82 ambayo yalikuwa yanajengwa, nimehakikishiwa na *engineers* kwamba ndani ya wiki tatu kutokea leo wataanza kuweka lami. Kwa hiyo, nina hakika kabisa kwamba, Wizara itaendelea kutoa pesa kwa wakati unaotakikana na Mkoa wa Tabora utakuwa umefunguka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Samahani, Mheshimiwa Rage. Waheshimiwa Wabunge, ambao mko karibu na Mheshimiwa Rage, nadhani hiyo *mike* ina matatizo, kwa hiyo, mnachoongea ndicho kinachosikika kwenye *mike* ya Mheshimiwa Rage. Kwa hiyo, ningeomba sana labda mpunguze kidogo maongezi kusudi Mheshimiwa Rage amalize kwanza. Mheshimiwa Rage endelea!

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Tabora tuna Mamlaka ya Maji, naweza nikadiriki kusema kwamba, Mamlaka yale ya *TUWASA* wanafanya kazi nzuri pengine kuliko Mamlaka nyingi katika nchi yetu, isipokuwa wanavunjwa moyo au wanavunjwa nguvu na Serikali. Nasema hivyo kwa sababu *TUWASA* wanadai Wizara ya Ulinzi na Polisi peke yake shilingi milioni 646. Hizi ni pesa nyingi sana kwa mji mdogo kama wa Tabora. Mkiweza kutupatia, tutaweza kuhakikisha tunatoa maji kwa Wananchi wa Tabora bila wasiwasi. Wakati nachaguliwa mwaka 2010 *TUWASA* walikuwa wanatoa maji lita milioni saba kwa siku, sasa hivi baada ya kupata *Management* mpya, wanatoa maji karibu lita milioni 14.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni dhahiri kabisa kwamba, wakipewa pesa zao, wataweza kufanya kazi

vizuri na Wananchi wa Tabora watafaidika sana. Nipeleke malalamiko yangu mengine kwa Wizara hii ya Fedha, ambayo mwaka jana ilitenga fedha kwa ajili ya Mradi wa Bwawa la Inara. Kwa masikitiko makubwa kabisa, fedha ambazo zilikuwa zimetengwa hazikutumika kwa ajili ya Bwawa la Inara, badala yake zikahamishwa kupelekwa Mkoa mwingine, kwa sababu anatoka Waziri huo Mkoa mwingine; jambo hili kwa kweli mimi limeniuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu umekaa sasa haufanyi shughuli yoyote, Wananchi wa Inara wanashindwa kufanya kilimo chao wakati wa kiangazi na lile bwawa lilikuwa ni kubwa mno, ambapo tulikuwa tunategemea kupata mpunga ambao ungeweza kusaidia kupunguza bei ya mpunga hapa nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba fedha zinapopangwa au zinapopitishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Miradi yake, isiwe inahamishwa kwa sababu tu kuna Waziri mwingine kutoka mahali pengine anataka na yeye asaidiwe jimbo lake, halafu sisi wanyonge ambao katika jimbo langu mimi hakuna Waziri, basi fedha zangu zinatolewa tu. Jambo hili limenikera na nimesikitika mpaka nimelalamika kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu suala hili, naomba lisirudiwe tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilikuwa nasoma Ripoti ya Benki ya Dunia iliyotayarishwa na yule Bwana Moriset. Anasema, Bandari ya Dar es Salaam tunapoteza bilioni 1.8 *dollars* kwa sababu ya uzembe, rushwa na kutokufanya kazi inavyotakikana. Kwa hiyo, tutakuwa tunawaonea watu wa Hazina kwamba hawatafuti fedha, lakini na sisi wenyewe Watanzania tunatakiwa tubadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale katika Bandari ya Dar es Salaam kwa mujibu wa Ripoti hii ya Benki ya Dunia, meli inakaa siku kumi kabla haijaingia kwenye gati na ikiingia kwenye gati inakaa tena siku kumi, *twenty days;* huu wakati ni wakati wa biashara ya mashindano. Nchi jirani Mombasa meli kutoka nje na kuingia kwenye gati ni kati ya siku tatu

mpaka nne. Kwa hiyo, unapoweka meli nje kwa zaidi ya siku 20, unaongeza gharama ya *almost 22 percent* kwenye kontena na asilimia tano kwenye *loose cargo*. Sasa gharama hii unampa nani?

Kwa hiyo, nina hakika kabisa kama tutafanya *efficiency* au kuboresha katika Bandari ya Mtwara na lazima nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, kwa kazi nzuri ambayo ameanza, ipo haja Wabunge na Wananchi tumuunge mkono na mimi nampongeza kabisa.

Mheshimiwa Mwenyeketi, kuna methali moja, mchezaji mmoja wa mpira wa zamani kule Uingereza alikuwa anaitwa George Best, alikuwa anasema hivi kwa Kiingereza naomba ninukuu: *"The smarter you appear on the ground, is the smarter how you are going to perform on the ground."* Kwa hiyo, Waziri huyu anaonekana kwamba anafanya kazi yake vizuri, atatusaidia vizuri sana katika kuhakikisha Bandari ile inapata pesa za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapopanua bandari au unapoifanya bandari ifanye kazi kwa ufanisi zaidi, *partner* wake au pacha wake ni reli, lakini reli imekuwa inasahaulika kila wakati. Kwa hiyo, ipo haja Serikali iangalie. Mwaka jana nilitoa shilingi, Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi ikalala, ikaongezwa shilingi bilioni 60 kwa ajili ya kukarabati karakana za Tabora, lakini kwa masikitiko mpaka hivi leo karakana zile bado hazijakarabatiwa japokuwa Bunge lilipitisha fedha hapa na hela ziliongezwa. Karakana ya Tabora ina uwezo wa kufanya *service* ya kichwa kimoja cha treni ndani ya saa tatu mpaka nane na kile kichwa kikaondoka kikaendelea. Kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba, karakana zile zinaboreshwa kwa sababu reli ya kwenda Kigoma inaanzia Tabora, reli ya kwenda Mwanza inaanzia Tabora, reli ya kwenda Mpanda inaanzia Tabora na reli ya kutoka Dar es Salaam kwenda Tabora inaanzia Tabora palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini

mnang'ang'ania kuwekeza kila kitu Morogoro tu? Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alikuwepo, nilimtembeza kwenye zile karakana akashtuka kuona hata kwenye bohari hakuna *spare parts.* Mheshimiwa Naibu Waziri nilipomwuliza swali katika kikao kilichopita, aliagiza kwamba, zile *spare parts* zipelekwe ili hizo karakana zifanye kazi; mpaka jana hakuna *spare* hata chache zilizopelekwa Tabora! Leo hii pamoja na uzee wangu huu niliokuwa nao, treni ya kwenda Mpanda ikiwa inaondoka pale Tabora kwenda Mpanda, tukikimbizana mimi nakimbia mbio zaidi kuliko treni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, nina imani kwamba Wizara ya Fedha sasa itakuwa makini kuhakikisha fedha zinakwenda kwa wakati unaotakikana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Aden Rage, nakushukuru sana kwa mchango wako na hasa kwa kuwa na uwezo wa kukimbia kuliko treni pamoja na umri wako kuwa mkubwa.

Waheshimiwa Wabunge, nilisema nitamwita mchangiaji anayefuatia ni Mheshimiwa Njwayo na nadhani dakika zitatutosha, Mheshimiwa Rweikiza atakuwa mchangiaji wa mwisho kwa asubuhi.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi mchana huu ili niungane na Wabunge wenzangu, kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza, naomba kusema naunga mkono hoja, kwa sababu yako mambo kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, yanayoashiria nchi yetu kusonga mbele. La kwanza, ni lile la kupunguza mfumko wa bei. La pili, kuna dalili ya kwamba ajira zitaongezeka nchini, lakini pia zipo jitihada zinazofanyika za kuongeza Pato la Taifa mpaka kufikia angalau asilimia 7.2 kwenye mwaka huu wa fedha. Vilevile kuimarika kwa Deni la Taifa Mambo haya yananishawishi kwa namna moja au nyingine, kuunga mkono hoja ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kwa Serikali ufuatao: La kwanza, Serikali ya CCM itaangushwa na Wizara ya Fedha, kama Serikali ya CCM itaondoka madarakani, mchango mkubwa utakuwa umetokana na Wizara hii ya Fedha. Kwa nini? Ndugu zangu Watanzania, wataalam wengi wa kawaida tulionao kule vijijini ni walimu, lakini walimu hawa wanadharauliwa na Wizara ya Fedha kwa kiasi kikubwa na wakikasirika watatu-*cost*. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri, usimame imara uwaangalie watendaji wako, wanakuangusha kwa kiasi kikubwa. Ninayo mifano, kule kwangu Tandahimba, nina walimu 150 wameingiziwa fedha na Kampuni ya *Bay Port* bila ya wao kuingia mkataba. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tandahimba anashangaa na amewaandikia mara tatu Wizara ya Fedha, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa na Kitengo cha Mishahara wala watu wale walioko kwenye mitandao ile. (*Makofi*)

Sasa hawa ndiyo wataalam wetu kule, hivi wakisimama imara leo kwamba tuachane na CCM hatutoki? Matatizo haya yako maeneo mengi; kwa sababu mara ya kwanza jambo hili lilipofika pale, Mkurugenzi alipopeleka pale barua, wakapunguza kutoka walimu 150 ikawa 87. Mbunge nikalichukua, nimekwenda pale, nimekutana na maafisa pale, wale maafisa walisema tatizo hili liko pia kwenye Wilaya ya Njombe; mnaona hiyo! Mpaka leo hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na naambiwa pia hata maeneo ya Moshi kuna kampuni inaitwa *Platinum,* nayo inawakopesha walimu bila kuwa na mdhamini! Wafanyakazi hawa wako kwenye Halmashauri ya Wilaya; inashindikanaje kudhaminiwa na Mkurugenzi? Wanaingizwaje kwenye mikopo, wanaingizwaje kwenye matatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mfano mwingine wa pili, yuko mwalimu mmoja, mpiga kura wangu, alikuwa anafundisha *DUCE* baadaye akateuliwa kuwa Afisa Elimu Taaluma Wilaya ya Mkuranga. Kwenye utaratibu ule wa kuhamisha mishahara, miezi miwili alikosa mshahara wake, halikuwa kosa lake lilikuwa kosa kati ya Kitengo cha Uhasibu

cha *DUCE* na Wizara ya Fedha, lakini tangu akose mshahara wake wa Desemba, 2012 na Januari, 2013, mpaka leo Hazina inaandika tu barua thibitisha. *DUCE* wanathibitisha kwamba, tulirudisha Hazina mshahara huu na wameonesha risiti, Mkurugenzi naye anaonesha ushahidi kwamba hakupata mshahara huyu mwalimu, rekebisheni, lakini mpaka leo hakuna kinachofanyika. Hivi unataka uthibitisho gani na mwalimu huyu ni Afisa Elimu Taaluma, ana nafasi kubwa ya kuwashawishi walimu wengine; ndiyo maana nasema itatugharimu na walimu hawa. *(Makofi)*

Hata madeni haya wanayodai, wakati mwingine Wizara hii ya Fedha haiwaambii tu walimu tatizo liko wapi ili warekebishe, maana wanaleta madai yao pale, kama kuna makosa inafanywa *pre-audit* pale, zile hoja zilizogunduliwa pale, hazifanyiwi kazi, wakaambiwa kwamba kuna tatizo hili ili mwalimu aone kweli alikosea au makosa yanayoweza kufanyiwa marekebisho yakamaliza tatizo. Tunaendelea kuwanyanyasa watumishi hawa kwa nini? Mheshimiwa Waziri, changamoto hii nimekupa, hebu fanyia kazi tumalize haya matatizo ya walimu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kwanza, naipongeza Serikali na Waziri wa Fedha, kwa kuleta mpango wa ushuru wa kwenye simu, ambao utapelekea kila matumizi ya huduma ya simu tutakatwa kama asilimia 14.5, lakini kuna asilimia 2.5 ambayo itakwenda kutatua matatizo ya elimu. Mimi naomba kutoa rai hapa kwamba, kutokana na hii basi katika matatizo yale tuondoe ada ya 20,000 kwa wanafunzi wa sekondari. *(Makofi)*

Kwa nini nasema hivyo? Jamani 20,000 hii inaonekana ni ndogo, lakini kwa Wananchi wa kawaida ni kubwa. Mwananchi ambaye anabebeshwa michango ya madawati, michango mbalimbali, kwanza, ujenzi wenyewe wa hizo shule, wanafanya wao! Maana wanachangishwa mno mno, sasa tuwaondolee hii ada ya 20,000 na zile shule za bweni 75,000 wanaolipa kule ili angalau wajisikie tumewa-

*comfort* kwa kiasi fulani, maana chanzo hiki sasa kinaweza kusaidia sana kupunguza adha ya Wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ligine ninaloliona na ningependa kuchangia ni kwamba, mara nyingi tumekuwa tunaleta bajeti nzuri, lakini wakati wa utekelezaji fedha haziendi kunakotakiwa. Kwa mfano, mwaka jana tulikubaliana hapa kuondoa ushuru mbalimbali ili tu-*balance* kwenye mafuta na tusaidie kuimarisha suala la umeme vijijini kwa kuipa *REA.* Kila mtu anajua zile fedha wala hazikwenda za kutosha na tulizozipitisha hapa *REA*, mwaka huu tena tumeongeza *billions* za fedha, nina wasiwasi sana yasije yakajirudia yale yaliyofanyika huko nyuma.

Safari hii tuanze upya, tuhakikishe fedha zinazopaswa kupelekwa *REA* zipelekwe ili maeneo ya wapiga kura wetu yasiyokuwa na umeme yaweze kupata umeme wa uhakika kule vijijini na umeme huu uchangie maendeleo ya nchi yetu sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuungana na Kamati ya Bajeti, mchango wao umeelezea hapa tatizo lililopo la ukusanyaji wa mapato wa Halmashauri au Serikali za Mitaa kwamba, katika mwaka uliopita, iliweza kukusanya asilimia 49 tu ya bajeti. Tatizo hili jamani lipo na kubwa. Mimi nataka kuungana na Kamati ya Bajeti kwamba, tafadhali tuwatumie Watendaji wetu wa Vijiji na wa Kata, tuwape motisha watafanya vizuri, makandarasi hawa tunaowapa hawaendi pale kwa nia nzuri, wanakwenda kujiimarisha wao.

Ninao mfano wa Halmashauri ambayo sitaitaja hapa, ambayo kila mwezi ilikuwa inakusanya milioni kumi tu, lakini walipoamua kugangamala wenyewe, wamekusanya milioni 100 kwa mwezi, yaani mara kumi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tukitengeneza mazingira mazuri ya Watendaji wetu wa Vijiji na wa Kata, watafanya vizuri na

mapato yataongezeka. Naomba kuchukua nafasi hiyo hiyo, kulisemea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njwayo, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana kwa kutii Kiti na kujali muda.

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri dakika zetu zinamtosha Mheshimiwa Rweikiza, una dakika kumi kabisa zinatimia.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwisho kwa siku ya leo, nami nichangie katika Bajeti hii ya Serikali.

**MWENYEKITI**: Nafasi ya mwisho kwa asubuhi.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Kwa asubuhi hii. Nachukua nafasi hii kukushukuru na kuipongeza Serikali kwa bajeti nzuri iliyoileta hasa kwa kuzingatia kilio cha Wabunge, sisi tumelia sana humu kuhusu mambo mbalimbali, Serikali sikivu imesikia kilio cha Wabunge kuhusu mambo ya *REA*, Elimu, Barabara na mambo mengine; nawapongeza sana, lakini nina mawili, niseme kwamba, kwa vile Serikali ni sikivu na haya iyasikie. Kwanza, kuongeza kodi kwenye magari makuukuu. Ukisoma ukurasa wa 69 na 70 wa Kitabu cha Bajeti, kuna ongezeko la kodi katika magari yenye zaidi ya miaka kumi. Sasa hili ni tatizo, huku siyo kujenga ni kuua uchumi. (*Makofi*)

Maana yake ni kwamba, Watanzania wangapi ambao wanaweza kununua magari mapya au ambayo

yana umri chini ya miaka kumi; siyo wengi, walio wengi uwezo wao ni kununua magari makuukuu. Ukiwaongezea kodi ina maana wasinunue magari. Magari siyo anasa tena kama ilivyokuwa zamani, gari ni kitendea kazi; unakwenda sehemu mbalimbali, unafanya kazi mbalimbali, unabeba mizigo, unabeba abiria, ni kitendea kazi, ni shughuli ya kuboresha uchumi. Kwa hiyo na hili mliangalie upya, msiongeze kodi kwenye magari makuukuu, Watanzania wengi uwezo wao ni kununua magari makuukuu. *(Makofi)*

La pili ambalo ni kubwa zaidi, matatizo ya wakulima. Nizungumzie matatizo ya Wakulima wa Kahawa wa Bukoba. Bukoba wanalima Kahawa na mazao mengine, lakini zao kubwa la biashara ni kahawa. Sasa taarifa zilizopo za kuaminika ni kwamba, katika kilogramu moja ya kahawa anayoiuza mkulima, anapata asilimia 30 ya bei, anayopewa mkulima mfukoni, asilimia 70 ni kodi na tozo mbalimbali. Hili kwa kweli ni jambo baya sana kwa mkulima, kwa njia hii hatuwezi kuboresha uchumi. Inasemekana kwamba, mwaka jana pia *Tanzania Coffee Board (TCB),* wamekaa pale Morogoro, wakajadili wakakubaliana kwamba, waongeze tena tozo nyingine ya asilimia mbili kwa ajili ya kununua samani za ofisi, sijui kitengo gani kimeanzishwa pale na utafiti wa kilimo cha kahawa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mkulima anaambulia asilimia 28 ya kilogramu moja anayouza kwenye Soko la Dunia, asilimia 72 zinakwenda kwenye tozo na kodi, inakwenda kwenye kodi mbambali za Serikali Kuu, za Bodi ya Kahawa, za Chama cha Ushirika, Chama KIkuu kama *KCU* au *KMCU* na vyama vingine. Halmashauri za Wilaya zinatoza kodi mbalimbali, *cess* na nyingine. Chama cha Msingi, kama hivi utafiti wa kahawa *(TACRI),* kununua samani kwenye Bodi ya Kahawa alipe mkulima; kwa kweli mkulima anapunjwa sana. (*Makofi*)

Baadhi ya wakulima wanakopa fedha benki ili waweze kulima shamba lenye tija, waweke mbolea, wanunue madawa na wanunue mbegu nzuri. Riba wanayotoa benki ni asilimia 20, kwa hiyo, wanabaki na asilimia nane ya bei wanayopata kwenye Soko la Dunia, ni

ndogo sana! Inamkatisha tamaa mkulima na mkulima anabaki hana kitu. Kazi kubwa ya kuzalisha kahawa inafanywa na mkulima; tangu apande ule mche, aukuze, autunze, aweke mbolea, apalilie, aweke madawa, avune, akaushe, akoboe, ni kazi karibia asilimia 90 na kitu anafanya mkulima, lakini anaambulia asilimia 28 ya bei ya kahawa inayouzwa kwenye Soko la Dunia; hii siyo haki hata kidogo, mkulima anapunjwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, bajeti hii naiunga mkono, lakini nitoe tahadhari ya mapema, mwakani Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Ushirika sitaiunga mkono. Naomba Wizara hii ishughulikie jambo hili kwa haraka sana. Mkulima hawezi akawa anapunjwa kiasi hiki anaangalia. Nitawaomba Wabunge wengine ambao wanalima kahawa, Mkoa wa Kagera, Mara, kule Tarime na sehemu nyingine, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Ruvuma kule Mbinga na kwingineko, tutaungana katika kukwamisha Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Ushirika. Shughulikia jambo hili, simamia mkulima asipunje namna hii, ananyonywa! *(Makofi)*

Hiyo ni tahadhali au ni onyo kwa Wizara ya Kilimo na Ushirika la mapema. Tafadhali fanyia kazi dhuluma hii kwa mkulima siyo sawasawa. Dhuluma hii si kwa kahawa peke yake hata mazao mengine ya pamba, korosho, mkonge, chai, habari ni ile ile. Kwa hiyo, kimsingi, Wabunge wote tutakaposimama hapa kuzuia bajeti hii ya Kilimo isipite, msituulize kwa nini. Sababu ni kwamba, wakulima ambao wametutuma hapa wanapunjwa sana sana, kimsingi ni Wabunge wote. *(Makofi)*

Sasa kama hiyo haitoshi, wakulima wakiona dhuluma ni kubwa kwenye kahawa na mazao makubwa ya biashara, wanakimbilia kulima mazao mengine. Wengine wanang'oa mikahawa hii, wanalima ndizi, mihogo, kabichi, nanasi, nyanya na hivi wanauza kwenye magulio ili wapate fedha ya kununua sabuni, mafuta ya taa, ada za watoto kwenda shule na kadhalika. Akiwa anakwenda gulioni, akifika njiani kizuizi, nusu ya fedha ambayo angeuza kule gulioni analipa kwenye kizuizi, gulioni anatozwa ushuru mkubwa, nusu, ndizi

shilingi 3,000 analipa shilingi 1,000 au 1,500. Suala la ushuru tumeliongelea mara nyingi hapa lakini kilio chetu hakisikiki, wakulima wanageuzwa ndiyo kitega uchumi cha Serikali, cha Halmashauri, cha Bodi hizi; kwa kweli mkulima anapunjwa sana. *(Makofi)*

Naomba sana kusema kwamba, hata hii Wizara ya Serikali za Mitaa ikae chonjo, tumesema hii tumechoka. Mwangalie mkulima huyu, wanasema mkulima ndiyo uti wa mgongo, kilimo uti wa mgongo, mgongo gani? Unavunjika mgongo huu. (*Makofi*)

Kilimo ndiyo nguzo ya uchumi, huu uchumi hii siyo nguzo, itavunjika nguzo hii. Mkulima amevumilia miaka mingi anapunjwa, Serikali ijiangalie sana. Kwa hiyo, nasema Wizara ya Kilimo na Ushirika, Wizara ya Serikali za Mitaa, mkae chonjo, bajeti zijazo tutajipanga humu ndani tutazuia bajeti zenu. Pia Bajeti ya Serikali, kwa sababu Serikali ndiyo yenye jukumu la kusimamia Wizara hizi na Halmashauri zote za Wilaya kwamba zifanye vipi. Mzielekeze vizuri, wakulima wasipunjwe kiasi hiki, wapate nao ahueni ya kazi zao, waweze kupata matunda ya kazi zao. Huu mgongo ambao tunasema ndiyo uti wa mgongo utavunjika, kabla ya kuvunjika, tutazuia bajeti hizi, itakuwa ni tabu kwa Serikali na naomba hili mliangalie. (*Makofi*)

Kwa leo nasema naunga mkono hoja, lakini bajeti ijayo tutajipanga hatutaunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, orodha ambayo tumekuwa nayo asubuhi ya leo nafikiri imefikia hapo, tunakwenda kutengeneza orodha ya jioni. Labda nimtaje tu mchangiaji wetu wa kwanza, atakuwa Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa *CUF.*

Naomba sana wale Waheshimiwa Wabunge watakaohitajika kuchangia jioni wawepo ndani ya Ukumbi wa Bunge. Ninafikiri labda wale Waheshimiwa Wabunge

wa CCM ningewataja hapa kusudi waweze kujiandaa, maana wengi wanasema hawafahamu kama wanachangia.

Sasa kwa wenzetu wa *CUF* tutakuwa na Mheshimiwa Ali Khamis Seif kama nilivyosema, baada ya kuwasiliana na *Chief Whip,* tutakuwa pia na Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah na kama uwiano wetu utaturuhusu, tunaweza kuongeza mwingine mmoja, lakini uwiano wao kwa jioni ni watu wawili. Kwa hiyo, tukiongeza mmoja kwa mujibu wa orodha niliyopewa kutoka *CUF,* ataongea Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Kwa hiyo, hawa watakuwa ni Waheshimiwa Wabunge kutoka Chama cha *CUF.*

Kutoka Chama cha Mapinduzi, pamoja na wengine, lakini tutakuwa na hawa wafuatao; Mheshimiwa Batenga, Mheshimiwa Limbu, Mheshimiwa Shah, Mheshimiwa Kayombo, Mheshimiwa Mng'ong'o, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Prof. Msolla na Mheshimiwa Mfutakamba. Kama muda utaturuhusu, tutaongeza Waheshimiwa Wabunge wengine.

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo orodha, lakini Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA na wao wataendelea kuwa kwenye orodha yetu.

Waheshimiwa Wabunge wa NCCR-Mageuzi, tumeshamaliza orodha yao. Kwa hiyo, hatutawapa nafasi tena kwa kipindi cha jioni, kwa sababu uwiano wao tayari tumeshamaliza. Huo ndiyo utaratibu tutakaoutumia jioni. Ninaomba sana hawa waliotajwa na waliosikia majina yao, tafadhali sana wajitahidi kuwahi ndani ya Ukumbi wa Bunge tayari kwa kuchangia.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli hizi mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge liliahirishwa hadi saa 11. 00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na shughuli za siku ya leo kwa jioni hii, kabla hatujaahirisha saa 1.45 usiku. Ninaomba nimwite mchangiaji wetu wa kwanza kwa jioni hii, Mheshimiwa Ali Khamis Seif aweze kuchangia.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai na uzima na kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu kuchangia Bajeti hii ya Serikali.

La pili, ninashukuru na kuwapongeza Wananchi wa Jimbo la Chambani, kwa kumchagua Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, kuwa Mbunge wa Jimbo la Chambani kwa kupitia *CUF. (Makofi)*

Mheshmiwa Mwenyekiti, Mkutano wako huu wa Bajeti ulianza tarehe 10 Aprili, 2013 na tayari Wizara mbalimbali zimeshawasilisha Bajeti zao na zimedhihirisha Miradi ya Maendeleo itakayofanyika. Pia katika mkutano huu kumeonekana kuwa, kuna mabadiliko ya utaratibu mzima wa uwasilishaji wa Bajeti, ambao umeipa nafasi Bunge kuweza kuishari Serikali na kuielekeza kuongeza fedha katika Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyoonekana, Wabunge wengi wamefurahia habari hii, lakini mimi ninasema Waswahiil wanasema mipango siyo matumizi; la msingi ni utekelezaji wa Bajeti hii na inawezekana hapa ikaonekana ni maneno mazuri, lakini utekelezaji wake ukawa una upungufu. Nina wasiwasi mkubwa katika suala hilo, kwa sababu ya uzoefu wa Bajeti zetu. Zinakuwa utekelezaji wake

haufikii katika kiwango ambacho tunaarifiwa Wabunge hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake, Wabunge wengi unakuta wanalalamika wana miradi pengine ya miaka miwili, mitatu, ambayo ilikwishatengewa katika Bajeti zilizopita, lakini Miradi hiyo haikutekelezwa. Kwa hiyo, hii ni dhahiri inaonesha kuna udhaifu mkubwa katika Bajeti yetu. Labda nitoe mfano tu nini kinachotokea katika suala zima la Bajeti hasa ya Maendeleo na niseme hili kwa kutoa mifano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya mwaka 2010/2011, Bunge lako Tukufu liliidhinisha fedha za maendeleo shilingi trilioni 3.7. Hizo ndizo fedha ambazo ziliidhinishwa ziende katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake katika Bajeti hii, fedha ambazo Serikali imetoa ni shilingi trilioni 2.2. Hii ni kuonesha kuwa, hapa kuna upungufu wa shilingi trilioni 1.5, hizi fedha za maendelo. Sasa kama nilivyosema mwanzo, bajeti utakuta inaonekana labda inakidhi kwa kuleta maendeleo, lakini matokeo yake fedha za maendeleo hazitolewi. Kwa hiyo, kinachozungumzwa hapa siyo ambacho kitatekelezwa. Mimi ninasema, bado Serikali hapa ina suala zima la kujifunza nini kilichoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuangalie Bajeti ya mwaka 2011/2012. Bunge lako liliidhinisha hapa baada ya Serikali kuombwa kuwa fedha maendeleo ziwe shilingi trilioni 4.3 na fedha ambazo zilitolewa na Serikali au Wizara ya Fedha kwa kupeleka Wizara mbalimbali na mikoa ni shilingi trilioni 3.3. Katika hali hii hapa kuna upungufu wa shilingi bilioni 926. Sasa haya ndiyo yanayotokea katika Bajeti zetu, ukakuta sehemu ya maendeleo hakuna maendeleo yanayofanywa makubwa, yale ambayo yamekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia kwa Bajeti ya 2011/2012, hizi bilioni 926 zina athari gani katika Bajeti hiyo. Utakuta hizi kama ingelikuwa kuna Wizara

zikoseshwe fedha hizi basi ingelikuwa ni Wizara tano kwa wakati mmoja. Kwa mfano, Wizara ya Kazi na Ajira, bajeti yake ya maendeleo ni shilingi bilioni sita fedha za maendeleo. Wizara ya Katiba na Sheria, fedha za maendeleo ni shilingi bilioni 30. Wiraza ya Uchukuzi, shilingi bilioni 197. Wizara ya Nishati na Madini ni shilingi bilioni 325. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni shilingi bilioni 365. Jumla ni shilingi bilioni 923. Fedha zilizokosekana shilingi bilioni 926, maana yake hizi zina athari kubwa kabisa katika suala la maendeleo. Katika Bajeti ya sasa hivi tuna shilingi trilioni 5.6, lakini fedha hizi hazitapatikana kwa uzoefu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie mwelekeo wa hii Bajeti ambayo inaishia mwezi Juni, 2013. Fedha za Maendeleo ni shilingi trilioni 4.5. Mpaka mwezi Aprili, 2013 ni shilingi trilioni 3.9. Hivi sasa kwa hii miezi miwili ina maana Mei na Juni, 2013 Serikali kweli itapata fedha hizi shilingi bilioni 642, hii bajeti ambayo tunaitumia hivi sasa na inaishia mwezi Juni, 2013.

Mheshimwia Mwenyekiti, ninahisi hapa kuna tatizo la msingi kabisa. Siyo vizuri Serikali kuona labda kuwa inakuza tu fedha kwa ajili ya Bajeti. Shilingi trilioni 11, kutoka shilingi trilioni 11 ikaenda 13, shilingi trilioni 15, leo hii tuko shilingi trilioni 18.2. Ni vizuri Wizara ya Fedha ninawashauri mambo mawili; ushauri wa kwanza ni kuwa, wapitie Bajeti karibu za miaka kumi nyuma, watakuta matatizo haya. Twende katika hali halisi, kile ambacho tutaambiwa katika Bunge hapa kionekane asilimia kama 90, 95, 98 kinatekelezwa.

Ukiangalia katika Bajeti ya 2010/2011, ilikuwa asilimia 41 ya fedha za maendeleo hazikupatikana. Hii ya 2011/2012 asilimia 21, kama hali itabakia hivi hivi inaweza kuwa karibu asilimia 18. Kinachoelezwa kwenye Bunge siyo ambacho kitakafanywa na Serikali. Kwa hiyo, Serikali wakae, watafakari na wawe wanatuletea kitu ambacho kinakaribiana na hali halisi. Kwa kuwa ninaelewa ni makisio, lakini siyo kwa kiasi hiki; kwa sababu bilioni 625, bilioni 926,

shilingi trilioni 1.5, kwa kweli hizi ni fedha nyingi, wakae waone. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Serikali ijikite katika vyanzo vya mapato vya ndani. Kwa sababu kinachoonekana ni kwamba, fedha nyingi hizi ambazo zinakosekana Serikali haipati ni fedha kutoka nje. Bado nina imani suala la uvuvi na suala la utalii, Serikali haijafanya ipasavyo. Kama ingelifanya ipasavyo, basi hapa naamini tungelipata mapato ambayo yangeliweza kuja hapa na yangeliweza kutusaidia katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uvuvi ni mbaya sana kwa kweli, haina matumaini yoyote. Mwaka 2008 uvuvi ulikua kwa asilimia tano na ulichangia Pato la Taifa asilimia 1.2. Bahari yote tuliyonayo na Maziwa yote tuliyonayo, mchango wa uvuvi ni huo. Mwaka 2008, kama nilivyosema ukuaji wa uvuvi ulikuwa asilimia tano. Mwaka 2012 kwa Ripoti ya Hali ya Uchumi wa Nchi ni asilimia 2.9. Sasa hii ndiyo hali ya uvuvi ilivyo katika nchi yetu. Pato la Taifa limechangia uvuvi kwa asilimia 1.4. Hii ndiyo hali ya uvuvi na haya yote tuliyonayo. Ninahisi huu uvuvi ukiendelezwa, basi unaweza ukatupatia fedha nyingi ambazo zinaweza zikafidia sehemu ambayo fedha zinakosekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka huu, Mipango yake katika kuendeleza uvuvi wanasema watafungua maeneo saba ya kufuga samaki kwa shilingi 217.7 milioni. Maeneo matano katika samaki wa maji baridi na maeneo mawili, Tanga na Mtwara, itakuwa ni maeneo mawili. Hivyo ndivyo Wizara inavyosema au Serikali inavyosema katika mpango wa kuendeleza uvuvi. Lingine wanasema kuwa, katika mwaka huu wataimarisha Taasisi za Utafiti, wametenga katika hili shilingi 292.3 milioni; ni vizuri utafiti ufanyike. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashirika kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Elizabeth Batenga, atafutatiwa na Mheshimiwa Dkt. Festu Limbu.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache katika hoja ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mahusiano na Uratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niipongeze Serikali na niupongeze Uongozi wa Bunge, kwa kukubaliana kuanzisha huu utaratibu au mfumo mpya wa kujadili Bajeti. *(Makofi)*

Mhehsimwia Mwenyekiti, nimekuwepo katika Bunge hili karibu miaka 17 mpaka 18, lakini nilikuwa ninaumia sana ninapoambiwa au watu wanapolisanifu Bunge kwamba Bunge ni *rubber stamp.* Kwa Mfumo huu mpya, nimeona kwamba, Bunge siyo *rubber stamp* tena, ni Chombo madhubuti ambacho kinaweza kujadili na kupendekeza na kuelekeza na Serikali ikaweza kubadilisha au kukubali mapendekezo ya Wabunge katika vipengele mbalimbali vya Bajeti za Wizara. Kwa hiyo, hilo ninalipongeza sana na nadhani tumeanza vizuri na katika miaka inayokuja mambo yatakuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niipongeze Bajeti iliyosomwa mbele ya Bunge lako Tukufu, ni Bajeti nzuri sana, ni Bajeti ambayo imewajali Wananchi kwa kiasi kikubwa na ndiyo maana Wabunge tulipopendekeza kwamba katika Wizara mbalimbali; Kilimo, Mifugo, Maji hata Nishati na Madini kwa maana ya umeme vijijini, Serikali imekubali na kuongeza mafungu katika Wizara hizo, kwa sababu hizo ni Wizara ambazo zinawagusa moja kwa moja Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini uzuri wa Bajeti na utekelezaji wake, inawezekana ikawa ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, ninaomba sana, kwa msaada wa *Presidential Delivery Bureau,* basi usimamizi uwe mzuri ili fedha hii iweze kufanya kazi ambayo itaonekana kwa Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Bajeti ni kitu, ni sawa sawa na mtu katika familia yake, baba, mama hata watoto wote wanachangia ili kufanikisha mapato na matumizi katika nyumba yao. Kwa hiyo, Wananchi wote ni lazima tuchangie, mwenye kidogo achangie, hatimaye kile tunachochangia kiweze kuturudia kwa njia nyingine katika kutekeleza Miradi mbalimbali ambayo imepangwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wanachotamani ni kupata maji katika maeneo yao kwa ajili ya mahitaji, kwa sababu maji ni uhai, maji ni kila kitu. Kwa hiyo, kama maji yatawafikia Wananchi, Wanawake wakipata maji katika umbali wa mita 400 kama ilivyopangwa hapo awali, basi Bajeti hii itakuwa imetekelezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme kama wezangu walivyosema, siyo starehe ni kitu cha kawaida kwa matumizi ya kawaida kwa mtu yeyote ambaye amepiga hatua ya maendeleo. Kwa hiyo, umeme ukipelekwa vijijini, watu watapenda kuishi vijijini. Vijana wanaofikiri kwamba mijini ndiko kwenye maendeleo, watakaa vijijini kwao wataweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa wazee ndiyo wanaobaki vijijini kulima, wazee wa kiume na akina mama ndiyo wanaobaki vijijini, vijana wanakimbilia mjini. Mojawapo ya matatizo yanayowapeleka vijana mjini ni mazingira mabaya ya vijijini. Hata na wazee wale wanakosa pa kwenda, lakini kwa kweli hali ni mbaya huko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hii *Presidential*

*Delivery Bureau,* ningepata tafsiri yake kwa Kiswahili kwa haraka haraka ningeweza kusema; ninaomba isije ikawa kama mifumo mingine ambayo imewahi kuanzishwa lakini haikufanya kazi tukaiona. Ipo mifumo mingi tu, lakini nitoe mfano wa Mikataba ya Huduma kwa Wateja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikataba ya Huduma kwa Wateja, iliandaliwa karibu kila Wizara, kila Idara na ilizindulliwa rasmi hapa Bungeni, sikukumbuki ilikuwa kipindi gani, lakini ilizinduliwa kwa kishindo sana. Kila Wizara ilikuwa inajitahidi izindue kwa kishindo cha namna yake. Katika baadhi ya Wizara hata kuku tulikula. Nikiuliza hivi sasa hiyo Mikataba ya Huduma kwa Wateja iko wapi na ilifanikisha nini, kwa sababu ililenga watoa huduma waweze kutoa huduma katika muda unaotakiwa na mfupi iwezekanavyo kwa wale wateja ambao wanawahudumia. Wapo Wabunge wengi wamewahi kulalamika hapa, hata na mimi ninaweza nikalalamika, Mbunge unaandika barua kwenye Idara ya Serikali au Wizara ya Serikali, lakini hupati majibu! Wakati mwingine unaipeleka mwenyewe kwa mkono, lakini hupati majibu. Sasa hiyo ni huduma kwa mteja?

Daktari anakupa *appointment* tena ya wiki mbili, unakwenda pale tangu asubuhi mpaka jioni hujamwona Daktari, hiyo ni huduma kwa mteja kweli? Kwa hiyo, naomba bajeti hii isimamiwe, fedha hizi zilizopangwa na hizo zilizoongezwa kwa kilio cha Wabunge zifike zinakotakiwa kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza pia ili na sisi kujiridhisha basi uwepo mfumo mwingine wa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kila baada ya miezi kadhaa, labda miezi mitatu au minne, tuwe tunaletewa taarifa hapa tunaambiwa kwamba mimi Waziri wa Maji katika vijiji kadhaa nilivyosema vitapata maji, sasa ni vingapi vimepata. Waziri wa Nishati na yeye atueleze ni vijiji vingapi vimepata umeme, hapo utekelezaji utakuwa umekamilika.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge ni kengele ya pili hiyo.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Elizabeth Batenga na sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, atafuatiwa na Mheshimiwa Betty Machangu, kwa sababu Mheshimiwa Shah naona hayupo Ukumbini.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato lazima yalingane na matumizi, lakini nafikiri tatizo la kwanza linaanza kwenye hii *question,* mapato na matumizi yetu. Ukiangalia ukweli ulivyowasilishwa na Waziri wa Fedha ama na Serikali ni kwamba, mapato ya ndani ambalo ndiyo tatizo la kwanza, hayatoshi kugharamia Miradi yetu ya Maendeleo. Makusanyo ya ndani ni shilingi trilioni 11.5, lakini bajeti ya matumizi ya kawaida ni shilingi trilioni 12.5. Kwa hiyo, hapa ndiyo unakutana na tatizo asubuhi asubuhi hata kabla hujanawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *equation* yetu ya matumizi na mapato ina matatizo yafuatayo; kwenye matumizi yetu asilimia 17 inakwenda kulipa madeni. Ukiangalia katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti, ukurasa wa mwisho kabisa kuna *chart,* kuna *pie* na mduara ambao unaonesha kwamba, ukijumlisha madeni yote na riba nafikiri na Mfuko Mkuu wa Serikali uko huko, asilimia 17 zinakatwa kwenye shilingi trilioni 18, uondoe asilimia 17, unakwenda kulipa madeni na Mfuko wa Serikali.

Unakuta kwamba, asilimia 26 lazima ulipe mishahara, lakini kwenye bajeti tunaambiwa makusanyo ya ndani, asilimia 17 zinakwenda kuwasha umeme. Sasa ukijumlisha

asilimia 17 ya kwenda kulipa madeni, asilimia 17 ya kuwasha umeme na asilimia 26 ya mishahara, jumla inafanya asilimia 60. Kwa hiyo, matumizi mengine yote yanabakiwa na asilimia 40; hapa ndiyo tatizo la msingi lilipo, asilimia 40 inayobaki ndiyo iende kwenye matumizi mengine na asilimia 40 inayobaki ndiyo iende kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kama matumizi ni makubwa kuliko mapato, basi inabidi ufanye mojawapo kati ya mawili haya; aidha, upunguze matumizi ama ufanye juhudi kubwa kuongeza mapato yako, lakini huwezi kuendelea na *equation* hii kwani haitekelezeki. Kwa jinsi ilivyo hivi unaanza ku-*fail* kabla hata hujaanza, unapoanza tarehe 1 Julai, tayari umeshavuruga bajeti haitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu mfumuko wa bei. Waziri wa Fedha ametuambia kwamba, katika kipindi cha miezi 12 kati ya Juni 12 na 13, mfumuko wa bei ulishuka kutoka asilimia 18.7 kwenda asilimia 9.4. Maana yake ni kwamba, kila mwezi mfumuko wa bei ulikuwa unapungua kwa asilimia 4.2 kwa wastani. Mimi sijawahi kuona Duniani ambapo mfumuko wa bei unashushwa kwa asilimia nne kila mwezi mfululizo na unashushwa kwa asilimia 50 ndani ya miezi 12; sijawahi kuona! Hili inawezekana lilifanyika kweli lakini lilifanyika kwa gharama gani na kwa athari kwenye uchumi na kwenye jamii? Lazima tuelezwe, suala hili linahitaji maelezo na ufafanuzi zaidi, lakini jinsi linavyokuja kavukavu hivi halijakaa vizuri, kwa sababu sera wanazotumia kushusha mfumuko wa bei kuna Sera za Kifedha *(Monetary Policies),* lakini kuna Sera za Kibajeti, *(Fiscal Policies)* na Sera nyingine kuongeza uzalishaji, kupunguza *demand* katika uchumi na kadhalika. Sasa nahitaji maelezo iliwezekanaje kushusha mfumuko wa bei kwa kiasi kikubwa namna hii vinginevyo kuna tatizo mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye hoja yangu ya tatu; vipaumbele ni vingi mno. Sura ya tatu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka huu unaokuja 2013/2014, ukurasa wa 46 mpaka 72 kuna Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati, lakini pia kuna miradi mingine

muhimu. Sasa kuna miradi ya kimkakati ya kipaumbele, lakini kuna miradi mingine ya kipaumbele. Nimejaribu kuorodhesha harakaharaka, miradi ya kimkakati ipo mitano; miundombinu, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu, utalii na huduma za fedha.

Kwenye miundombinu peke yake kuna miradi 42, reli ipo miradi sita, barabara miradi minane, bandari miradi saba, nishati miradi kumi, teknolojia ya habari na mawasiliano miradi minne na maji miradi minne, kilimo miradi minane, viwanda miradi saba, hivi vipaumbele vitatu vina miradi 57, sasa bado maendeleo ya rasilimali watu, utalii na kadhalika. Bado kwenye miradi mingine muhimu kuna maeneo 17 ambayo kila eneo lina miradi isiyopungua mitano au sita. Sioni kama kweli kuna vipaumbele, yaani kila kitu kwetu ni kipaumbele.

Ukienda katika ugawaji wa fedha sasa kwenye Mpango wa Maendeleo huoni picha kwamba kweli kuna miradi ambayo imeelezwa kwenye Mpango ndiyo imepewa fedha nyingi katika bajeti; huoni hilo linajitokeza? Kwa hiyo, nasema hii bajeti inakuwa kama bajeti ya kijamaa kwamba, kila sekta ipate angalau kidogo, ni bajeti ya kijamaa kila Wizara ipate angalau kidogo. Kuna haja gani ya kuweka vipaumbele kama kila mtu unamgawia angalau kidogokidogo? Hatuwezi kwenda na sera ya kila Waziri apate; haiwezekani! Tukiweka kipaumbele tuainishe vipaumbele na vipaumbele hivi nimesema havipo. Vipaumbele vinakuwepo unatenga mwaka huu vichache unavitekeleza unamaliza, lakini siyo vipaumbele ambavyo kwa maelezo yaliyopo kwenye kitabu cha mpango huoni yakijitokeza kwenye bajeti.

Kwa hiyo, bajeti hii naiona kama ni bajeti ya sogea nikae, kama mko wengi unamwambia mwenzako sogea na mimi nikae, sogea na mimi nikae! Huwezi kutekeleza bajeti ya maendeleo kwa utaratibu huu. Sekta zinaongezewa fedha kidogokidogo kila mwaka, kama mwaka jana alikuwa na shilingi bilioni 200, mwaka huu anaongezewa bilioni 220 na kila sekta tunadai ipewe fedha, haiwezekani hatuwezi

kwenda hivyo. Kama ni *Big Results Now* haiwezi kupatikana, itapatikana sijui miaka mingapi na lazima tuwe na utaratibu wa bajeti iwe kama mchezo wa mpira. *(Makofi)*

Mchezo wa mpira ni *first eleven,* watu kumi na moja, unachagua ndiyo wanakamata hata kama timu ina wachezaji 30, wengine wanakaa benchi wanawatazama hawa wanavyocheza ama akichoka ndiyo mwingine anaingia. Tukimaliza kutekeleza ndiyo tunaingiza mchezaji mwingine, lakini huwezi kukuta timu ya mpira wanacheza watu 30, timu ya mpira ni wachezaji kumi na moja. Tuchague sekta ambazo tunasema tunaanza na hizi nyingine zikae benchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nizungumzie kwenye viwanda. Sekta ya Kilimo inaajiri watu wengi na ndiyo inabeba watu wengi ambao hali zao ni duni, lakini tumesema kuna tatizo moja kubwa la bei ya mazao ya kilimo. Mkulima anapozalisha kwa wingi bei zinashuka, bei ikishuka kwenye Soko la Dunia mkulima anapata bei kidogo; tunamsaidiaje Mkulima? Bajeti iko kimya! Tunamsaidiaje mkulima wa Korosho? Bei ya Korosho inashuka na tumesema tuongeze thamani tusiuze Korosho yetu nje, kupeleka India na Pakistan tunakwenda kuwaajiri Wahindi. *NSSF* wamejitolea kwamba, watatoa asilimia 60 ya fedha za kuanzisha viwanda; Serikali inashindwa nini kutenga fedha hiyo? Kwenye Pamba *NSSF* wamejitolea wametoa asilimia 60 ya kuanzisha viwanda vya kuongeza thamani kwenye Pamba na kuanzisha viwanda vya pamba na nguo, lakini Serikali ina kigugumizi. Kwenye vipaumbele hapa sikuona kwenye viwanda kwamba kuna hili linatiliwa mkazo. Ninaiomba Serikali iliangalie hili kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naamini kwamba, utaratibu huu mpya wa *Budget Cycle* utatusaidia kuondoa upungufu na matatizo mengi ambayo tunayo. Naamini kwamba, hata kama hiyo ni pemandu au *Big Results Now,* zitaanza kujengwa kwenye bajeti ijayo lakini siyo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Waziri wa Fedha kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 pamoja na Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia naipongeza Serikali kwa kuja na mfumo mpya wa ku-*discuss* bajeti. Huu mfumo ni mzuri kwa sababu tulipata fursa ya ku-*discuss budget* na yale maeneo ambayo tuliweza kuiambia Serikali iongeze na ikaongeza, lakini ni mfumo mzuri kuliko ule tuliokuwa nao zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, ilivyosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, inatoza asilimia 14.5 kwenye huduma zote za simu za mkononi, *all mobile services,* badala ya kile kiasi cha asilimia 12 tuliyokubaliana. Kwa hiyo, kuna ongezeko la asilimia 2.5, lakini hapo hapo Serikali inaanzisha ushuru wa bidhaa kwa kadi za simu za mkononi, yaani *sim card*, wata-*charge* shilingi 1,450 kwa mwezi. Hiki kiasi ni kikubwa sana, ukijumlisha shilingi 2,500 na hiyo itakuwa ni kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, ...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Imefutwa!

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Naambiwa na Mheshimiwa Keissy kwamba imefutwa na kama imefutwa basi Serikali imefanya vizuri sana; naomba niipongeze kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba, asilimia 2.5 inayotozwa kwenye simu itaenda kwenye elimu. Sasa najiuliza kwa nini Idara hii ya *Telecommunication* tu, Idara nyingine za Serikali kwa nini hazichajiwi wakati tunajua kabisa elimu ni muhimu sana katika nchi hii? Kwa nini imekuwa ni kwa Idara hii ya *Telecommunication* peke yake? Naomba Waziri atakapokuwa analeta majumuisho na hilo alijibu tafadhali!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Sheria ya Ushuru wa Mafuta, Sura Namba 220, kuna ongezeko la *fuel levy* shilingi 63 kwa lita, kuna Sheria ya Petroli *(Petroleum Act)* Sura 392, ina ongezeko la shilingi 50 kwa lita. Tukumbuke pia kwamba, kuna *excise duty* kwa hayo mafuta yatakavyokuwa yameagizwa. Kwa hiyo, katika mafuta kuna kodi tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili litakuwa na *impact* kwa mlaji na siyo kwa wafanyabiashara wanaoagiza. Pamoja na hiyo, Serikali inasema kiasi fulani kitakwenda kwenye *REA* na kiasi kingine kitatengeneza barabara na hapo hapo Serikali inawa-*charge* wafanyabiashara asilimia 0.6 kama *destination inspection fee* ya biashara zote zile zinazoingia au mali zinazoingia nchini kwa *FOB* na katika hiyo asilimia 0.6, asilimia 0.4 inakwenda *REA* na asilimia 0.2 inabaki *TRA*. Sasa kwa sababu hawa wafanyabiashara wanalipa *preshipment fee* na kwa sababu hiyo *destination inspection* haipo tena, kwa kuwa ilikuwepo wakati ule *COTECNA* ilivyokuwa imefanya mkataba na Serikali ambapo mkataba ule ulivunjika mwaka 2010 Desemba, sasa kwa sababu haipo tena na Serikali inahitaji fedha kwa ajili ya maendeleo ya Wananchi, basi hiyo asilimia 0.6 iende *REA* ili kuondoa huu mzigo wa shilingi 50, ambao utakuwa umewekwa kwenye mafuta na hivyo utakuwa ni mzigo mkubwa sana kwa Wananchi. Kwa hiyo, nashauri basi hiyo asilimia 0.6 iende kwenye *REA* badala ya kuongeza shilingi 50 katika mafuta ya *petrol*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Jumuiya ya Afrika Mashariki, sheria ya mwaka 2004 ambayo inatoa msamaha kwa ushuru wa forodha kwa malighafi ya kutengeneza sabuni, yaani *lump sum.* Hapa naomba ku-*comment* kwamba, mimi sijaona sabuni za maana hapa Tanzania. Nakwambia ukweli kwamba, kwenye *super market* ukienda kama kweli ni sabuni nzuri ya miche utapata ni Jamaa kutoka Kenya. Huu ni mkataba wa *East Africa* kwamba, viwanda vitengeneze sabuni, wafanyabiashara wapunguziwe kodi ili waweze kutengeneza kitu kizuri. Ukienda kwenye *super market* au madukani, sabuni unazoziona za Tanzania *quality* yake ni mbaya.

Zamani sabuni ya mbuni ilikuwa ni nzuri sana na Komesha pia ilikuwa ni nzuri sana, lakini sasa hivi sijaona sabuni nzuri inayotengenezwa hapa Tanzania, hata za vikundi zinakuwa ni nzuri zaidi kuliko hata hizi za Wafanyabiashara wakubwa. Ukienda kwenye sabuni za unga, nyingi zinatoa povu lakini zina-*breech* nguo, ukiweka nguo ya maua uki-*compare* na Omo, ile sabuni ya Tanzania inachubua nguo zako. Kwa hiyo, sisemi wasipate hii *exemption,* lakini nataka niiombe *TBS* na Serikali yenyewe waangalie *quality* ya hizi sabuni ambazo tunawapa *exemption.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kupitia Sheria ya *Public Procurement Act* ya mwaka 2011 na *PPP* ya mwaka 2010. Serikali imefanya vizuri, kwa kurekebisha hii Sheria ya *Public Private Partnership* na kusema kwamba, zile *unsolicited bids* zisiingie kwenye ushindani kwa ajili ya kuvutia wawekezaji. Nakubaliana kabisa na Serikali, lakini nataka kuweka angalizo kwamba, lengo letu hapa litakuwa kulenga Halmashauri za Wilaya ziingie kwenye mikataba na watu *private* kwa ajili ya kuweka viwanda kwenye maeneo Halmashauri zilipo. Hii sheria ya ushindani kiasi ilikuwa inazuia wizi, kwa hiyo, Serikali kuwe na angalizo kwamba sasa hivi ndiyo mikataba mibovu itafanywa baada ya siku mbili utasikia mali za Halmashauri zinauzwa na watu wajanja na Halmashauri zenyewe kama tunavyojua tunaita mchwa. Kwa hiyo, naomba hapa Serikali iweke kanuni na sheria kali kuhusu hii mikataba itakayokuwa inaenda bila ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna pendekezo la *Labs* la kushauri ambalo lilishauri kwamba, kuwe na vyanzo vingine vya mapato na wakashauri kuuza vitalu vya misitu na uwindaji kwa njia ya mnada. Hili wazo ni zuri sana, lakini niiulize Serikali kwamba tumejiweka sawa namna gani na tumejiandaa vipi namna ya kusaidia sasa Watanzania waingie kwenye minada kama hii? Kwa sababu hizi *tender* za vitalu vya kuwinda yanakwenda malaki na malaki ya madola na wanaopata ni watu wa nje. Nataka kuangalia kwamba, mtu wa nje amekuja hapa ana pesa nyingi

anashindana na huyu Mtanzania, benki zetu ndiyo hizo hazitoi mikopo na zikitoa riba inakuwa juu; Mtanzania wa kawaida atakuwa wapi? Kwa hiyo, naomba Serikali kama inataka kuleta hili iandae vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Hotuba ya Waziri, *page 62,* Sura 148, kwa ajili ya kurekebisha mapitio ya Kodi ya *VAT* na wamesema wanapunguza mikataba na sasa hivi ndiyo wanapitia hiyo sheria, lakini hapo hapo wamefuta msamaha kwa Idara ya Utalii. Sasa mimi nasema ili kutokuwachanganya Wananchi; kwa nini Serikali isipitie Idara zote ikaona ni wapi pa kupunguza, ikapunguza kwa pamoja kwa ajili ya kuleta iwe *effected* kwa wakati mmoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *exemption* pia ya viwanda vya pamba, wakasema wanatoa kwa bidhaa ambazo zitakuwa zinatumika kwenye hivi viwanda. Nikajiuliza sasa Serikali inajuwaje kwamba hii pamba imetoka Kenya, Southern Sudan, Tanzania au wapi; ndiyo wawape *exemption?* Nataka kuangalia tu kusiwe na *abuse* ya hizi *exemptions*. Watu wanaweza wakachukua zile *exemptions* wakaleta mali au vitu vingine, lakini wakati huo huo wanapata *exemption* ya kodi na hawatengenezi nguo na tunashuhudia viwanda vya Tanzania havizalishi kiwango cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, ninaomba kuzungumzia Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 418 na Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura 245. Serikali inataka sasa hizi Wakala; *TCRA, TAA* na *EWURA* waipe *ten percent* ya malighafi yao, yaani *gross revenue.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajiuliza kwamba, tulikuwa na mashirika ya umma yakafa, tukaanzisha wakala zika-*operate* vizuri sana na zilikuwa zinalipa *ten percent* ya *profit,* sasa Serikali inataka walipe *ten percent of gross revenue*. Ninaogopa, kwa sababu kama mashirika tuliyashindwa tukaanzisha wakala na sasa hivi tunachukua hii fedha kutoka kwa hawa wakala ambayo ni *ten percent*

ya *gross revenue*; naiomba Serikali tuwe makini ili na hizi wakala nazo zisije zikaendelea kufanya vibaya na *at the end of the day,* ikawa tunaanza kutafuta mtu wa kununua mashirika ambayo yamekuwa hayafanyi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Betty Machangu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Zitto Kabwe hayupo, Mheshimiwa Gaudence Kayombo hayupo, tutaangalia huko mbele wachangiaji wengine wanaweza wakaziba hizo nafasi. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Mfutakamba na Mheshimiwa Iddi Mohamed Azzan ajiandae kama atakuwepo, kama hatakuwepo basi tutaendelea na mchangiaji mwingine.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Bajeti ya Serikali. Kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Bajeti hii pamoja na upungufu kidogo, lakini ina lengo kubwa la kumsaidia Mwananchi apate umeme vijijini, kwa sababu fedha zimeongezwa na apate maji kwa sababu bajeti ya maji imeongezwa, sisi wafugaji kule Igalula tuweze kupata miundombinu ya ufugaji, kwa sababu Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeongezewa fedha na pia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la vipaumbele vya bajeti, nimesoma Taarifa ya Mheshimiwa Waziri Wasira, nimeangalia Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mgimwa na pia Taarifa ya Kamati ya Bajeti. Ninapongeza kabisa utaratibu huu wa kuwa na bajeti. Nampongeza Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ni mzuri, tuendelee nao. Hata hivyo, napenda kusema suala la vipaumbele kweli nimeona Kamati ya Bajeti imependekeza labda kilimo, miundombinu na nishati. Ukiacha elimu, afya na maji, utaratibu wa maendeleo uko kama virutubisho

vinavyohitajika katika mmea. Ile sayansi ya mmea kuna baadhi ya virutubisho kwa mfano, *boron*, madini haya yakikosekana ule mmea unaweza kuwa mzuri kabisa, ukapata mpaka maua, lakini usipate matunda. Sasa nilikuwa nafikiria tutafute vyanzo zaidi vya mapato ili kuisaidia Serikali iende na vipaumbele vyake hivi kama ilivyoainisha kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Wasira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika Hotuba ya Mheshimiwa Wasira, hakuzungumzia jinsi ya kuunganisha Reli ya Kati na *TAZARA* ili tuweze kupata uwezo wa kuleta meli kubwa Bandari ya Dar es Salaam, kwa sababu hii bandari ipo. Hotuba ipo *silence* kwenye Gati 13 na 14. Gati hili lijengwe kwa utaratibu wowote, kama tutachelewa kujenga hili Gati, Mombasa watatupita na Nkala Msumbiji watatupita. Mwenyezi Mungu, ametupa rasilimali hii tunachelewa kuitumia. Kwa utaratibu wowote, naomba Gati Na. 13 na 14 liwe kipaumbele katika bajeti yetu, tujenge haraka. Kenya wameshajenga Gati Na. 17 na 18 na mwaka kesho wataanza kuingiza meli za *forth generation,* ambazo zinabeba *twenty foot container equivalent,* kontena 10,000 mpaka 15,000 kwa meli moja. Ingawa tuko *natural hub* ya nchi hizi zinazotuzunguka zisizo na bahari; DRC Kongo, Rwanda, Burundi, Zambia na Malawi, tutakosa mizigo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Ripoti ya Benki ya Dunia imesema waziwazi kwamba, hii ni *get away* yetu, Dar es Salaam tuiimarishe haraka ili tuweze kupata pato kubwa na tuweze ku- *finance* bajeti hii ambayo tunahangaika kwamba fedha zitafutwe wapi. Kwanza, fedha ziko bandarini hasa ya Dar es Salaam. Tusimamie tu ukusanyaji wa mapato na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Charles Tizeba, wanafanya kazi nzuri pamoja na Katibu Mkuu - Eng. Omar Chambo. Wizara ya Fedha iisaidie *TRA* ili nayo isimamie kidete zisitoke kontena nyingine bila kulipiwa ushuru unaostahiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kodi ni lazima tuangalie utaratibu gani tunaweza kuanza ku-*charge*

hizi kampuni zinazofanya *exploration* ya *oil* na gesi. Hili naona limesahaulika, lakini ni lazima kwenye marekebisho ya kodi zetu, tuunganishe hawa watu na hasa wale wanaotoa huduma, *subcontractors* wanaotoa huduma waanze kutozwa kodi, kwa sababu baadhi ya vifaa wanavyotumia ni vya teknolojia ya hali ya juu, tukiwaachia kwa kuwapa *exemptions* tutaendelea kupotea. Nashukuru sana *exemption rate* tumesema itapunguzwa mpaka iwe asilimia moja ya *GDP* kutoka asilimia tatu. Napongeza hilo, twende kwa utaratibu kama huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala la msingi la Deni la Taifa. Suala la Deni la Taifa nimeona linazungumziwa kwa wasiwasi. Nimefanya tafiti ya haraka nikaangalia uhimilivu wa Deni la Taifa na hili unalitazama katika kugawanya deni na *DGP,* yaani Pato lako la Taifa. Nimeangalia nchi nyingi ambazo zina takwimu zinazolinganishwa na Shirika la Fedha Duniani *(IMF)* na Shirika la Ujasusi la Marekani *(CIA)* ndiyo *documents* zile zipo. Sasa tumetazama Tanzania, ukiangalia *ratio* ni asilimia 40, ukiangalia Ghana asilimia 50, Kenya asilimia 47, Mozambique asilimia 47, Nigeria asilimia 16, Norway wenzetu kwa sababu ni uchumi mkubwa sana ni *negative* sitini na saba, yaani wao wameshalipa yale madeni, bado wana kiasi kikubwa cha *reserve* kwenye Serikali. Sisi ni asilimia 40, hoja kubwa hapa kwenye deni ni kwamba fedha zile zimetumikaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za lami tunaziona, Miradi mbalimbali ya Maji inakuja, sasa hayo ndiyo matumizi bora ya ukopaji. Tuendelee kuishauri Serikali, nimeona sasa hivi kuna dola milioni 700 tumepata ile *Euro Bond* imekwenda vizuri, tunakopesheka. Kwa hiyo, sisi tuna-*manage* deni letu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tu sasa kuna Kitengo nafikiri ni cha *ODM* ambacho kinasimamia suala la ukopaji na jinsi gani yale madeni yatalipwa. Hii taasisi ambayo inahusisha Makatibu Wakuu mbalimbali, samahani ni *DMO* – Ofisi ya kusimamia Deni la Taifa, ishirikishe pia watu wa jamii; yaani zitafutwe taasisi za jamii ziweze kushirikishwa

ili zione vile vipaumbele katika ulipaji wa deni hili vinakwenda vizuri na tuweze kukuza uchumi wetu haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa fedha zilizoongezeka kwenye Nishati na Madini ni kwamba, kule Igalula utapatikana umeme wa uhakika na minara itapatikana, kwa sababu ya mawasiliano ya sayansi na teknolojia, fedha zimeongezeka. Kwa hiyo, ninaomba tujitahidi sasa, tatizo tunalo katika ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye madini hasa dhahabu.

Ripoti ya Kofi Annan imesema tangu mwaka 1998 mpaka 2011, dhahabu tuliyouza ina thamani ya bilioni 27, lakini malipo ambayo Serikali imepata ni milioni 447. Tutazame hili kwani kuna mahali ambapo hizi kampuni za madini hatuzitozi vya kutosha. Najua ile *TMAA* inafanya kazi yake, lakini iongeze bidii ili tukusanye fedha nyingi zaidi kutoka kwenye hizi kampuni zetu mbalimbali za madini. Pia kampuni za mawasiliano tuwatoze kodi. Wote tunafahamu kwamba, Kenya, Uganda na Rwanda wanakusanya fedha nyingi kuliko sisi, kwa hiyo, naomba sana kile kifaa cha ku-*monitor* fedha kiasi gani zinaingia kwenye kampuni hizi za simu kisimamiwe vizuri tupate mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho japo siyo kwa umuhimu, pale Tura na sisi tuna *querry.* Ninaenda kwenye ukurasa wa 17 wa Ripoti ya Mheshimiwa Wasira, kifungu cha 36 kuhusu *querry,* tunahitaji Tura na sisi tupate mrabaha, kwa hiyo, *TMAA* ipige hesabu tunahitaji fedha kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mfutakamba. Nilimwita Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, lakini simwoni ndani ya Ukumbi wa Bunge. Naomba nimpe nafasi sasa Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Sitta, lakini kwa taarifa rasmi nilizonazo, Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, wamekwenda kushiriki

mkutano unaohusu masuala ya UKIMWI, wakishirikiana na Marais wa Nchi za Afrika. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Mbarouk Mohammed. Hapa nimeandikiwa Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, hayupo, basi tutaangalia baadaye ngoja tumwite mwingine halafu tutawasiliana na *Chief Whip* wa *CUF.*

Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed hayupo, kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Zaynab Vullu na Mheshimiwa Bwanausi ajiandae.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi hii na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji katika bajeti hii ya leo.

Awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha sisi sote kuwa humu ndani na *Inshallah* atujalie katika kila lililokuwa la kheri. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia Bajeti ya Taifa na ukiangalia ongezeko la watu linalotokea katika nchi yetu siku hadi siku, naipongeza Serikali kwa jitihada zake ambazo imeweza kuwekeza katika maeneo ambayo yataboresha na kuimarisha maendeleo ya Wananchi wake. Pia naiomba Serikali izidi kuangalia vile vipaumbele muhimu. Kwa mfano, tukiangalia suala la maji, tunaipongeza Serikali, lakini bado inahitajika nguvu ya ziada iongezwe kwa ajili ya maeneo ambayo bado Serikali haijafika. Mwananchi anachukua muda mrefu sana kuhangaika kupata maji. Ukiangalia kwenye sekta ya uzalishaji, anaacha kuzalisha mambo mengi sana, muda mwingi anautumia katika kutafuta maji na kwa upande wa akina mama wanaacha kulea watoto. Ni muhimu sana tuiombe Serikali iendelee kuongeza fungu la fedha kwenye Wizara ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kwenye suala la kuendeleza uchumi, miundombinu ni muhimu sana. Wenzangu wamezungumzia suala la miundombinu katika maeneo mengi, mimi naomba nigusie suala la miundombinu

ya barabara. Tunashuhudia barabarani magari mengi yanayokwenda nje ya nchi kusafirisha mizigo na muda yanaotumia yakiwa barabarani. Kwa bahati mbaya sana, pamoja na juhudi za Serikali, ninaipongeza kwa kufungua milango ya njia ya barabara kutoka Dar es Salaam kuelekea mikoani, lakini bado kuna tatizo. Naiomba basi iangalie ni vipi itaweza kuongeza njia nyingine zinazotoka au kuingia Dar er Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kutokea Dar es Salaam kupitia *Morogoro Road* kuja Dodoma na kwenda maeneo mengine, linapotokea tatizo magari ya mizigo yaliyosheheni bidhaa mbalimbali zinazoingizwa nchini au kutoka kwenda nje ya nchi, yanakuwa yamesimama hayaendi kokote kwa saa kadhaa. Sasa ni wakati mwafaka Serikali ikaangalia uwezekano wa kuweka njia nyingine, ikafungua barabara nyingine, siyo lazima kila mtu apite *Morogoro Road*. Unaweza ukaingilia njia ya Kisarawe ukatokea *Morogoro Road* au ukatokea Morogoro moja kwa moja. Hii nayo pia itasaidia kupunguza msongamano wa magari katika kuendeleza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamezungumzia suala la Deni la Taifa. Kuwe na jitihada mahususi ili kuondokana na hili suala la Deni la taifa kwa sababu kuwa nalo ni kukwamisha maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Serikali, kuna suala la ongezeko la bei ya mafuta. Ukiongeza bei ya mafuta hata kama ni senti hamsini au shilingi moja tu, umeubebesha mzigo huu wa bidhaa kwa Wananchi. Lengo ni zuri, nia ni nzuri, lakini basi tuangalie ni vipi Serikali itahakikisha Mwananchi habebi huu mzigo wa ongezeko la bei ya biadhaa, kwa sababu ukipandisha mafuta tayari umeongeza bei ya vyakula, usafiri na kila kitu. Hali hii itamfanya Mwananchi akose nafasi ya kupumua vizuri katika kujitafutia maisha na kuendeleza kipato chake. Hatuna sababu ya kumwumiza Mwananchi kwa kumpa mzigo mzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati iliyowekwa ya kuimarisha na kuboresha ni mizuri, lakini bei ya mafuta ikiongezwa, naomba sana tuangalie ni vipi Serikali itasimamia na kuangalia ni vipi bei za vyakula hazitapanda, kwa sababu bei ya mafuta ikipanda, bei ya chakula itaongezeka. Sasa hivi bei ya mafuta imeshuka na kila mtu anafurahia. Ukienda madukani mchele umeshuka mpaka shilingi 1000 au 1200 kwa kilo. Pamoja na kwamba, iko juu lakini afadhali Mwananchi amepata ahueni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakapoongeza bei ya mafuta, umeongeza pia mzigo wa nauli. Tunashuhudia wafanyakazi wengi hasa walimu wanapofuata mishahara yao inabidi watumie fedha kwenda kufuata mishahara. Wafanyakazi walioko vijijini, ukiwaongezea nauli na mshahara kama hakuupanga vizuri, huu mzigo anakuwa ameubeba mfanyakazi bila kutarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali yangu kwa kuwa ni sikivu, basi iangalie ni vipi itaweza kutatua tatizo hilo na kuepusha mzigo huo ili Wananchi wasiumie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Zaynab Vullu, kwa mchango wako. Nilisema sasa nitamwita Mheshimiwa Bwanausi na Mheshimiwa Mendrad Kigola ajiandae.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Hotuba hii ya Bajeti ya Serikali. Pia ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya na wanastahili pongezi kwa kazi hii ambayo Watanzania wamekuwa na matumaini makubwa kwenu katika kuhakikisha kwamba, tunapata maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kupanga bajeti ni jambo la kwanza, lakini ili bajeti hii iweze kufanikiwa ni lazima kuwe na nidhamu katika kukusanya mapato, katika kugawa mapato hayo, lakini pia katika kusimamia mapato hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali kwenye eneo hasa makusanyo kwa kweli bado mkazo wa ufuatiliaji wa mapato ni mdogo sana. Kwa mfano, hapa *TRA* wamekadiriwa kwamba, wakusanye karibu trilioni 10 hivi, lakini pia ikiunganishwa na Halmashauri bilioni 385. Mheshimiwa Waziri nina uhakika kabisa kwamba, mikakati mikubwa ikiandaliwa mapato haya upo uwezekano mkubwa sana wa kupanda na kuifanya Serikali iweze kutekeleza shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa sana la Wizara ya Fedha la kutogawa fedha hizi kwa wakati. Jambo hili limeleta usumbufu mkubwa sana na kufanya miradi mingi sana isiweze kufanikiwa. Wakati fedha zinapatikana mara nyingi sana inakuwa ni mwishoni kabisa mwa mwaka wa fedha na hivyo kupelekea fedha hizi kwenye Halmashauri kutotumika vizuri kwa sababu ya muda mfupi wa maandalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la usimamizi wa fedha. Kwa mfano, fedha nyingi zinazopelekwa kwenye Halmashauri zetu kutoka Wizarani na kutoka Hazina zinakosa ufuatiliaji kutoka kwenye *source* ya fedha zilikotoka. Nashauri sana kila Wizara iunde timu ya ufuatiliaji wa fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri ili kujua kweli fedha zile zimepatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pendekezo lingine ambalo naona lipo tatizo. Tumependekeza muda mrefu sana hapa kwamba, ratiba ya Bunge iende sambamba na ratiba za vikao vya Halmashauri zetu. Jambo hili la Waheshimiwa Wabunge kutoshiriki kwenye Mikutano ya Halmashauri, kunapelekea Waheshimiwa Wabunge kutotoa mchango ipasavyo katika utekelezaji wa miradi katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, pamoja na tatizo hilo la ratiba, lakini fedha zinazotoka Wizarani kuelekea kwenye Halmashauri zetu ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wakapata nakala ili wajue ni kiasi gani cha fedha kilipelekwa kwenye Halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali sana na kwa kweli wale waliosema Serikali ya CCM siyo sikivu siyo kweli. Nadhani tumedhihirisha kwa kiasi kikubwa sana kwenye bajeti hii kwamba, Serikali ya CCM ni sikivu; kwa kuwa mapendekezo mengi ya Waheshimiwa Wabunge yamezingatiwa kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwa na uhakika sasa kwamba, suala la umeme kwenye Jimbo Lulindi katika Kata ya Chiwata, Nanjota, Mbuyuni, Nyamalenga, Uchauru, Mnavira na Chikoropola sasa watapata umeme kupitia Mradi wa *REA*, tunaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nyongeza ya fedha zilizopelekwa kwenye maji zinapelekea kutoa imani kwa wananchi wa Jimbo la Lulindi sasa kwamba, miradi mikubwa kama ile ya mradi wa Chiwambo, mradi ule wa utoaji wa maji kutoka kwenye Mto Ruvuma kuelekea kwenye maeneo ya Mkaliwata, Manyuli, Namiyomiyo na Mnavira, pamoja na Nachipingo utaweza kutekelezwa. Naamini kabisa kwamba, nyongeza hii ya fedha itanufaisha na pia itahakikisha kwamba maji yanapeleka katika Kata Mpindimbi kupitia mradi wa Miwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie pia suala la elimu. Kama wachangiaji wengine walivyoeleza na kama vile alivyoeleza ndugu yangu Mheshimiwa Juma Njwayo, kwa kweli suala la matatizo ya Walimu tusipolitilia maanani na hasa Hazina kutoa fedha kwa wakati, litaisumbua sana nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote sisi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba, mazingira ya Walimu katika

maeneo yetu si mazuri. Wanaishi katika maeneo ambayo wakati mwingine hata kufuata mshahara inabidi aende, alale Wilayani, arudi siku ya pili kwa ajili ya kufuata mshahara wake. Hili linapelekea kuwa tatizo kubwa zaidi pale ambapo fedha zenyewe upelekaji wake na ulipwaji wa baadhi ya madeni unakuwa hauzingatiwi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba, Wizara ya Fedha sasa itahakikisha kwamba madeni na fedha zinazohusiana na Walimu ambao ndiyo asilimia kubwa ya waajiriwa kwenye Halmashauri zetu zinatengwa fedha na kupelekwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona si vyema nisigusie pia katika muundo wenyewe wa Serikali yetu. Muundo wa Serikali yetu huanzia kwenye maeneo ya Vijiji, Mitaa pamoja na Vitongoji. Lakini bado Serikali yetu haijaona umuhimu mkubwa sana wa kuhakikisha viongozi waliopo kwenye Vijiji na Mitaa na Vitongoji wanapewa umuhimu angalau kufikiriwa katika suala zima la kuwawezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwamba, Serikali kwa kuwa inayo dhamira kupitia kwenye Halmashauri zetu zile fedha zinazorejeshwa kama asilimia kwenye Vijiji na Mitaa yetu, pia nazo zitumike vizuri kuhakikisha kwamba, zinatoa motisha kwa viongozi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoweza kuhakikisha kwamba mfumo wa mawasiliano unapewa umuhimu, naipongeza Serikali kupitia Wizara husika kwa jinsi ambavyo imepanga utaratibu wa kuweka minara katika maeneo yetu. Lakini minara hiyo haiwezi kujengwa kama fedha hizi hazikutolewa na Hazina kwenda kwenye Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri Wizara hizi zinazohusika na suala la mawasiliano zipewe fedha kwa wakati. Nashukuru kwenye mpango wa mwanzo, Jimbo la Lulindi, wananchi wa Kata ya Likumbulu, Kata ya Sindano wamewekwa kwenye awamu ya kwanza kupata minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo tatizo kubwa sana katika Kata ya Chiwata, Mkundi, Mkululu na Chikolopola, ningeomba sana upatikanaji wa fedha uweze kupatikana kwa wakati ili na maeneo haya mengine ambayo hayaku-*opt* kwenye awamu ya kwanza yaweze kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine muhimu sana ambalo naona ni vizuri sana nilichangie kwenye bajeti hii ni suala la kilimo. Tumeamua kuwa na utaratibu wa kuwa na Kilimo Kwanza. Najua Wizara ya Kilimo inafanya juhudi kubwa sana, lakini kwenye suala la ruzuku za pembejeo za kilimo bado suala hili lina utata mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, fedha hizi hazipatikani kwa wakati na fedha hizi zinapopelekwa ni wakati ambapo pembejeo zenyewe hazitakiwi kwa wakati huo. Lakini pia hata mgawanyo wa pembejeo hizo hauleti tija na maeneo mengine fedha hizi zinatumika vibaya. Kwa hiyo, naiomba Hazina kwamba, izingatie misimu ya kilimo kwa kutoa fedha zile mapema ili Wizara ya Kilimo isimamie vizuri na kuhakikisha ruzuku hizi zinapatikana vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa safari hii kwa zao la korosho ningependa kuipongeza sana Bodi ya Korosho kwa kuhakikisha kwamba, wananchi wamepata pembejeo kwa wakati, lakini pia kwa bei nafuu sana. Safari hii Mfuko wa pembejeo wa mbolea ya *sulphur* umepatikana kwa 15,000/= badala ya 60,000/= ambayo ilikuwepo kwenye msimu uliopita. Kwa kweli napenda sana kuipongeza Bodi ya Korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maboresho ya Mfumo wa Kodi. Kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameonesha kabisa kwenye ukurasa wa 63 kwamba kutakuwa na punguzo la kiwango cha chini cha kodi kwa wafanyakazi kutoka asilimia 14 hadi 13. Nataka niseme kiwango hiki ni kidogo mno. Ni mwanzo mzuri, lakini kwa kweli kuna haja kabisa ya kuhakikisha kwamba,

mfanyakazi anapewa unafuu katika suala zima la kodi maana yake wafanyakazi kodi wanayolipa ni kubwa kweli ukilinganisha na hali ya maisha ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ningependa nizungumzie suala la wastaafu. Hali ya wastaafu wetu ni mbaya sana. Kwanza, kiwango ni kidogo na ningependa kumwomba Waziri, kwa kweli aone uwezekano wa kuongeza kiwango kile ambacho wastaafu wanapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, hata muda wa kupata zile fedha zenyewe. Mara ya kwanza walikuwa wanapata baada ya miezi sita, baadaye wakarekebisha ikawa wanapata miezi mitatu, lakini haiwi miezi mitatu. Kwa hiyo, namwomba sana Waziri wa Fedha kwenye eneo hili wale wanaoshughulika na kitengo hiki cha wastaafu pale Wizara ya Fedha hebu jaribu kuwaonea huruma wastaafu hawa kwa kuwapelekea kiwango kile kinachostahili kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nirudie kukushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Bwanausi kwa kujali sana muda.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Kigola, halafu Mheshimiwa Magdalena Sakaya ajiandae.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nianze kwa kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mufindi Kusini hasa Kata ya Mbaramaziwa kwa kuichagua CCM, kwa kumchagua Diwani wa CCM, tumepata ushindi wa kishindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuishukuru Serikali kwa mipango yake mizuri ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. Leo hii tunajadili masuala ya mapato na matumizi kwa Serikali. Huu ni mpango mzuri kabisa na mpango huu nimeupenda sana kwa sababu tulianza kujadili kila Wizara na kila Wizara tumeshaona matatizo yake na changamoto na tukapitisha zile bajeti na leo sasa tunakuja kujadili mfumo mzima wa Serikali jinsi zitakavyotumika hizi fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu matumizi ya Serikali yamepanda na vile vile makusanyo ya Serikali yamepanda. Tuna malengo kwamba tutakusanya trilioni 18, mwaka jana ilikuwa trilioni 15. Maana yake tumepanda kwa trilioni tatu imekuwa zaidi na matumizi vilevile yamepanda kufuatana na mahitaji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nimekipenda sana, kwanza, nimesoma Mpango wa Taifa na Hali ya Uchumi wa Taifa letu. Tulivyosoma, tukaja kuangalia sasa tunakwenda kukusanya na tukienda kukusanya tunakwenda sasa kupanga, tutatumiaje yale matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vile vile niishukuru Serikali kwa kuangalia hata sekta za watu binafsi. Kwa sababu kwenye Wizara ya Kazi na Ajira waliangalia hata Sekta Binafsi kwamba, mishahara imepandishwa kwa asilimia ambazo zilitajwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri wananchi waelewa vizuri kwamba Serikali imepandishwa mishahara kwenye Mashirika ya Umma; Serikali imepandisha mishahara kwenye mashirika ya watu binafsi. Kwa mfano, Viwanda na Biashara ni asilimia 43.8 imepandisha mshahara, hoteli na huduma za majumbani ni asilimia 55, ulinzi binafsi asilimia 46, madini asilimia 25, afya asilimia 65 na Serikali imekubali kabisa kupandisha viwango vya mishahara, kuangalia kwamba maisha sasa hivi yamepanda na mishahara lazima ipande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utakuta kuna viwanda vingine ambavyo ni vikubwa vinaanza kupunguza ile asilimia

ambayo imepangwa na Serikali na tumeipitisha hapa Bungeni. Sasa na sisi Wabunge tukisikia kwamba kuna makampuni hayafuati utaratibu wanaanza ku-*bargain* asilimia za kwao, sisi hatutazielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba, Vyama vya Wafanyakazi wasikubaliane kabisa, sisi tumeshapitisha hii. Tuliyopitisha Bungeni ndiyo Serikali imeshapitisha moja kwa moja. Kwa hiyo, Vyama vya Wafanyakazi lazima vifuate masharti haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, tukisema tumepandisha mshahara, halafu tena ukapandisha kodi. Kwa mfano, sasa hivi kodi tumesema tumepunguza kama asilimia moja. Halafu unakuwa haujapandisha mshahara kwa sababu kodi bado ipo juu na mishahara ipo juu. Sasa uwiano huu ni mdogo sana. Kwa hiyo, bado maisha yatakuwa magumu sana kwa wafanyakazi, tutakuwa bado hatujawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri wa Fedha aiangalie hii hesabu ya kodi kwa wafanyakazi wetu, bado ipo juu sana. Sasa tukipandisha kodi halafu tukasema na mshahara umepanda, hapo bado *formula* inakataa, inaonesha kwamba hatujapandisha kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ni la msingi sana ambalo nimeliona ni kwamba, ukiangalia Walimu mishahara yao bado ni midogo na makato ni mengi sana, sasa hapo bado hatujawasaidia. Sasa namwomba Waziri wa Fedha, hili ni suala la kuangalia tena upya na vile vile ningependa kuomba kwamba haya mabadiliko ya mshahara lazima twende na muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema mabadiliko ya mshahara yataanza *effectively* mwezi Julai. Sasa tusianze kusikia tena watu wanaanza kudai malimbikizo, tunaomba twende na muda, ndiyo maana bajeti tumeibadilisha, tumeanza kuijadili mwezi Aprili na tunamalizia mwezi Juni ili mwezi Julai mabadiliko yote yawe yameshafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kuna watu walikuwa hawajapandishwa madaraja, waanze kufanya hesabu zao vizuri hasa Sekta ya Elimu yenye matatizo makubwa na Sekta ya Afya, waanze kupandishwa mwezi huu unaokwisha na mwezi Julai, hesabu iwe imekwishakamilika, tusisikie malimbikizo, tusisikie sijui hesabu ilikosewa wapi, hapana. Walimu walipandishwe madaraja, watu wa Afya wapandishwe madaraja, kila kitu kiende kwa hesabu nzuri, ndiyo tutakuwa tunakwenda na mfumo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika bajeti imelenga katika maeneo mengi sana, tunasema kwa mfano, kwenye vijiji vyetu masuala ya maji, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea. Masuala ya maji ni sawasawa, kwa mfano, kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini wananchi kwa upande wao walishachangia gharama kwa mfano, wananchi wa Sawala, wananchi wa Kibao na sehemu nyingine mpaka kule Kiponda kuna vile visima, bahati nzuri tumeweka kwenye mpango tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii fedha namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aiangalie sana, fedha tumeshaiweka kwenye mpango na mwaka huu tuhakikishe wale watu wanapata maji. Tunapokuja mwakani tusianze kusema bajeti sijui ilikuwa imefanya nini? Ndiyo maana kuna trilioni tatu pale imeongezeka, kwa ajili ya ku-*cover* yale matatizo mengine ambayo tulishindwa na wananchi tumeshawambia kwamba, mwaka huu sehemu kubwa watatatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine bahati nzuri kwenye sekta ya umeme tunakwenda vizuri na Mheshimiwa Waziri alishaniahidi, amenitengea bilioni 1.9 kwa ajili ya kupeleka umeme kule Malangali. Sasa hiyo bilioni 1.9 sitapenda tena mwakani kuanza kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua mwakani tukifika tutakuwa tumeshafanya tayari tumemaliza na wananchi kule walisharuhusiwa waanze kufanya *wiring* ya umeme na juzi

nilivyokwenda walinipongeza wakasema wameanza kufanya kazi. Sasa na bajeti imesema kwa hiyo, kwa hili siwezi kupata wasiwasi kwa sababu tulishaitenga tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwenye vituo vya afya lazima tuangalie. Bahati nzuri kwenye vipaumbele vipo. Kwenye vituo vya afya kuna matatizo ya madawa na hatutapenda matatizo haya ya madawa yaendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu suala lingine ni la wahudumu, tuna zahanati nyingi sana, tuna vituo vya afya vingi sana, lakini wahudumu bado ni tatizo. Hebu Serikali ijikite sana kuangalia kusomesha hawa watumishi wa Sekta ya Afya, nao ni muhimu sana ili tuhakikishe kwamba kwenye zahanati zetu na kwenye vituo vya afya Waganga wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi hapa nimetembelea kwenye hospitali moja ya Kibao; wahudumu pale hawapo na ukienda huko kwenye hospitali kuu wanasema wao wafanyeje? Sasa naomba Serikali kwenye bajeti hii ihakikishe kwamba inaongeza ajira kwa upande wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka niongelee hapa ni suala la barabara. Bahati nzuri sekta ya barabara inajitahidi sana, lakini mwaka jana tulitenga fedha kwa ajili ya kutengeneza ile barabara ya Nyororo mpaka Mgololo kwa kiwango cha lami na hatukufanya upembuzi yakinifu na mwaka huu tumeiweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sitapenda tena mwakani tukija, tunaona ile fedha bado haijatumika hata tukisema upembuzi yakinifu, sisi hatutaelewa. Tunapenda mwaka huu upembuzi yakinifu tumalize, mwakani tunapokuja tunaanza kujenga kwa kiwango cha lami ili tuwe tumeshamaliza moja kwa moja ndiyo bajeti tutasema inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile fedha za Halmashauri. Kule Halmashauri wanapata shida sana, fedha zinakwenda kipindi cha mwaka wa fedha kimeshapita.

Bahati nzuri haya makosa tumeshayaona na Mheshimiwa Waziri wa Fedha anaelewa, yamesharekebisha. Tunafikiri mwaka huu itakuwa inakwenda *intact,* hatutapenda tusikie tena Halmashauri wanasema wanapata fedha za maendeleo kwa kuchelewa, hapana, kwa hiyo, lazima iende na muda kama tulivyopanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine Mheshimiwa Waziri wa Fedha nadhani anajua, kuna wale watu wa Mgololo, bado wanapata shida sana hawajalipwa mafao yao. Bahati nzuri imeanza kama miaka sita pamoja na kwamba kesi ipo Mahakamani na Serikali imekubali kuitoa hiyo kesi Mahakamani. Naiomba Serikali itoe haraka hiyo kesi Mahakamani na iwalipe wale watu. Wale watu walishinda na Serikali mkawapeleka Mahakamani hawana kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hiyo ni *critical issue* kwa sababu wale watu wanapata shida sana halafu watu wengine wanakufa. Sasa pale mtu akifa, maana yake anakosa haki yake. Sasa namwomba hili aliweke kwenye bajeti, kwa kuwa tumeongeza bajeti ya Taifa trilioni tatu na Mheshimiwa Waziri bahati nzuri analifanyia kazi na hapa naweka msisitizo tu kwamba, baada ya miezi mitatu au minne awe ameshawalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuliongelea sana ni kuhusiana na mfumko wa bei. Sasa hivi Mheshimiwa Waziri amesema ameanza ku-*balance,* lakini ukiangalia mfumko wa bei bado haja-*balance*. Kwa nini nasema bado, bado kwa sababu katika uchumi wa nchi yoyote ile duniani, ukiongeza bei ya mafuta bado huja-*control* mfumko wa bei kwa sababu mafuta yanatumika kwenye sekta zote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia sekta za viwanda, inatumia mafuta, ukiangalia usafirishaji wa bidhaa, hata ukichukua bidhaa za kawaida kwa mfano, wakulima wanasafirisha mahindi, lazima watumie magari, sasa kama bei ya mafuta ipo juu, maana yake hata usafirishaji

huo utakuwa juu, halafu vitu vile lazima bei yake itapanda. Yaani ukienda kwenye *logic* ya kiuchumi kamili, bado hujafanya kitu chochote. Sasa hivi utakuta sukari chumvi na hata huduma za hospitali zitapanda kwa sababu mafuta yapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia hesabu ya mafuta, Mheshimiwa Waziri wa Fedha akisema amepandisha mafuta tayari atakuwa ameliingiza Taifa kwenye ugumu wa maisha, hakuna *factors* nyingine ambayo utaiangalia ukipandisha mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kwa mfano mafuta ya taa, mafuta ya taa tumesema bei haijapanda na sababu kubwa tunasema kwamba tunaangalia uwiano kati ya petroli na mafuta ya taa, yaani hatujapunguza bei ya mafuta ya taa kwa sababu watachakachua, bado hatujasaidia kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni uchakachuaji wa mafuta, lazima tuweke sheria kali, mtu atakayefanya hivi tumchukue sheria kali. Wananchi wengi wanaotumia mafuta ya taa ni watu wa vijijini na kule Serikali bado haijapeleka umeme na kama umeme haujakwenda vijijini, halafu unapandisha mafuta ya taa, bado unamtengenezea maisha magumu huyo mtu wa kijijini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kigola. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Baada ya Mheshimiwa Magdalena Sakaya atafuata Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii muhimu ili nami niweze kuchangia kidogo kwenye bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze hotuba yangu kwa kushangaa, kila mwaka tunapoletewa bajeti ya Serikali, tunaona vyanzo vya mapato ni vile vile. Nakaa najiuliza kwamba, inapokuja bajeti Waziri anakaa, anaanza kuangalia bia, soda, ushuru wa mafuta na wanaangalia labda ni kukata kodi kwenye mishahara ya wafanyakazi, wanaangalia kwamba vile vyanzo ambavyo tunaainisha miaka yote hapa Bungeni kwa nini havifanyiwi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa ni bajeti yangu ya nane na kila mwaka Wabunge tumeainisha mambo mengi sana ya msingi, hapa Bungeni, lakini inavyokuja bajeti tunaona havipo. Ukienda kwenye kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa kinasema kwamba kiwango cha ukuaji wa sekta ya mifugo kilikua kwa asilimia 3.1 mwaka 2012 ukilinganisha na asilimia 3.9 mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tujiulize hapa mifugo tuliyonayo Tanzania, leo badala pato la Taifa kwa upande wa mifugo lipande linazidi kushuka. Kwenye Sekta ya Mifugo tu, Serikali haijaweza kuwa na mpango makini na mkakati wa kutumia Sekta ya Mifugo kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mifugo tu masoko ya uhakika Tanzania hakuna. Hapo hapo Viwanda vya Ngozi karibu vyote vimekufa na juhudi hatuzioni za kuweza kufufua viwanda hivi. Kwenye Sekta ya Mifugo, maziwa yananunuliwa Tanzania kwa bei chee, ya kumwaga, yanapelekwa Kenya, wanakwenda ku-*pack* wana-*export,* wanapata fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mifugo, ng'ombe wananunuliwa Tanzania kutokea hapo Longido, Arusha wanakwenda Kenya wana-*process,* wana *export products* za mifugo inayotoka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais mwaka 2010 amezindua ujenzi wa Machinjio ya kisasa pale Ruvu, leo ni mwaka 2013, machinjio yale yameshindwa kuanza ujenzi kwa sababu mchoro umechelewa, hivi kweli tuko tayari kutumia sekta ya mifugo kuongeza Pato la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna tatizo kubwa, Serikali haiwazi vyanzo vilivyoko kuvitumia. Sekta ya uvuvi kwa miaka mitatu mfululizo imeingiza asilimia 1.4 kwa miaka mitatu mfululizo. Tumekuwa tunashauri hapa miaka yote, sekta ya uvuvi tuna Maziwa, Bahari Kuu, tuna samaki kibao hatuwalishi ngano wala hatuwapi unga, wanajilisha wenyewe, ni kuwalinda na kuwavuna, tumeshindwa kutumia fursa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumeishauri Serikali tangu mwaka 2006, tujenge bandari ya samaki Dar es Salaam, meli zinazotoka huko mbali, zinakuja kuvua, ziweze kujaza mafuta kwenye bandari yetu. Hapo hapo tuweke kitengo cha kuangalia idadi ya samaki waliovuliwa thamani yake ili walipe. Kila siku meli zaidi ya 20 zinakuja kuvua bahari kuu, ni shamba la bibi, wanavuna na kuondoka, halafu tunawakamua Watanzania walipe kodi kwa ajili ya pato la Taifa, hatujaweza kutumia vizuri vyanzo vyetu vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Utalii; Kenya ambao hawana wanyamapori kama Tanzania, hawana vivutio vizuri kama Tanzania, hawana kila kitu kizuri, leo wanaongoza kwa pato lao la Taifa, tumeshindwa kutumia sekta ya utalii Tanzania tuongeze pato la Taifa. Leo hii tumebaki kwenda kwenye bia, soda kwenye ushuru, ni tatizo. Tunaiomba Serikali iainishe vyanzo vya mapato na ivitumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye deni la Taifa. Kwanza nashangaa, nashangaa Wabunge tunakaa hapa Bungeni tunajisifu kwamba tunakopesheka *it is a shame*. Tunasema ni aibu kwa sababu Tanzania ni tajiri wa rasilimali, hakuna nchi ambayo ina neema kama Tanzania, leo

tunashuhudia mali zetu zinakwenda kunufaisha Mataifa ya nje. Sisi tunakwenda kukopa kwa ajili ya shughuli zetu za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafananisha na mfano mwepesi kabisa, una shamba lako lina mahindi mazuri na yamestawi, unaruhusu mtu anakuja kuvuna kwa ajili ya familia yake wewe unakwenda kukopa kwa ajili ya kununua chakula cha familia yako, hiyo ni aibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani deni la Taifa kuendelea kukua kwa asilimia 17, hili ni kubwa sana. Pamoja na kuwa fedha hizi zinakwenda kwenye miradi ya maendeleo tunawabebesha Watanzania mzigo ambao hawakustahili kwa sababu tunavyo vyanzo ambavyo vingeweza kuingiza fedha ya kutosha kwa ajili ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba "Deni la Taifa linahimilika" tena akaendelea kusema kwamba, "Serikali imejipanga na imepiga hatua kubwa sana kufanikisha zoezi la nchi kufanyiwa tathmini ya uwezo wa kukopesheka". Hivi ni sifa kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio sifa kwa sababu Tanzania sio jangwa, ingekuwa ni Namibia ambao sehemu kubwa ni jangwa, tungesema ni kweli, lakini hapa sio jangwa. Tuna misitu, bahari na kila kitu kwa nini tuendelee kuwabebesha Watanzania mzigo kwa jambo ambalo sio la msingi. Naiomba Serikali ije na mikakati ya kupunguza deni la Taifa, tena naliomba Bunge liingilie kati madeni makubwa ya Taifa, lazima Bunge liidhinishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya mapato; nimeona kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, Serikali imeeleza kufanya mapitio ili sheria mbalimbali zinazotoa misamaha ya kodi ziweze kudhibiti au kupunguza misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli nilifikiri bajeti ya mwaka huu ingekuja na punguzo kubwa la misamaha ya kodi ambayo tunayo. Kwa sababu kodi zinafahamika, sikutegemea kwamba ni kwenda kufanyia mapitio tena. Kila mwaka hapa tunazungumza, *CAG* amezungumza, Wabunge wanazungumza, mapitio haya yanachukua muda gani na wakati huo huo tunaendelea kuwabana Watanzania. Tuna tatizo kubwa, lazima Serikali ihakikishe inakwenda *speed,* kuhakikisha kwamba si watu wachache wananufaika na mali za Tanzania kupitia misamaha ya kodi, wakati huo Watanzania wanaendelea kubinywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii inakwenda kuwabinya kweli Watanzania, kwa sababu ukiangalia kila mahali kodi imeongezwa. Wamezungumza wengine, ukishaongeza mafuta, umembinya kwelikweli mwananchi kwa sababu atanyanyasika na utakuwa umeongeza kodi ya nyumba, umeongeza usafiri na umeongeza huduma za afya na kila kitu. Serikali haina mpango makini wa kuweza kuhakikisha kwamba, angalau tunakuwa na fedha za ndani za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya mapitio kwenye kitabu cha Waziri; "Vyanzo vya mapato ya ndani kwa kuangalia ukusanyaji ushuru, mapato katika Serikali za Mitaa, tumeona mwaka 2013 mpaka Aprili, mapato ya Serikali za Mitaa walikusanya asilimia 49 tu kati ya shilingi bilioni 362 zilizotarajiwa, wamekusanya shilingi bilioni 177.4. Tangu mwaka 2009 tumekuwa tunaainisha maeneo yote kwenye mianya ya mapato, kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti ya *CAG* imeeleza vizuri kabisa, kuna watumishi wasiokuwa waaminifu kwenye *Local Government*, kuna vitabu bandia *Local Government*, kuna kutumia Mawakala ambao sio waaminifu, mianya yote, watumishi wengine wanashirikiana na Mabenki kuiba fedha za Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitegemea leo Waziri aseme kwamba, tumeziba mianya hii ya mapato ya

Halmashauri, leo wanakwenda kupitia, *we are not serious*. Ni tatizo kubwa kwa sababu kwa kweli tunahitaji fedha kwa maendeleo, lakini hatuhitaji kubebeshwa mzigo wakati tunavyo vyanzo vya ndani vikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, kwenye mafanikio, Waziri anasema, kuendelea na upembuzi yakinifu katika miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na Liganga. Hivi kweli miaka yote kila siku ni kuendelea na upembuzi yakinifu. Tunayo makaa ya mawe yako ndani ya nchi yetu tena wenzetu wanayatafuta, wanayakosa, sisi tumeendelea kupembua kupembua na kupembua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka yote Serikali haina dhamira na nia ya kweli kuhakikisha kwamba makaa ya mawe yanatumika angalau kwa nishati ya Taifa. Leo umeme haushikiki kwa nishati ya kupikia, gesi haishikiki kupikia, moto poa ndio usiseme kabisa, mafuta ya taa Waziri mwenyewe amesema hapa kodi zinaongezeka, hakuna anayeweza kupikia mafuta ya taa, wananchi karibu wote wanatumia mkaa kwa kiasi kikubwa. Tunaendelea kuwa jangwa kama Taifa, lakini hapo hapo Serikali inaendelea na mchakato kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Magdalena Sakaya, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ajiandae.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja na kumpongeza Waziri na Manaibu wake imara, akinamama mahiri kabisa kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwanza kwa kukopesheka, naipongeza sana. Nasema hivi kwa sababu kuna nchi hazikopesheki, wana kitu kinaitwa

*sanctions,* wamewekewa *sanctions International Monetary Funds*, wamewekewa s*anctions* na *World Bank*. Kwa hiyo, kitendo cha Tanzania kukopesheka maana yake imekidhi vigezo vya Kimataifa na hakuna nchi ambayo haikopesheki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila nchi, kila Serikali zina utaratibu wao wa kuendesha bajeti na wanaweka mikopo ya namna fulani. Kwa hiyo, niipongeze sana Serikali yetu kwa kuaminika na Umoja wa Mataifa na *World Bank* na benki zote za ulimwenguni kiasi kwamba inakopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitazungumzia zaidi walichonituma wananchi. Kule Iringa tunasema “Siasa ni kilimo” na ukisogea pale mkoa wetu mpya wa Njombe “Siasa ni kilimo”, lakini kilimo chetu sisi kinakwenda sanasana na barabara. Sasa wananchi wa Mkoa wa Njombe wanakumbushia barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Njombe una Wilaya zipatazo nne, lakini miundombinu ya kuunganisha Wilaya hizi bado haijakamilika. Barabara ya kutoka Njombe kwenda Ludewa hadi Manda, Njombe/Ludewa hadi Lupingu imekuwa ikizungumziwa muda mrefu sana. Tunaomba *topic* hii sasa tuweke nukta, isiwe kila wakati tunazungumzia jambo hilo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo barabara ya kutoka Njombe – Makete, tunamshukuru Mheshimiwa Rais alitoa maagizo ikatengenezwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, lakini kuna maeneo bado haijakamilika. Pia ni muhimu sana Tanzania tukaweza kuunganisha barabara ya kutoka Wilaya moja hadi nyingine. Barabara inayotoka Wilaya ya Ludewa kwenda Makete bila kupitia Njombe nayo lazima ikamilike tena kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia maendeleo na sisi Mkoa wa Njombe tumekuwa ni mikoa ya mstari ya mbele, tunalisha nchi nzima, tunazalisha sana mahindi. Mahindi yale wafanyabiashara wanaishia Njombe

Mjini kwa sababu kuna lami. Tunaposema tuna soko la Afrika Mashariki wafanyabiashara hawafiki Ludewa na Makete kutokana na miundombinu hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati umefika, wananchi wamenituma, Waziri unatuelewa, tunaomba fedha za barabara ziende haraka na barabara hizi zikamilike. Sisi kule tunazalisha sana, lakini kama mazao hayatakuwa yanatoka kwa haraka kwenda kwenye *common market* ya *East Africa,* bado ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu, tuna miradi ya Mchuchuma na Liganga, miradi ya muda mrefu. Miradi hii inahitaji miundombinu ya uhakika ya kuweza kusafirisha makaa ya mawe yale mazito. Tunaomba sana barabara ya kiwango cha lami. Miradi hii ikifunguka haraka kwa kweli kipato cha Taifa kitakuwa kikubwa yaani maeneo mengine watakuwa wanaenda likizo Mchuchuma na Liganga ikianza kazi, lakini muda mrefu tumeambiwa bado utafiti unaendelea. Tunaomba maeneo hayo yaangaliwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia fedha za barabara ziende, liko suala ambalo naomba tulitazame, suala hili ni kama ifuatavyo. Mara nyingi sana Wizara ya Fedha ikitoa fedha, kwanza inakwenda kwenye Wizara husika, kama ni Tawala za Mikoa, kama ni Miundombinu, baadaye zikitoka Wizara Mama ndio zinakwenda kwenye *agency* husika kama ni *TANROAD* Mkoa au kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi haiwezekani Wizara ya Fedha au Hazina tukatoa fedha Hazina bila kupitia Wizarani, kule Wizarani zikaenda *figures* tu fedha zile zikaenda moja kwa moja kwenye *project* inayotakiwa, maana zinapopita Wizarani zinakuwa na *bank charges*, milolongo ni mingi, *audit query*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni fedha zinatoka Hazina, zinahusiana na mradi wa Mchuchuma na Liganga, basi ni bora, moja kwa moja zikaenda kwenye *respective*

*department,* kuliko ilivyo sasa na huku kwingine ziende *figures,* lakini zenyewe zi-*move* kutoka pointi moja kwenda kwenye *destination*, tupunguze hii milolongo. Kwa hiyo, hilo ni eneo ambalo nitaomba tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo lingine ambalo naomba tuliangalie, ni kwa habari ya kitabu cha hotuba ya Waziri, ukurasa wa mwisho, pale tumechorewa *pie chart* nzuri sana, inaonesha matumizi mbalimbali ya maendeleo, mikopo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza, pamoja na hii *pie chart* nzuri sijaona wapi tuna-*save* fedha za bajeti, kwa mfano tuna miradi ya madini, miradi hii inatuongezea fedha. Lazima tuwe na utamaduni wa ku-*save* wa ku-*invest* bila ya kujali bajeti yetu ina *deficit* kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato haya ya madini tunayotumia leo, kuna watoto wa Tanzania watazaliwa mwaka 2040, yamkini watakuja baadhi ya maeneo kwenye madini watakuta mashimo. Haina maana kwamba sisi tuliozaliwa leo, tuna haki zaidi ya wale. Ile *portion* tuliyoipata lazima tuwekeze, tukishawekeza baadaye *in future* watatumia kwa elimu, *Loans Board* na kadhalika. Kwa hiyo suala la ku-*save* na ku-*invest* ndani na nje ya nchi ili ituletee mapato, ni jambo ambalo halikwepeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana *policy* hiyo tuichukue na wakati Waziri ana-*wind* naomba anielekeze vizuri sana tume-*invest* wapi ndani ya nchi kwenye *Stock Exchange Market,* unakuta nchi ambayo ina *surplus budget* kama Norway kutokana na mafuta, lakini bado wana-*invest*. Kwa hiyo, suala la ku-*invest* ni suala la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda haraka. Niipongeze Serikali kwa kufuta kodi za bajaji, vijana wetu sasa wanapata kufanya ujasiriamali bila kodi za bajaji, lakini niombe tusaidiane kuwaelekeza matumizi bora ya bajaji. Kuna wodi huko vijana wanapata ajali yanaitwa *SunLG*, yaani

huko ni wale wenye matatizo ya pikipiki, huyu amekwenda kavunjika mguu, mwingine mkono. Kwa hiyo tuwaelekeze wavae *helmet* na kadhalika. Hayo ni maeneo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme vijijini. Wilaya ya Ludewa tuna Kata 25, kati ya Kata 25 ni Kata tano tu zenye umeme wa uhakika, napo ni wa kutafuta. *Almost* asilimia 75 ya Wilaya ya Ludewa pamoja na Makete umeme vijijini haujafika. Tumeongeza bajeti shilingi bilioni 186, tugawane sawasawa, kama kila mkoa ni asilimia 30, *no lobbying here*. Mikoa 30 kila mkoa shilingi bilioni 186, wanapata sawa na sio mkoa fulani wanapata zaidi na mikoa mingine wanapata chache, aah! Umeme vijijini tuletewe vizuri kabisa, mkoa wangu una vijiji vingapi, mkoa fulani una vijiji vingapi, yaani ni *proportional,* igawanyike vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake ni wadau muhimu asilimia 51, lakini mpaka leo kuna mabenki wanawake hawa wakienda kukopa au kwenye *SACCOS,* riba inakuwa kubwa. Unakuta mama akienda kukopa anakuwa sawasawa na kampuni, asimilia 16 *interest* ataweza wapi. Naomba Mabenki, *SACCOS*, vikundi vya Wanawake hawa wapewe mikopo ambayo hata ikiwezekana riba yake isiwepo kabisa, maana ukimwezesha mwanamke umewezesha Taifa zima, haina haja ya kuwawekea riba kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano; tunazo kero za Muungano, Waziri wa Muungano. *Joint Finance Commission* iko chini yake, *formula* ipatikane, isipopatikana *formula* ndiyo tunakuja tunataka Serikali tano, sita, saba, tukiamini kuwa hizi Serikali ndizo zitatatua kero za Muungano. Kero za Muungano zinatatuliwa kwa kukaa chini na kuona ni maeneo gani yaboreshwe na siyo kuongeza Serikali. Haya ni maeneo ambayo tunaomba myaangalie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba muda mrefu, *formula* ya Muungano, mgao wa Zanzibar shilingi ngapi uende? Hatuhitaji muda mrefu, huwa tunakaa tu wataalam mtuite, wengine tuta-*volunteer,* Madaktari tupo, tutaleta

*formula* imara. Sasa mnavyochelewesha ndio Watanzania wanakuja na kutaka Serikali tatu, Serikali nne, Serikali sita, hizo ndizo zitaongeza kero, *struggle for resources,* maana yake tutakuwa na Marais watatu, Mawaziri Wakuu watatu, wanne, Mabaraza na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana.

Nimeletewa swali hapa, nimeulizwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bunge, kwani una taarifa zozote rasmi kuwa, huyo Mheshimiwa Kafulila ndiyo Kaimu Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na huyo mwenzake Mheshimiwa Rashid, Mbunge wa *CUF* ndiye Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni? Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba utupe maelezo na Mwongozo wako.

Nadhani hawa wanataka ku-*refer* yale mambo yanayofanyika kwenye hivyo viti huwezi kujua. Kwa hiyo, nafikiri labda tuache tu warithi yale ambayo yako kwenye maeneo hayo, lakini sina taarifa zozote hapa mezani kwangu kuwa leo Kafulila ndiyo Kaimu Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, wala sina taarifa rasmi kama Mheshimiwa Rashid leo ndiyo Mnadhimu wa Kambi ya Upinzani Bungeni. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, nadhani tuwaache tu warithi hayo wanayotaka kuyarithi, sisi tuendelee na Mkutano wetu. Mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Rita Kabati.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, Katibu

Mkuu, Makamishna wa Bajeti na Maafisa wote wa Wizara hii nyeti ambao ndiyo kitovu kikuu cha uchumi wa nchi yetu na hongereni sana kwa kazi nzuri mnayoifanya ya ku-*manage* uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niipongeze Benki Kuu na Wataalam wote, Wachumi ambao wamefanya kazi nzuri sana ya kudhibiti mfumuko wa bei wamefanya kazi nzuri. Naomba waendelee, naamini kabisa kuwa watakuwa wamepata uzoefu zaidi. Kwa hiyo, nawatakia kila la heri, tuendelee kudhibiti mfumuko wa bei wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachumi wanatueleza kuwa Sera, Mipango, Bajeti vinaenda pamoja na wote sisi tunafahamu Sera ni matamko ya maandishi ya makusudi yenye lengo la kufanikisha malengo ya kusaidia ustawi wa wananchi wetu. Sasa kama tunatengeneza bajeti au tunatengeneza mpango kutokana na Sera, lazima katika utekelezaji wake tufuate msingi wa Sera na mipango yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu kule Namtumbo katika miradi yetu ya maendeleo Serikali ilitusaidia, tuliomba kuwa tujengewe hospitali ya Wilaya na Serikali ilitusaidia kwa awamu ya kwanza kutupa milioni 400 za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na awamu ile ya kwanza tumeikamilisha vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali ikaanza kutupa milioni 150 kila mwaka na tunachoweza kuomba ni kwamba, gharama za ujenzi wa Hospitali ile ya Wilaya ni zaidi ya bilioni mbili. Tukiwa tunapewa milioni 150 kwa mwaka itachukua muda mrefu sana kufikia lile lengo. Kwa hiyo tunaomba sana angalau mtupe milioni 300 kwa mwaka ili tuweze kutimiza lile lengo letu mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachosikitisha pia mwaka huu bajeti hii ya 2013/2014 tumekatwa 50% ya mgao huo. Tunawaomba Serikali itufikirie ili tukamilishe mapema ujenzi wa hospitali ya Wilaya. *Phase one* imekamilika, tunaanza kutoa huduma hivyo hivyo kwa ugumu, tunaomba

Serikali pia itupatie *ambulance* (gari la wagonjwa) ili tuweze kufanya kazi yetu vizuri ya kuwahudumia wananchi wetu katika sekta hii ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu; katika bajeti ya maendeleo ya Halmashauri yetu tulikuwa tupate milioni 500, tulitenga kwa ajili ya ujenzi wa majengo, milioni 300 madarasa 25 na ujenzi wa hosteli ya wanafunzi katika shule yetu ya sekondari ya Magazine iliyoko mbali mpakani na Msumbiji. Lakini tunasikitika sana zimekatwa milioni 300, tumebakiziwa milioni 200. Hizi milioni 300 tulikuwa tunataka kujenga madarasa 25 kwa sababu tuna shule wanafunzi wanasoma kwenye madarasa ya manyasi mpaka leo, kwenye magazeti huwa mnaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo tumetenga hizi milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 25, tumepunziwa. Tunawaomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI muangalie jinsi ya kuzirudisha hizi fedha. Leo hii tunawashukuru kwa kutupatia milioni 500 kujenga nyumba za Walimu, lakini wale Walimu tukishajenga zile nyumba watakwenda kufundisha kwenye madarasa ya nyasi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana hizi milioni 300 mturudishie. Tunawashukuru kwa kutupa milioni 500 za kujenga nyumba za Walimu, lakini ni lazima tujenge haya madarasa. Lakini kwenye hizi tulikuwa tunataka kuzungumzia mabweni ya shule ya sekondari Magazine ambazo zilikuwepo katika hizi milioni 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hii ya sekondari iko katika Kata ambayo inahudumia vijiji ambavyo kimoja kiko kilomita 30 Kijiji cha Amani, lakini kijiji kingine Lingusanguse kiko kilomita 55, tuna-*drop out* au tuna mdondoko wa wanafunzi 19 wasichana ambapo pale hakuna hosteli, kwa hiyo, wameshindwa kukaa kwa sababu wanatakiwa wapangishiwe nyumba. Sasa vijijini utapangisha nyumba ya nani? Kwa hiyo tunaomba sana hizi milioni 300 turudishiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia naomba kusema kwamba, Serikali ilikuwa inatakiwa iturudishie fidia ya vyanzo vya mapato; sisi tulikuwa tunatakiwa turudishiwe milioni 238 Halmashgauri ya Wilaya ya Namtumbo, lakini tumekuwa tunarudishiwa 144.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya mwaka jana tuliambiwa kuwa itakuwa vile vile kama mwaka juzi na mwaka huu tumeambiwa itakuwa vile vile na sasa hivi tuna *deficit* ya milioni 94. Mwaka huu tumeambiwa *ceiling* ya bajeti yetu iwe kama ya mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea kuwa na *deficit,* lakini hapo hapo tumeongeza posho za Waheshimiwa Madiwani kutoka 120,000 kwa mwezi mpaka 250,000, Bunge hili liliidhinisha. Fedha hizi hazitoshi tutawalipaje posho hawa Madiwani pia? Tunaomba pesa ya fidia ya vyanzo vya mapato tuweze kuipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo Namtumbo, naomba nizungumzie pia suala la pikipiki na tozo hii iliyofutwa ya *Road License*. Unajua wengine wameweza kufikiria kana kwamba imefutwa kodi yote mpaka ya *import duty,* nilivyomwelewa Waziri ni kwamba, imefutwa kodi ya *Road License* ili kutia motosha katika eneo hili lenye nguvu kazi kubwa sana ya vijana ambao hawana kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguvu kazi ya Taifa inayoweza kufanya kazi ni milioni 23, lakini Serikali ajira zake imeajiri watu laki sita na tisini elfu tu, sawa na 3% ya milioni 23, lakini sekta rasmi ambayo ni sekta binafsi imeajiri watu milioni moja, laki moja na hamsini sawa na 5%, lakini sekta hii isiyo rasmi, ndiyo waendesha pikipiki, mama lishe, wajasiriamali wadogo, inaajiri watu milioni sita na laki tisa wakiwepo hawa waendesha pikipiki ambao ni 30%, tuna 15% *un employment,* milioni tatu na laki nne na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo eneo hili naipongeza sana Serikali kwa kuwa ni lazima tuipe motisha kwa kutoa hii tozo ili tuajiri vijana wengi na kuwa *temporary*

*solution* wakati Serikali inaandaa *long term solution* ya kuhakikisha kwamba, kutakuwa na ajira kwenye viwanda na wawekezaji wakubwa. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusiana na *cash crops* zetu. Katika hizi *cash crops* zetu wenzangu wengine wamesema, ni lazima tuweke viwanda vya kuongeza thamani ni kweli. Katika sekta ya tumbaku kulikuwa na Sheria kuwa huwezi ku-*export* jani la tumbaku lazima liwe limekuwa *semi processed.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna viwanda vya tumbaku ambavyo hapa vinatengeneza tumbaku ile inayokwenda kuzalishwa sigara na 90% inauzwa nje, sasa inaongezwa thamani, leo hii tumetoka kwenye mauzo ya milioni 124 mpaka msimu huu tumeuza milioni 350 *US* Dollars, kwa sababu zimeongezewa thamani. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa, lazima Viwanda vya Korosho viwepo na lazima Viwanda vya Pamba viwepo. Lakini katika eneo hili pia hizi *Crop Boards* zimekuwa mzigo kwa Serikali, Serikali ilisema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Jimbo la Namtumbo. Sasa nitamwita Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Josephat Kandege ajiandae.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi na nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kupata nafasi ya kuchangia jioni ya leo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, samahani ilikuwa aanze Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, sasa nimemruka kwa sababu hayupo, Mheshimiwa Ritta endelea.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza mchango wangu kwanza nichukue nafasi hii kupongeza ushindi mkubwa wa Chama cha Mapinduzi katika Kata zetu na niwapongeze wale wote waliosababisha ushindi huu ukiwepo wewe Mwenyekiti pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu pia nimpongeze Waziri wa Fedha, Manaibu wa Wizara hiyo pamoja na Watendaji wote ambao wameweza kuwasilisha bajeti katika Bunge letu. Vile vile niendelee kupongeza Bunge letu ambalo limeweza kubadilisha mfumo wa kujadili bajeti hii. Huu mfumo umetusaidia kwa sababu tumeweza kuijadili bajeti kabla ya kuwasilishwa na baada ya uwasilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niipongeze Serikali kwa kuzingatia michango ya Wabunge wengi na kuweza kuongeza fedha katika baadhi ya Wizara. Ningeiomba sasa Serikali tumeona Wizara nyingi sana zimekuwa zikicheleweshewa pesa ambazo tumekuwa tukizipitisha hapa Bungeni na kusababisha ucheleweshaji wa miradi mingi sana.

Sasa naomba sasa hivi kwa sababu kwanza kabisa bajeti hii tumeipitisha kwa muda muafaka, kwa hiyo zile pesa ambazo tunakuwa tukizipitisha zifike 100% ili kusiwepo na matatizo katika utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa sababu ukichukua tu mfano wa Wizara ambazo zinapata 100%, kunakuwa na tofauti kubwa sana. Kwa mfano, Wizara ya Ujenzi imekuwa ikifanya kazi zake vizuri kwa sababu imekuwa ikipatiwa fedha zake 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu ndiyo maana nataka kuweka mfano, ukichukua Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Sayansi utakuta kuwa miradi yake mingi inachelewa kwa sababu pesa hawapati 100% ambazo wameziomba. Utaona pesa ya

mwaka jana Wizara ya Sayansi na Teknolojia wamepatiwa 65% tu mpaka sasa hivi tunaanza bajeti hii ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeiomba Serikali izingatie sana, kuwepo uwiano kwa Wizara zote ili ziweze kufanya mipango yao kama inavyotakiwa. Ukija katika Halmashauri zetu pia kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa sana wa pesa ya maendeleo, lakini nina imani sasa hivi kutokana na mfumo huu pesa hizi hazitacheleweshwa tena na ningependa kupata ufafanuzi kuwa vigezo gani vinatumika kugawanya hizi fedha katika Halmashauri zetu, nichukue mfano wa Jimbo langu la Iringa Mjini. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Nampa taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8), Mbunge wa Iringa Mjini anaitwa Mchungaji Peter Msigwa, taarifa ni hiyo tu kama hajui. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati taarifa hiyo.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake ni ya uongo kwa sababu mimi ni Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa mzima na naingia katika Halmashauri ya Iringa Mjini. Kwa hiyo, hii taarifa ni ya uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Iringa Mjini lina changamoto nyingi sana lina matatizo makubwa sana ambayo tusipoyasemea wananchi wa Iringa Mjini wataendelea kutuhukumu miaka hadi miaka. Nikitolea mfano, kuna miradi ambayo haitekelezeki, pesa haiji kwa wakati au hailetwi kabisa. Kwanza kabisa kuna mradi wa daraja la Tagamenga katika Kata ya Ruaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja hili uchambuzi yakinifu unaonesha kuwa, inatakiwa kama 1.1 bilioni, lakini Halmashauri hii haina uwezo kabisa wa kujenga hili daraja. Daraja hili limekuwa likileta maafa kila mwaka, kwa hiyo,

ningeomba Serikali miradi kama hii ingeiangalia kwa kuwa ni tatizo kubwa sana katika Mkoa wetu wa Iringa na Jimbo la Iringa Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi mingine ambayo haitekelezeki katika Jimbo hili. Kuna miradi ya umwagiliaji ambayo nimekuwa nikisemea sana kila mwaka kwamba, hii miradi kila mwaka tumekuwa tukiiombea fedha, lakini hazifiki kwa wakati. Upo mradi wa Kitwilu *Irrigation Scheme* ambao unahitaji kama milioni 526 na uko mradi mwingine wa Mkoga *Irrigation,* mradi huo unahitaji kama shilingi milioni 556.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi hii tayari kuna nguvu ya wananchi, pia kuna nguvu ya Halmashauri ambayo imekuwa ikitumika, inakuwa haikamiliki kwa wakati. Kwa hiyo, ningeomba Serikali ingeangalia miradi angalau kuwe na uwiano wa ugawaji wa hizi pesa katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mradi mwingine wa hospitali, Mkoa wetu wa Iringa tuna hospitali ya Mkoa. Hospitali hii imekuwa na msongamano mkubwa sana wa wagonjwa, hospitali hii imekuwa na ukosefu mkubwa sana wa watalaam yaani Madaktari Bingwa. Nimshukuru sana Mheshimiwa Mwanri, nilikuwa nasema sana kuwa tufungue hospitali ya Wilaya katika Halmashauri yetu, kweli alikuja tukaweza kupata hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna tatizo kubwa katika hiyo hospitali ya Wilaya. Hospitali ya Wilaya toka imefunguliwa sasa hivi ina karibu mwaka mmoja na nusu, hakuna mgawo wa madawa inayopata, hospitali hii bado haijasajiliwa, hatujapata vifaa tiba, hospitali hii haina gari la wagonjwa, jengo la *maternity* tayari limekwishakamilika lakini hakuna vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tungeomba hospitali hii tupatiwe vifaa ili tuweze kupunguza msongamano ambao uko katika hospitali ya rufaa kwa sababu wagonjwa wamekuwa wakipata matatizo makubwa sana. Wakienda

katika hospitali ya rufaa wanaambiwa warudi katika hospitali ya Wilaya ambayo haipatiwi mgao. Mpaka sasa hospitali ile bado inapatiwa mgao kama kituo cha afya ama zahanati wakati ina wagonjwa wengi sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali jambo hili ilizingatie sana ili tuweze kusaidia wananchi wa Iringa wasiweze kupata matatizo katika hospitali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali kwa ajili ya kutenga pesa kwa ajili ya Benki ya Wanawake. Benki hii ya Wanawake bilioni mbili zimeongezeka, lakini sasa tunaomba iweze kufika mpaka vijijini na mpaka Mkoani kwetu Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki hii wanawake wengi wamekuwa wakitupa maswali makubwa sana tunapokwenda kwenye vikundi vyao, kwamba imekuwa kama Benki ya Wanawake wa Dar es Salaam. Sasa ifike sehemu Serikali ijaribu kufikisha huduma hata pembezoni, kwa mfano, katika Mkoa wetu wa Iringa na vijiji vyake ili iweze kuwasaidia wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kuna udhalilishaji mkubwa sana wa akinamama kwenda kukopa kwenye hizi taasisi ambazo zinawakopesha kwa riba kubwa sana kama *PRIDE, TUNAKOPESHA, FINCA,* hizi benki zimesababisha hata ndoa nyingi za wanawake wa Iringa kuanguka kabisa, kwa sababu wamekuwa wakipokonywa vitu, ile riba watu wanashindwa kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Hazina au Wizara ya Fedha iangalie hizi benki ambazo zinatoa riba kubwa sana hasa katika vikundi hivi vya wanawake. Tumeona kwamba hizi taasisi zimekuwa zikikopesha hata Walimu na watu wengi sana ambao wanashindwa mikopo hii inakuwa haikopesheki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali kwa kutenga bilioni tisa katika Mfuko wa Vijana. Hizi pesa bilioni tisa, tunaomba tuwekewe kabisa mkakati wa jinsi ya kuzigawa kwenye Halmashauri zetu, kwa sababu tumeona hizi pesa zinaweza kuwasaidia vijana sasa kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Serikali sasa hivi imeondoa kodi katika leseni za bodaboda, tuna imani pengine hii mikopo au hizi pesa ambazo zitakuja kwenye Halmashauri zetu, vijana wengi sasa wanaweza wakafanya biashara wao wenyewe. Kwa sababu tumeona vijana wengi wanaendesha zile bodaboda lakini unaona walio ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ritta Kabati. Ili kuweka kumbukumbu za majadiliano vizuri, Mheshimiwa Ritta Kabati ni Mbunge wa Viti Maalum, lakini anahudumia ndani ya Halmashauri iliyomo kwenye Jimbo la Iringa Mjini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na mchangiaji anayefuata, nilisema namwita Mheshimiwa Josephat Kandege na Mheshimiwa Rashid Abdallah ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti kwa jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kupongeza wale wote waliofanikisha utaratibu wa mzunguko huu wa bajeti kufanikiwa, walioshiriki ni wengi, nawapongeza wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja na nina sababu za kuunga mkono hoja. Sababu ya kuunga mkono hoja ni kwa sababu sasa nina uhakika umeme utafika Kalambo kwa maana ya Vijiji vya Matai, Mbuza, Mkoe, Kisumba hadi Kasanga, lakini siyo huko tu, umeme sasa utafika Mwazye, utafika Ninga, Mwimbi hadi Ulumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ya pili ni uhakika juu ya kupatikana kwa maji. Maji yatafika Kisumba, maji yatafika Mwazye, Ulumi, Kafukula, Kamawe, Katete, Miunga pamoja Mambwekenya. Kwa hiyo nina kila sababu ya kupongeza na kuunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kuchangia katika baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza ni kuhusiana na wingi wa vipaumbele, Waheshimiwa wengi wamesema. Ni ukweli usiopingika kwamba kupanga ni kuchagua, haiwezekani tukasema vyote vikawa vipaumbele na tukatekeleza vyote haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza tungejikita zaidi katika ujenzi wa miundombinu kwa maana ya reli na bandari. Reli si maana yake reli ya kati peke yake, reli ni pamoja na kuhakikisha kwamba fursa ya uwepo wa *TAZARA* tunaitumia, kwa kuhakikisha kwamba inafika Kasanga, inafika Mpanda na inaunganisha kwenda mpaka Kigoma kwa ndugu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo naona ingekuwa kipaumbele cha kututoa haraka ni katika suala zima la kilimo. Asilimia 75 ya Watanzania wako vijijini na hawa ni wakulima. Maana yake unapowekeza kwa wakulima, tafsiri ya uchumi unaposema unakua na unapotaka kutoa matunda ya haraka ni kwa kuwekeza kwa Wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ihakikishe kwamba kilimo chetu kinakuwa na tija. Mtu avutiwe kwenda kwenye shughuli ya kilimo, isionekane kama vile kwenda kulima ni kama dhambi. Kwa hiyo, naomba tafsiri hii iwekwe kwenye bajeti, kiasi kilichowekwa kwa kuanzia siyo kibaya lakini hakitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, imekuwa ikiongelewa muda mrefu benki ya wakulima, benki hii isije

ikawa hadithi. Tunaomba mikakati ya dhahiri ili kuhakikisha kwamba benki ya wakulima inaanzishwa na iwe na mtaji wa kutosha. Kwa sababu kuanzisha benki ni jambo moja na kuipa benki mtaji mkubwa ni jambo la pili. Kwa hiyo, naomba Serikali ihakikishe kwamba kilimo kwa maana ya uanzishwaji wa Benki ya Wakulima unakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo ingependeza ni kwamba tungejikita na kuhakikisha kwamba tuna uhakika wa umeme, umeme ni maendeleo. Katika hili naomba niwasihi ndugu zetu wanaotoka Mtwara, Tanzania hii ni ya kwetu, umeme ni wa Watanzania. Gharama ambayo Serikali inabeba kwa ajili ya kukodisha mitambo kila Mtanzania anabeba mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama tunapata chanzo ambacho kinakwenda kuwasaidia Watanzania kwa ajili ya kuharakisha maendeleo, hebu tusianze kupigana wenyewe kwa wenyewe, hii ni neema ambayo tunapaswa tuitumie kwa ajili ya kuendeleza Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye matumizi ya Serikali, matumizi ya Serikali yamekuwa yakiongelewa na nimekuwa napata taabu sana pale ambapo Kiongozi Mkuu wa shughuli za Serikali Bungeni anaposema kuanzia sasa hivi yeye atatumia gari ambayo haitazidi *CC* 3000, lakini wengine wanakwenda kununua gari ambazo zinazidi *CC* 3000, nashindwa kuelewa jeuri hiyo wanaipata wapi? Kama kiongozi anaonesha kwamba tunataka kubana matumizi kwa kuondokana na gari za anasa, wao hiyo jeuri inatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe kwamba, Waziri Mkuu anaposema naenda kuanza kutumia gari hiyo na wengine wote hupaswi kupigiwa mbiu, hiyo ni *automatic* unapaswa ufuate, huo ndiyo unapaswa uwe msimamo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kumekuwa na gharama kubwa sana za ununuzi wa magari, lakini kwa utaratibu mzima kwamba kila Wizara inanunua gari

kwa wakati wake, itoshe sasa na ifike mahali ambapo Serikali inaponunua magari inunue kwa ujumla wake. Wapate *requirement* ya kila Wizara na wanunue *direct* kutoka kwa watengenezaji wa magari, ndiyo namna pekee ambayo Serikali inaweza ikapunguza matumizi ya magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama katika bajeti, inaonesha kwamba mishahara inabeba trilioni 4.2 ambayo kwa asilimia katika bajeti ya trilioni 18.2 ni asilimia 23, ndiyo mishahara. Lakini unashangaa Watanzania hawa, Walimu, Manesi, hawa ndiyo wanaolipwa mshahara mdogo, sasa huo mshahara mkubwa anayelipwa ni nani mpaka asilimia 23 ya pato lote iende kwenye mishahara? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ana wajibu na kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba hiyo mishahara mikubwa mpaka inafikia asilimia 23 inabebwa na nani kama Watanzania walioajiriwa wanasema wanalipwa kipato kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningetaka kuongelea ni namna ambavyo inaonekana katika upande wa kulipa deni la Taifa. Kukopa siyo dhambi nimekuwa nikisema siku zote, dhambi ni kwamba hicho ulichokopa unakwenda kukifanyia nini? Nasumbuliwa na namna ambavyo pale tunapokwenda kukopa tunakwenda kutumia kwenye shughuli za maendeleo, lakini tunapolipa inaonekana kwamba tunatumia pesa ambayo siyo ya maendeleo. Tafsiri yake nashindwa kuelewa, watalaam mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile pesa ambayo tunakwenda kulipa ambayo tulikopa tukafanyia shughuli za maendeleo, kwa nini inaonekana kama vile ni *recurrent expenditure*. Mtafute namna ya kuiripoti na watu wamekuwa wakipotosha sana. Inaonekana kama vile Serikali pesa yake ni matumizi ya kawaida ya anasa. Sasa mimi nimekopa nikaenda kujenga barabara, leo nikilipa naonekana nafanya anasa, hesabu hii siielewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwafuata *TRA* wanakwambia wanakusanya vizuri kweli, lakini takwimu

zinaonesha kwamba kwa mwaka ongezeko ni 0.075, halafu wao wanasema wanavuka malengo? Unavukaje lengo kama ongezeko ni 0.075, hii haikubaliki! Ndiyo maana unakuta katika vyanzo ambavyo wanavyo vya uhakika ni *pay as you earn*, kwa sababu wana uhakika hiyo itaenda tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, hiki kiasi kilichopunguzwa kutoka asilimia 14 iwe nafuu kwa mfanyakazi iongezwe iende mpaka asilimia tatu, halafu *TRA* waende kukusanya pesa, siyo kukaa ofisini ukawa na uhakika wa kuletewa pesa kutoka kwenye *payroll* ukasema unafanya kazi, hii haikubaliki! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa maduhuli, asilimia 55.5 na sisi tunasema nchi hii tunataka tuondoke kwenye kipato cha umaskini kwenda kwenye kipato cha kati, kwa *speed* hii hatuwezi kufika. Ni lazima tukubaliane kwamba utendaji ambao tumekuwa tukifanya haukubaliki, ni lazima tufanye mapinduzi kuhakikisha maduhuli yanakusanywa na yakatumike ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla muda haujakwisha nisemee juu ya *East African* na jinsi ambavyo wenzetu wanaitumia zaidi kiuchumi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Kengele ya kwanza au ya pili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni kengele ya pili.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge sasa namwita Mheshimiwa Rashid Abdallah.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha jioni hii kusimama hapa, lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuwapongeza kwa dhati kabisa wanachama wote wa *CUF* wa Chambani na wananchi kwa ushindi mkubwa wa kishindo wa Chama cha *CUF*, lakini pia kuwashinda CCM na washirika wake. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitachangia kuhusu mpango wa maendeleo ya Taifa, lakini pia nitagusia deni la Taifa na matumizi ya Serikali. Wahenga wanasema, ili ujue unakokwenda ni vizuri ujue unakotoka. Nimeamua kusema hili kabla ya kujadili mpango uliopo sasa ili niangalie mipango iliyopita ilifanya nini katika masuala mazima ya uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya Taifa hili ilikuja na mpango wa muda mfupi wa miaka mitatu kutoka mwaka 1961 hadi 1964 na shabaha kubwa ya mpango huu ilikuwa ni kuondoa umaskini, ujinga na maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutekeleza haya, Serikali ikaja na mpango wa muda mrefu kutoka mwaka 1964 hadi mwaka 1980. Mpango huu ulifanikiwa awamu mbili lakini ukashindwa awamu ile ya tatu. Sababu kubwa ni ukame na njaa iliyokithiri, lakini pia ni kupanda kwa bei za mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine ilikuja kutoka mwaka 1980 hadi mwaka 2000, mpango huu haukufanikiwa hata kidogo, sababu ilikuwa ni kudorora kwa uchumi na ukame. Ikaja *program* ya muda mfupi ya *National Economic Survival Program (NESP)* mwaka 1981/1982 na ikaunganishwa na *Structural Adjustment Programme (SAP)* mwaka 1982 na mwaka 1985. *Program* hizi hazikufanya vizuri hata kidogo, sababu ni kukosa rasilimali na wadau kutilia shaka program hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1986 mpaka mwaka 1989 ilikuja *program* ya *Economic Recovery Programme* (ERPI) na mwaka 1989/1992 ikaja *program* hiyo hiyo ya ERPI II. *Program* hizi hazikufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna dira ya mwaka 2025 na dira hii kila mwaka inaleta marekebisho yake ya kiuchumi. Hapa ukiangalia *program* zote zilizopita za maendeleo, tatizo kubwa lilikuwa ni ukame na njaa na kupanda kwa mafuta. Nilipoangalia program hii ya Waziri, Mheshimiwa Wassira haikutoa jibu kuhusiana na ukame na njaa, iligusia kidogo tu kilimo na ikaenda *irrigation* kidogo, lakini haikutoa jibu hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupanda kwa mafuta, tumeona Wizara ya Fedha imepandisha mafuta na ni sababu kubwa iliyofanya *program* zote hizi kufeli, lakini leo tunapandisha sisi wenyewe mafuta. Nashauri kwamba, ongezeko hili la mafuta liondolewe, *petrol* pamoja na *diesel*. Lakini pia mpango huu uangalie zaidi kilimo cha umwagiliaji, kama hatukuangalia hili vizuri basi hali ya uchumi inaweza ikaathirika kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye matumizi ya Serikali, siku nyingi Serikali ilikuwa inaahidi kupunguza matumizi ambayo siyo ya lazima, lakini jambo hili linafanywa kinyemela na kwa usiri mkubwa sana. Nasema hivi kwa sababu, ukiangalia mafungu kwa ujumla ya warsha, mwaka jana ilikuwa ni bilioni 66, lakini mwaka huu ni bilioni 79, kuna ongezeko la bilioni 13, haya ni matumizi ya warsha tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vinywaji na viburudisho, mwaka jana ilikuwa bilioni 19, lakini mwaka huu ni bilioni 24, ni ongezeko la bilioni tano. Ofisi pamoja na watu wengine wanakaa ofisini, wanakula na kunywa, tumeongeza bilioni tano. Wangeweka fedha angalau akitokea mgeni wamfariji, wewe unatoka nyumbani unakunywa chai, ili hizi fedha zikaenda kwenye shughuli za maendeleo, afya pamoja na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuta, mwaka jana ilikuwa bilioni 66, lakini mwaka huu yamepanda bilioni 70 na kwa hiyo, kuna bilioni nne zimeongezeka, ni sawa na asilimia sita. Kuhusu safari pia zimeongezeka, mwaka jana ilikuwa bilioni 147, lakini mwaka huu ni bilioni 163, ni ongezeko la bilioni 16, ni ongezeko la asilimia 12. Bado haya ni matumizi ya kawaida, fedha nyingi zinatumika katika matumizi ya kawaida. Kwa hiyo, bajeti bado na Waziri bado hajaamua kupunguza matumizi ambayo siyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu deni la Taifa, hapa kuna ripoti ambazo zinatukanganya, kuna ripoti ya Wizara ya Fedha imeweka deni la Taifa, lakini pia kuna ripoti ya Kambi ya Upinzani. Nataka Waziri anieleze na atoe ufafanuzi kama, deni la Taifa halikujumuisha madeni yale ya *ATCL, PSPF* na Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atakapokuja atueleze deni la Taifa kuhusiana na mashirika haya, kwa mfano, Mashirika kama Shirika la Ndege la South Africa na *Citibank* ni bilioni 8.8, inasemekana kwamba fedha hizi hazikujumuishwa katika deni la Taifa kwa sababu Serikali tayari walichukua dhamana na kukubali kulipa fedha hizi. Kwa hiyo, watueleze, hizi fedha zote ni kweli hazikujumuishwa katika deni la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana kwamba deni la Taifa linazidi trilioni 22, Waziri akija atupe ufafanuzi na siyo tu ufafanuzi kwa Wabunge, lakini kwa wananchi ambao wanasikiliza bajeti hii ili kuweza kutoa elimu kwa ufupi, kwa sababu sasa tunachanganywa, wengine wanasema deni halikuingizwa mwingine anasema madeni yameingizwa, tunaomba tupate usahihi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamesema kwamba, Taifa likope na linakopesheka, lakini wamesahau kwamba kuna riba inaongezeka kila mwaka, riba hii wanaolipa ni wananchi, kuna deni lile la kawaida na kuna riba. Kwa hivyo, hizi riba naona tuziangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana, unapokopa uangalie ni riba kiasi gani, siyo unakwenda kukopa tu, maana yake tunashindwa, tunalipa deni lenyewe halafu baadaye tunakuja kulipa riba tena. Kwa hiyo, itakuwa tunalipa mara mbili zaidi *(double payment)* na hivyo kubebesha mzigo wananchi. Kwa sababu leo wewe unatia sahihi unaondoka, wale waliopo watakuja kushindwa kulipa deni hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkapa, alipoandaa program zake zile za kuondoa umaskini, nakusudia *HIPC,* alisamehewa madeni sana na Mataifa mbalimbali. Ile iliwezesha Rais aliyekuja akawa na nguvu ya kuendesha Taifa hili. Kwa hiyo, panapokopwa, siyo kwamba tunakopa tu, lakini uangalie na riba kwa sababu riba inatafuna Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Rashid Abdallah kwa mchango wako. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Profesa Peter Msolla ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, nilikuwa katika matibabu na nimerudi salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru na nimpongeze sana Waziri wa Fedha na Manaibu wake. Umri siyo sababu ya kutokufanya maendeleo, Mahadhir Mohamed wa Malaysia alikuwa na umri wa miaka 73. Alileta mabadiliko makubwa ya maendeleo kwa muda wa miaka 20 kutoka dunia ya tatu ikawa katika dunia ya kwanza, lakini alikuwa na washauri wazuri ambao walikuwa wanamshauri katika maendeleo yale. Walikuwa wanamshauri katika

uchumi, kilimo na sekta zote, iwe viwanda, biashara na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunasema katika *big and fast result now,* tuna-*import* kibiriti nje, tunaleta mafuta ya kula kutoka nje, tunanunua kanga mbovu na vitenge vibovu kutoka nje, tunaleta mchele mbovu kutoka nje, wakati tuna mchele wa Kyela ambao tungeuendeleza tungelisha nchi nzima na tusingetegemea kuagiza mchele kutoka nje na kutumia pesa nyingi na tukaacha mazao ya watu wa ndani yasitumike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hali sijamkubalia Mheshimiwa Waziri kama kweli ana washauri wazuri wa uchumi na maendeleo, wenye mipango bora ambao wataweza kumfikisha katika *big and fast results now. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ni muda wa Mheshimiwa Waziri kukaa na timu itakayomsaidia, *business as usual* hakuna tena tunataka *business unusual.* Leo inasikitisha ufuta unalimwa Lindi, tunaagiziwa mafuta *Korie* nje kwa sababu zipi za msingi? Kiwanda cha Mafuta cha Nachingwea kimefungwa na aliyesema anawekeza amekifunga karibu miaka 20 hakifanyi kazi. Leo tunaagizia mafuta *Korie* nje wakati tuna uwezo wa kuzalisha mafuta alizeti, mawese kutoka Kigoma na mafuta ya karanga kutoka Tanzania. Hii ni aibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, akae tena na timu yake awaambie kama hawawezi kuleta maendeleo katika *big and fast results* aachane nao, atafute watu wengine na timu nyingine imsaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nizungumzie neno la *SAGCOT. SAGCOT* maana yake ni *Southern Agricultural Corridor of Tanzania.* Hapa nisije nikapewa mwongozo, nataka wao wanipe taarifa, badala ya kunipa mwongozo. Maana ya kutaja *Southern Region* Lindi, Mtwara na Ruvuma katika *SAGCOT* haipo, nataka taarifa hii niipate badala ya kunipa mwongozo, nataka wanielezee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SAGCOT* ni maendeleo ya kilimo na zimetengwa fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo ya kilimo katika Mikoa ya Kusini, lakini Lindi, Mtwara, Ruvuma hamna. Tutafutieni sisi tuko kanda gani? Tuko Kusini, Kaskazini au Magharibi tutajijua katika *SAGCOT*, kama si hivyo hapatoshi hapa. Tunataka SAGCOT Mikoa hii iingie, isije ikawa kero kwa Taifa. Imani yangu Waziri ananisikia ambaye ni Waziri wa Fedha na wa Mipango, naomba Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma iingie katika *SAGCOT* isije ikawa maudhi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *definition* ya *South* inaonekana ni kama Lindi, Mtwara na Ruvuma, *SAGCOT* inakwenda kuingia Morogoro na Dar es Salaam, wakati tuna bandari ya Mtwara ambayo ingefanya kazi katika Mikoa ya Kusini, haimo. Hii ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana kuna wataalam wameamua kwa makusudi kuhakikisha Mikoa ya Kusini haiendi na wala haitoki halafu baadaye iwe kero, hatutaki hili. Tunaomba Waziri kwa hekima na taadhima alisimamie hili na atupe jibu kama je Lindi, Mtwara, Ruvuma itaingia katika *SAGCOT* au haingii?

Mheshimiwa Mwwenyekiti, nakuja katika barabara. Sasa hivi kero kubwa ya barabara ni kile kipande kidogo cha kutoka Nyamwage mpaka Somanga. Hivi kwa kweli Waziri wa Fedha anashindwa kutoa fedha kupeleka ili tukamaliza kile kipande, kero ikaisha? Miaka 50 mnashindwa nini kumaliza pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri ameingia katika *big and fast result now,* nataka ile barabara iishe. Maana yake hapa inatakiwa kupeana amri tu ili angalau tuone kweli haya yanayozungumzwa utekelezaji wake unakubalika au Mheshimiwa Waziri anataka kuja hapa kutupa furaha ambayo mwisho wake ni kilio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri kwa usikivu, aiangalie barabara ile kipande kile cha kutoka

Nyamwage mpaka Somanga ni sehemu ndogo imebakia pamalizike. Hii kero mojawapo itakuwa imekwisha na CCM tutazidi kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitangulize mapema mimi ni mdau katika Maliasili. Lakini tumepiga kelele kwa muda mrefu juu ya suala la *Wildlife* ya Niasa, Selous *Game Reserve.* Hapa kuna pato kubwa kuliko la *TANAPA*, kuliko la Ngorongoro, lakini limeshikwa na wajanja. Hii *wildlife* ni ya tembo kutoka Mozambique wanakuja Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa na takwimu tuliambiwa mwaka 1970 kulikuwa na tembo 2,000,000, sasa hivi kuna tembo 70,000. Hiki ni kilio na taarifa tunazopewa za *DNA test,* pembe zinazokamatwa Vietnam, Malaysia, Thailand, China zinatoka Selous. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hekima na taadhima kuna baadhi ya Wabunge wameshakuwa tayari kujitolea kusimamia hii. Tumieni nafasi hii ndogo tuliyokuwa tayari kujitolea tuisimamie Selous ijitegemee na Serikali itapata pato kubwa. Leo kuna viwanja vya ndege ndani ya Selous, ukikaa *Airport* toka asubuhi ni ndege zinaelekea Matambwe mapato yako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Selous ni mbuga kubwa, wale wanyama wanazunguka kutoka Mozambique, wakifika Tanzania kipindi cha uwindaji wanyama wamekwisha. Hivi kweli tunataka mapato au tunataka kuleta maneno?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wajanja waliokuwa ndani wana vurugu kiasi ambacho watakaposikia neno hili la Selous kwamba tunataka kusimamia hawatakubali. Maoni yetu tunaona kwa vile wimbi la wanyama linakwisha, tunaomba iwe *Conservation* inayojitegemea isiingie katika *Tanzania Game Authority.* Hapa tutongeza tena ubadhirifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwe *Conservation* itakayojitegemea kama Ngorongoro *Conservation,* basi na

*Selous Conservation Agency* iundwe mara moja ili ilete mapato katika nchi hii. Tusitegemee kila kitu tutakopa kukopa, kama una chako kwa nini ukope? Kwanza tunaaibika kuendelea kukopa wakati tuna chetu ambacho tukikiboresha tutatanua wigo wa mapato na mapato yatapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutapunguza masuala mengine madogo madogo na ujirani mwema, Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma watapata kwa kupitia *Selous Game Conservation Area.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napingana kidogo na baadhi ya wenzangu kusema kuna fujo ya wanyama. Mnyama kama binadamu ana mapito yake. Yale mapito wananchi wameyavamia na tembo kila mwaka anapopita lazima apite mle mle.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika maeneo yao mmejenga, mnaanza kulima, atapita wapi huyu mnyama? Maeneo yao mnamwinda, anakimbia ovyo ovyo, atakwenda wapi huyu mnyama? Mmeamua kumchanganya asijue anapopita, ndiyo anapita katika mashamba ya watu, lakini wakiwa ni wanyama wanaolindwa, wanaendelea kufanya vizuri kama ilivyo katika maeneo mengine kama Tarangire na kwingineko japo kuna kasoro ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali sikivu iangalie pato hili ambalo linapotea, liko mikononi mwa watu na ndani mna madini watu wanachimba sisi wenyewe tuko hapa tunafanya nini? Hii ni kero na ni aibu kuiona Selous ambayo imekuwa *established* mwaka 1870, Serengeti mwaka 1950. Selous ukubwa wake ni wa kwanza duniani, inafanya nini? Kweli tunasema nchi hii inataka kukopa wakati tuna kitu kikubwa ambacho kimekaa pale hakifanyiwi kazi na waliokuwa mle ndani wana kazi ya kukitumia. Hivyo ni hasara kubwa katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe wasikivu na tuachane na urasimu. Kama tunataka kwenda katika *big and fast*

*results;* nataka ninukuu kwanza *goals* zetu na *strategy, commitment, seriousness, monitoring and evaluation* viende sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haviendi sambamba hakuna maendeleo hapa. Itakuwa kila siku tunasoma makaratasi, tunaambiwa zitatolewa shilingi 50 itapelekwa katika *REA* haziendi. Waziri fuatilia hizi fedha zipatikane zisaidie kweli maendeleo ya umeme. Unaambiwa umeme...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili Mheshimiwa.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa Profesa Msola.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nianze kwa kuwapongeza sana wananchi wa Kilolo na hususan Kata ya Ng'ang'ange kwa kuhakikisha kwamba, ndugu Msuva amepita na kuwa Diwani kwa kupitia Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara ya Fedha kwa kuleta bajeti nzuri ambayo naiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono ningependa nijikite katika maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kipaumbele namba nne ambacho ni maendeleo ya rasilimali watu. Imetamkwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo kwamba ifikapo mwaka 2025, Tanzania tuwe na uchumi wa Kati, unaotegemea zaidi viwanda kuliko kilimo. Ni dhahiri basi kwamba, kama hiyo

ndiyo azma yetu ni lazima tusomeshe vijana wetu tupate wataalam ili azma hiyo iweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo azma, elimu yetu kwa sasa tumeangalia zaidi wingi kuliko ubora. Kupitia mpango wa MMEM na MMES, udahili katika ngazi zote za elimu umeongezeka sana kutoka elimu ya msingi, sekondari na vyuo vikuu, lakini ubora wa wahitimu kwa kweli uko mashakani na wote tumeona matokeo kwamba, vijana wetu wanahitimu lakini ubora wao ni kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuzungumza hapa wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu kwamba moja ya eneo kubwa ambalo litaleta ubora wa elimu katika nchi yetu ni ubora wa Walimu na mafunzo wanayopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wetu kwa sasa hivi wanatumia muda mwingi sana kujifunza *teaching methodology pedagogy* kuliko ile *subject matter* ambayo atakwenda kufundisha, kama ni wewe una-*specialize* kwenye *chemistry,* unatakiwa ujifunze uwe mbele ya mwanafunzi katika somo hilo. Lakini hili halifanyiki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudahili hawa Walimu nilizungumza wakati ule nikasema tuangalie mfano wa Finland, Singapore hata Malaysia wanafanya nini ili tupate vijana wazuri lakini na kazi yenyewe iwe ya kuvutia ili kusudi hawa vijana waweze kupewa mishahara mizuri zaidi. Kwa sasa hivi tunawakabidhi watoto wetu kwa watu ambao uwezo wao ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbaya zaidi kwenye upande wa sayansi udahili wa wanafunzi ni mdogo sana na hata wale wanaodahiliwa kwa upande wa sayansi kwenda hata katika vyuo vikuu ufaulu wao ni mdogo vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna haja ya kuangalia katika maeneo haya ili kuona kwamba, tunawapata vijana wengi na wanaofaulu vizuri. Mwaka huu Walimu wa sayansi waliokuwa wanahitajika walikuwa ni

29,000, lakini waliopatikana ni 2,000 tu, sawa na asilimia 6.7. Hii ni sehemu ndogo sana, bado kuna upungufu mkubwa wa Walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata katika vyuo vikuu, vijana wanaokwenda kuchukua masomo ya sayansi ni wachache. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina wanafunzi 16,000, wanaochukua masomo ya sayansi ni 4,000 tu. Chuo Kikuu cha Dodoma kina wanafunzi 14,000, wanaochukua masomo ya sayansi ni 3,400. Chuo cha Walimu *DUCE* kule Dar es Salaam kina wanafunzi 3,000, wanaochukua masomo ya sayansi ni 300 tu. *MUSE* kule Mkwawa, wanafunzi 2,000 na wanaochukua masomo ya sayansi ni 200 tu. Ni dhahiri kwamba, bila kuwa na mikakati mizuri hatuwezi kupiga hatua ya haraka katika maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa elimu ya ufundi, huko nako tuko nyuma. Tumekazania sana kusema kwamba mwanafunzi aende Chuo kikuu, ili apate digrii, lakini tunawatengeneza hawa ma-*genuine* wanaokwenda kutoka vyuo vikuu tunaacha hawa ambao ni wimbi la wafanyakazi kamili *technicians.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa naangalia Rais alipotembelea Singapore, aliezwa juu ya elimu ya Singapore. Kule wanachofanya si zaidi ya asilimia 25 wanaokwenda vyuo vikuu, lakini asilimia zaidi ya 75 wanakwenda kwenye *technical education.* Hawa ndiyo wafanyakazi na hili ndiyo lengo ambalo tulilokuwa tunalitazamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hayo machache niliyosema mimi nina ushauri ufuatao:-

Kwanza tutenge fedha za kutosha ili kujenga idadi kubwa ya wanasayansi katika jamii yetu (*a critical mass of scientists). (Makofi)*

Pili, tunasema *big results now* jambo ambalo tunalikopi kutoka Malaysia. Napenda kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge, ile *big results* ya Malaysia, walichotanguliza wao

ni elimu katika sayansi na teknolojia kwanza. Hiyo ndiyo baadaye ikaja kutumika kupata hizo *big results,* hawakuanza na *big results* halafu ndiyo waende kwenye sayansi. Kwa hiyo, naona tumekwenda kinyume kidogo, ni vema tukafuata hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hapa Bungeni tuna Kamati nyingi sana. Sayansi na teknolojia iko chini ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, hazina uhusiano. Nashauri kwamba Bunge liunde Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kusudi iweze kupata nafasi nzuri zaidi. Zamani tulikuwa na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, ikarudishwa na kuunganishwa na Elimu ya Msingi na Sekondari ambako tayari kuna matatizo ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iirudishe tena Elimu ya Juu iwe Wizara pekee ili kusudi ipate nafasi ya kuendeleza sayansi na utafiti, maana huko ndiko vilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia utafiti, mwaka 2010/2011, tuliomba Serikali itenge fedha kufikia asilimia moja kwa ajili ya utafiti na maendeleo. Wakati ule ikatajwa kwamba Serikali itatengwa bilioni 30, lakini hazikupatikana zote, zilipatikana bilioni 15. Mwaka unaofuata bilioni saba, mwaka huu tunaomalizia ni bilioni 5.6. Nchi zote ambazo tunaona zimeendelea ni kwamba, wamewekeza zaidi kwenye elimu na kwenye utafiti na maendeleo. Sisi haya yote tumeyaweka pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana hata kuona kwamba Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia bajeti yake imekuwa ikishuka mwaka hadi mwaka, kiasi kwamba hawawezi kutekeleza majukumu makubwa. Ndugu zangu Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ndiyo nyenzo kubwa ya kuleta maendeleo ya haraka katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna somo hili la TEHAMA. Ushauri wangu ni kwamba, kama tunatenga bajeti kubwa kwa mambo mengine tutaachwa nyuma kama TEHAMA haifundishwi vya kutosha. Siku hizi kuna vikomputa vidogo

vinavyotumia *solar power* ambavyo ukiweza kutenga bajeti hata awamu kwa awamu, vijana wetu wataweza kusoma hili somo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za jirani kama Rwanda hata Kenya wameanza utaratibu huu. Kwa nini tusitenge bajeti ya kutosha katika maeneo hayo ili kusudi tuweze kuwa na Taifa la ushindani. Sasa tutazungumza mambo yote haya hata ya maji, lakini bila kuwa na wataalam wa kwetu hatutafika mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kumekuweko na ongezeko la bajeti katika maeneo mbalimbali. Napenda kuipongeza sana Serikali na utaratibu wa bajeti wa mzunguko huu kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa sikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye ongezeko la bajeti, katika Wilaya yangu, sehemu kubwa ni kilio kikubwa cha maji hasa katika Mji Mdogo wa Ilula. Ni mategemeo yangu kwamba, Wizara imeyasikia haya na kwamba itapewa kipaumbele. Vile vile tuna matatizo ya umeme katika vijiji mbalimbali kama walivyoeleza watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna tatizo la utengenezaji wa madawa hapa nchini. Malighafi inayoletwa kwa ajili ya kutengeneza madawa ya wanadamu hazitozwi kodi yoyote, lakini malighafi ambayo inatumika kutengeneza madawa ya mifugo inapoingizwa nchini inatozwa kodi kubwa. Wakati madawa hayo hayo yakiletwa yametengenezwa ng'ambo hayatozwi kodi, lakini malighafi ya kutengeneza madawa ya mifugo inapoletwa hapa nchini inatozwa kodi na wananchi wanapata madawa haya kwa gharama kubwa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona muda uliobaki ni dakika tano ambazo, Mheshimiwa Machali vipi tena?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Utaratibu gani tena? Haya kuhusu utaratibu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(g) ambayo inasema naomba ninukuu: "Kwamba Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine".

Leo asubuhi Mheshimiwa Mwenyekiti, kulitokea hali ya mimi kutofautiana na Kiti. Lugha kidogo ambayo ilitumika haikuwa nzuri na kwa kuwa baadhi yetu sisi Watanzania ni *Statesmen* na siku zote huwa tunapenda kusimamia ukweli lakini pia kuweza kuheshimiana na kwa kuwa nilikuwa *provoked* na Mbunge mwenzangu ndiyo ikaja kupelekea hali ile, naomba niyaondoe yale maneno ambayo niliyatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kuweza kuwasihi Waheshimiwa Wabunge tujaribu kuwa tunavumiliana. Maana yake unaweza ukakuta wakati mwingine Mbunge anazungumza, unasikia wengine wanaguna na kuonesha ishara za kejeli pamoja na dharau, hali ambayo kwa kweli wakati mwingine uvumilivu unakosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaweza tukawa ni watu wa kuangalia kwamba tuko hapa kwa sababu ya nini? Haya hayawezi yakaendelea kufanyika ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba niishie hapo. Ni imani yangu kwamba, hata Mbunge ambaye ameni-*provoke* namheshimu sana, naye anaweza

akapima mwenyewe kwa dhamira yake na kwa nafsi yake alichokifanya kilikuwa ni *fair* au laa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, napokea Mwongozo huo wa Mheshimiwa Machali na naomba niendelee kusema Waheshimiwa Wabunge, Kiti na hata mimi mwenyewe binafsi nimekuwa nikisema sana, tujenge tabia ya kuheshimiana ndani ya Bunge.

Mara nyingi Mbunge anapopata nafasi ya kuzungumza, iwe Mbunge yeyote au Waziri ama Kiongozi mwingine yeyote akitumia nafasi hiyo ama kwa matendo au kwa maneno ku-*provoke* kile ambacho kinaendelea iwe kwa Mbunge kwenda kwa Waziri ama Waziri kwenda kwa Mbunge au Mbunge kwa Mbunge mwenzake mara nyingi tunasababisha mitafaruku isiyo ya lazima ndani ya Bunge.

Kwa kitendo hicho Mheshimiwa Machali naomba nikupongeze sana. Nikupongeze sana na naamini kabisa vijana waliomo ndani ya Bunge hili kama watajifunza kwa mfano mzuri alioufanya Mheshimiwa Machali leo, Bunge hili litajenga heshima kubwa kwa vijana wa Tanzania na kwa Viongozi wanaotegemewa na nchi hii wajao.

Mheshimiwa Machali umeonesha uzalendo wa hali ya juu na naomba sana kwa kila Mbunge ambaye anaona amemkosea mwenzake, uungwana ni kitendo na kila Mbunge achukue nafasi ya kupima kila anapofanya makosa na kutumia nafasi hii ya Bunge kuomba msamaha katika yale yanayotokea.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwaagize *Hansard* wafute yale maneno yote ambayo hayakuwa yakistahili katika kipindi cha leo. Turudi katika heshima yetu ya Bunge na tuendelee kuchangia michango ndani ya Bunge kwa maslahi ya wananchi na siyo kwa kuleta vurugu na kusababisha kero kwa Mbunge mwingine ama kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Machali nakushukuru sana na nakupongeza sana kwa uzalendo mkubwa na heshima uliyoionesha kwa umri wako ndani ya Bunge hili kwa siku hii ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji imekwisha iliyokuwa hapa Mezani leo. Yako baadhi ya majina yamebakia, lakini tutaendelea nayo kesho. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii niahirishe shughuli za Bunge mpaka kesho, saa tatu asubuhi ndani ya Ukumbi wa Bunge.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku yaJumatano, Tarehe 19 Juni, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*